ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili – Tarehe 16 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: *"Bismilah Rahman Rahim"* Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Nembo namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera namba 12 ya mwaka 2004 na kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar wa mwaka 2016 na Mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Waheshimiwa Wajumbe sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa niaba ya Mwenyekiti Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Simai Mohammed Said: (Kny) **Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa napenda kuwasilisha mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Nembo Na. 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya 2004 na kutunga Sheria inayoweka Masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 65

Kudhibiti uhalifu nyakati za usiku

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza**:**

Limeibuka kundi la vijana wa kihuni ambao wamekuwa wakifanya vitendo vya kijambazi katika barabara ya Amani – Mtoni na eneo la njia ya Chumbuni kwa kuwaibia, kuwapiga na kuwadhalilisha watu hasa wanawake nyakati za usiku.

(a) Je, serikali inalitambua tatizo hilo.

(b) Ni lini serikali itaweka taa katika barabara ya Amani-Mtoni ili kupunguza vitendo hivyo viovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 65 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inatambua kuibuka kwa kundi la vijana wa kihuni ambao wamekuwa wakifanya vitendo vya kijambazi katika barabara ya Amani-Mtoni na eneo la njia ya Chumbuni, ndio maana Jeshi la Polisi linachukua juhudi ya kufanya msako kwa lengo la kuwakamata wahusika kama nilivyojibu katika swali la msingi nambari 44 la tarehe 15/02/2017.

(b) Mhe. Spika, Manispaa ya Wilaya ya Mjini kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inakusudia kuweka taa za barabarani kupitia mradi wa uwekaji taa awamu ya pili ambao unatarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China ikiwemo barabara ya Amani hadi mtoni.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Mradi huo, tarehe 25 Novemba 2016 Manispaa Mjini kupitia Wizara ya Fedha imepokea wataalamu elekezi kutoka Kampuni ya *SIPPR* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu yaani *Feasibility study* katika barabara zenye jumla ya urefu wa km 15.036 kama zifuatazo:-

Mhe. Spika, Uwekaji wa taa za barabarani kutoka Malindi hadi kwa Nyanya yaani *Malawi road* yenye urefu wa km 11 sawa na jumla ya taa 315.

Mhe. Spika, Uwekaji wa taa za barabarani kutoka Mtoni hadi Amani yaani *Mkapa raod* yenye urefu wa km 4.036 sawa na jumla ya taa 115. Mhe. Spika, nashukuru.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Spika, ni lini Barabara ya Mtoni-Amani itatengenezwa tena itatiwa lami sehemu ambazo kuwa zimechimbwa ilipokuwa inapita ile mitaro ambayo iliokuwa imeelekea karakana ya maji. Ni lini zitatiwa lami zile barabara kwa sababu zinaleta ajali sana katika misingi iliyotiwa vifusi tu ile bila ya kutiwa lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, serikali ilikamilisha mradi wa ujenzi wa barabara ya *Mkapa road* kwa kiwango cha kwanza. Lakini kutokana na maboresho ya kuweka *system* za maji kuwa katika mfumo uliokuwa bora zaidi ilitegemea na niliona makusudio ya kukata njia ile ili kupisha ujenzi wa aina ile. Mara ujenzi utakapokamilika tunaamini barabara ile itakamishwa na kurudi katika hatua yake ya awali. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa hawa wahali sio mara nyingi kukaa katika barabara ambapo Mhe. Waziri amejibu kwamba *solution* ni kwamba barabara zote zimewekwa taa mara nyingi sana hawa hukaa mitaani kama Mboriborini, Kwamtipura, Karakana.

(a) Je, serikali ina mkakati gani sasa wa kuona kwamba wanapeleka vile vikosi ambavyo vinafanya doria na ambavyo mara nyingi huonekana maeneo ya mjini kama Michenzani, Mlandege baada ya kwenda huko ambapo kuna shida za ulinzi.

(b) Je, serikali inakuja na mkakati gani sasa wa muda mrefu ambao utahakikisha usalama wa raia wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, serikali ina mkakati wa muda mrefu katika kuhakikisha suala zima la amani linapatikana katika maeneo yetu. Lakini kwa nini tumefikiria kuweka taa. Niseme kama nilivyojibu katika jibu letu la msingi tulitaka kuweka taa kwa hatua ya awali wale ambao walikuwa wanakuja kufanya uhalifu katika maeneo ya barabarani wataenda katika maeneo mengine.

Lakini hata katika maeneo yale Kwamtipura, Darajabovu na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mjumbe ameyataja serikali imekuwa ikiimarisha kila siku ulinzi kupitia vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama, ulinzi wa kwa miguu katika mitaa yetu yote hii, ndio maana unapoona leo wapo mjini lakini muda huo huo inawezekana wakawa wapo Chumbuni na ukiwaona wako Chumbuni inawezekana muda huo huo ukawaona wapo katika eneo la Kwamtipura.

Dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanakaa katika hali nzuri yenye usalama na amani. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kutokana na hali ya hatari katika maeneo ya Chumbuni, Mtoni na Amani na sehemu nyengine. Lakini vile vile kumekuwa na hali ya kutokuwa na usalama katika maeneo ya barabara ya Maisara kupitia barabara ya Mzee Ali Hassan Mwinyi hadi Mafunzo.

Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa salama na vile vile kuweka taa katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama vile nilivyozungumza awali katika jibu langu la msingi. Jukumu kubwa la serikali katika nchi yake na taifa lake kwanza ni kuhakikisha wananchi wake wanakaa katika hali ya amani na utulivu wanapata kufanya shuhuli zao za kula siku katika maisha yao.

Lakini pia kama ambavyo nimezungumza tena kwamba serikali hivi sasa katika kila sehemu ambayo imekuwa ikisikika na hata zisizosikika zimekuwa na uvunjifu wa amani kwa namna moja ama nyengine inekuwa ikiongeza ulinzi wa doria kadiri ambavyo nafasi inaweza kuruhusu, ndio maana leo serikali jukumu hili la ulinzi si tu idara moja ambayo imeachiwa. Ni vyema idara zote za serikali ambazo zinahusiana na ulinzi zimepata fursa na ziko sambamba katika kuhakikisha wananchi wetu wanakuwa katika hali nzima ya amani na utulivu katika maeneo yao. Nashukuru Mhe. Spika.

Nam. 111

Mashahidi wa mahakama kutolipwa posho zao

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza**:-**
Mashahidi ni sehemu moja muhimu sana katika kesi lakini kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya mashahidi kutokulipwa posho zao.

(a) Je, ni mashahidi wangapi wanaoidai Mahkama na ni kiasi gani wanazodai.

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa mashahidi hao posho zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 111 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba mashahidi ni muhimu sana katika uendeshaji wa kesi na upatikanaji wa haki mfumo wa kimahkama. Kwa mujibu wa kumbukumbu zetu, tunao jumla ya mashahidi 53 wanaoidai Mahkama posho la ushahidi. Aidha fedha zilizotengwa kuwalipa Mashahidi ni wastani wa Tsh 4,500,000/= kwa mwezi kupitia Idara ya Mahkama.

(b) Mhe. Spika, serikali inaendela kuwalipa mashahidi fedha zao za posho la ushahidi kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. Hadi hivi sasa mashahidi hao wanadai pesa za miezi mitatu (3) ambazo wataendelea kulipwa kupitia fedha za matumizi mengine yaani *other charges*.

(a) **Mhe. Shehe Hamad Mattar:** Mhe. Spika, je, idadi hii ya mashahidi 53 ni wangapi wa Unguja na wangapi wa Pemba na pia idadi hii ya Tsh. 4,500,000/= zilizolipwa je, Unguja ni kwa ajili ya Mahakama Kuu Unguja tu au pamoja na Pemba.

(b) Ni mkakati gani uliouweka wizara yako katika kuhakikisha bajeti inayofuata suala hili linapewa kipaumbele ili kusukuma kesi ambazo zimekaa Mahakamani bila ya kuendelezwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

(a) Mhe. Spika, idadi ambayo niliyotowa ni ya Unguja na Pemba, sasa kujua idadi Pemba ni wangapi na Unguja ni ngapi hilo nitamletea *inshaallah* kwa njia ya maandishi.

(b) Pesa zilizolipwa hizi idadi ya Tsh 4,500,000/= idadi hii ni kwa Unguja na Pemba. Halafu kuhusiana na suala la mikakati ili kuweza hao

mashahidi tuweze kuwamalizia hayo mafao yao. Mikakati ipo na tuko mbioni kuhakikisha kwamba ifikapo kipindi kijacho cha miezi michache ijayo mashahidi hawa wawe tayari fedha zao hizi wameshalipwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, Mhe. Waziri umetwambia kwamba kuna mashahidi ambao wanapaswa kulipwa posho na serikali.

(a) Je, ni mashahidi wa aina gani ambao wanapaswa kulipwa posho na utufafanulie utwambie hawa mashahidi ambao wanapaswa kulipwa hilo posho na serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, mashahidi ambao huwa tunawalipa hili posho kuna aina mbali mbali ya mashahidi na ulipwaji wa posho wao unategemea vile vile aina ya mashahidi hao. Kwa mfano mashahidi wa kawaida huwa tunawalipa posho la shilingi 800 pamoja na nauli ya kule ambako anakotoka. Mashahidi wengine kwa mfano wale wataalamu madaktari na watu wengine wenye sifa za kitaalamu hawa tunapowaita katika mahakama zetu hawa tunawalipa posho la shilingi kumi na tano elfu.

Sambamba na hilo tuweze kuelewa kwamba pamoja na posho wanalopewa pia wanapewa nauli zao kulingana na sehemu zile ambazo husika. Kwa mfano anaetoka Tanzania Bara mikoani tafauti na yule ambaye ametoka mjini Magomeni au sehemu nyengine ya hapa Unguja au Pemba.

Halkadhalika mtu ambaye anaetoka pengine Canada kwa kuwa tunamuhitaji kwa kutoa ushahidi nae pia tunapata fursa hiyo ya kumwita kule nae anakuja kutoa ushahidi pale ambapo unahitajika na vile vile posho lake litategemea kulingana na ile sehemu ambayo husika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, tumeshuhudia kwamba kuna kesi nyingi ambazo kwa utaratibu mzima wa kulipwa nauli au posho unashindikana na watu huwa hawaendi kutoa ushahidi. Kwa kuzingatia kwamba katika mwaka mzima uliopita Mahakama zetu au Mahakama yetu kuu kwa utaratibu wake imelipa milioni nne laki tano.

Je. Mahakama za wilaya zina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kuna kesi nyingi kuliko hata mjini baadhi ya wakati zinashindikana wananchi kulipwa posho la nauli na posho maalum, lina utaratibu gani wa kulifanya hili ili liendelee na kuto hizo fedha kwa ajili ya maendeleo ya kesi hizo zishe haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, Naomba nimjulishe Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kwamba zoezi hili la kulipa mashahidi huwa halichagui aina gani ya Mahakama, kwa hivyo kama tunaamua kulipa mashahidi tunalipa mashahidi wote bila ya kujali Mahakama gani, kwa hivyo mashahidi huwa tunawalipa wote na sio kwamba Mahakama kuu tu ndio tunalipa mashahidi na Mahakama ya wilaya tunaacha hapana. Kwa hivyo zoezi hili la ulipwaji wa mashahidi huwa tunalifanya katika Mahakama zote, lakini sambamba na hilo tutajitahidi kwamba mashahidi wote hawa tuwe tunawaharakishia kupata hili posho lao ili waweze kupata urahisi zaidi kuja Mahakama kusaidia ili haki iendelee kutolewa zaidi katika Mahakama zetu. Ahsante.

Nam. 105

Vigezo vya Kuanzishwa Manispaa

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa kuanzisha Manispaa kunahitaji kuwepo wadi 15. Na kwa kuwa hivi sasa kumeanzishwa Manispaa 2, ya Magharibi ‘A’ na Magharibi ‘B’ ambazo kuanzishwa kwake hazikukidhi matakwa ya Kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji na Mabaraza ya Miji.

(a) Je, ni kigezo gani kimetumika kuanzisha Manispaa ya Magharibi ‘A’ na ‘B’ wakati inajulikana kwamba zilizokuwa Halmashauri ya Magharibi ‘A’ na ‘B’ wadi zake hazifikii kiwango cha uanzishwaji wa Manispaa hizo.

(b) Je, Wizara haioni kwamba kuanzisha Manispaa zaidi ni kuongeza gharama wakati mapato yanayopatikana kwa sasa hayataweza kukidhi gharama za uendeshaji wa Manispaa hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.105 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Mabaraza ya Manispaa ya Magharibi ‘A’ na ‘B’ yameanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014 sambamba na Kifungu cha

33(b) cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali Nam. 5 ya Mwaka 2016 kinachoeleza kuwa "*Baraza la Manispaa litakuwa ni chombo kinachojitegemea, litagaiwa kwa idadi ya Wadi kama itakavyoamuliwa na Waziri kwa mujibu wa sifa kama ilivyoelezwa katika Jadueli la pili la Sheria hii".* Aidha, uanzishaji wa Mabaraza hayo pia umezingatia vigezo vilivyoainishwa katika jadueli la Pili la Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014. Vigezo hivyo ni:-

i. Idadi ya wakaazi kuanzia 150,000 hadi 300,000;
ii. Kuwepo kwa angalau nusu ya wakaazi wake wanaoishi maeneo yenye miundombinu ya kijamii na kiuchumi;
iii. Kuwepo kwa sehemu za kupumzikia *(Recreational Centres);* na
iv. Kuwepo kwa Ofisi za Serikali.

(b) Mhe. Spika, kwa kuzingatia kuwa, uanzishaji wa Mabaraza hayo umekidhi vigezo nilivyoviainisha katika majibu ya swali hili ya kifungu (a) na kwa kuzingatia vyanzo vya mapato vya Halmashauri vilivyoainishwa katika Kifungu cha 70 cha Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ haioni kwamba uazishwaji wa Manispaa hizo utaongeza gharama za uendeshaji kwa sababu kila Manispaa inavyo vyanzo vyake vya mapato inavyojitegemea. Kwa Mfano katika kipindi cha Oktoba – Disemba 2015/2016 Manispaa ya Magharibi 'A' ilikadiria kukusanya TZS. 97,018,550/- ambapo hadi kufikia Disemba Manispaa hiyo ilikuwa tayari imekusanya jumla ya TZS. 49,144,000/- sawa na asilimia 51 ya lengo lililopangwa. Kwa upande wa Manispaa ya Magharibi 'B' katika kipindi cha Oktoba – Disemba 2015/2016 Manispaa hiyo ililenga kukusanya jumla ya TZS. 341,089,400/- na hadi kufikia Disemba jumla ya TZS. 263,513,441/- sawa na asilimia 78 ya lengo zilikuwa tayari zimekusanywa na Manispaa hiyo.

Mhe. Spika, takwimu hizi zinaonesha mwelekeo wa namna ambavyo hali ya ukusanyaji wa mapato katika Manispaa hizi mpya utakavyoimarika. Juhudi ambazo Ofisi yangu imekuwa ikisisitiza ni pamoja na bidii na uadilifu katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kuzitaka Manispaa na Mabaraza yote kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na

Idara Maalum za SMZ inaendelea na matayarisho ya kuelekea katika mfumo wa ukusanyaji kwa njia ya elektroniki jambo ambalo kufanikiwa kwake kutasaidia kupunguza uvujaji wa mapato.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa tena nafasi ya kumuuliza Mhe.Waziri suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa sababu umetoa mfano wa Halmashauri ya Magharibi (A) ambayo kwa miazi mitatu imekadiria kukusanya Shs. 97, 018,550 na hadi kufikia Disemba ilikuwa imekusanya Shilingi milioni 49 sawa na asilimia 51%. Sasa suali langu liko hapa.

a) Je, ni gharama gani ambazo Halmashauri hizi za Wilaya au Mabaraza ya Manispaa hizi zinatumia kwa kila mwezi.

b) Je, hizi Manispaa zina vianzio vingapi ambavyo ni vya mapato ya uhakika vinavyopata kwa kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Alitaka kujua ni gharam gani ambazo zinatumia baada ya yale makusanyo au zimepanga kutumia Halmashauri zetu.

Mhe. Mjumbe suali hili linahitaji takwimu na kwa vile takwimu hizo kwa sasa hivi hazipo naomba nimjibu kwamba takwimu hizi nitaziwasilisha kwa maandishi.

Lakini vile vile vianzo vya mapato katika Manispaa zetu viko vya namna nyingi, au viko vya aina mbali mbali inategemea ni Baraza gani au sehemu gani ambapo Halmashauri yetu au Baraza letu lipo katika maeneo yale na fursa ambazo zilizokuwepo, lakini kwa mfano miongoni mwa vyanzo vya mapato ambavyo tunakuwa tunavitumia ni kukusanya kodi za maegesho ya magari ambayo yanalihusu Baraza, ukusanyaji wa maliasilia ambazo ziko katika maeneo yaliyozunguka katika Mabaraza na Manispaa zetu, vile vile kodi za biashara ambazo zipo katika kila maeneo katika Mabaraza yetu yamekuwa yakipatikana na vyengine vinavyofanana na hivyo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Mhe. Spika, kabla ya kuuliza suala kwanza naomba niwapongeze sana watendaji wa Wilaya ya Magharibi (A) kuanzia Mstahiki Meya na Mkurugenzi pamoja na Madiwani wote kwamba ni watu makini.

Lakini pamoja na pongezi zangu hizo sote tunaelewa kwamba Manispa (A) na (B) zaidi (A) ni mpya kabisa na kwasababu ni mpya hata malengo yake ya kukusanya mapato haiwezekani mwaka wa mwanzo wakafanikiwa, suala langu liko hapa.

Manispaa ile haina miundombinu ya Majengo, haina masoko, haina kituo cha daladala, na pia majimbo yote ya Wilaya ile yana matatizo sana barabara za ndani *feeder road* pamoja na maji safi na salama.

Je, Wizara yako itaisaidia vipi Manispaa ile kuhakikisha kwamba katika mwaka huu wa fedha wanalizingatia sana kuwepo kwa barabara za ndani *feeder road*, maji safi na salama lakini pia kulitumia vizuri eneo la Kwa Nyanya kujenga soko, kituoa cha dala dala na Ofisi zao Manispaa ili kuwa katika hali nzuri ya kimapato.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ukweli ni kwamba naungana nae kwamba Baraza la Manispaa la Magharibi (A) ni baraza jipya na kwa sasa bado ni kwamba kuna baadhi ya miundombinu yake haijakaa vizuri, lakini pamoja na hivyo naomba nimwambie Mheshimiwa kwamba dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara hii dhamira yake ni kuhakikisha kwamba katika mabaraza yake yote ni kwamba tunafanikiwa katika kupeleka huduma zikiwemo miundombinu na maji safi na salama na huduma nyengine zinazohitajika katika maeneo husika.

Hivyo basi katika mikakati ya Wizara itahakikisha kwamba kila linaloonekana kwamba lina maslahi kwa wananchi katika maeneo ya Mabaraza yetu basi tutahakikisha kwamba tunatumia nguvu kubwa kuona kwamba huduma zinapelekwa kwa mujibu wa mahitaji ya wananchi kama ambavyo yanahitajika katika maeneo yale.

Kuhusu mikakati basi tutahakikisha kwamba mikakati madhubu ya Wizara pamoja na ushauri na mashirikiano ya watu wengine basi tutahakikisha kwamba tunaboresha kwa kadri hali itakavyokuwa inaruhusu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba niulize suala moja dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, wakati tunapitisha sheria hii ya kuanzisha hizi Manispaa Mhe. Waziri aliongea mengi na kutupa malengo pamoja na yale ambayo yote

tungeweza kufaidika kwa pamoja katika nchi yetu, barabara ya kutoka Kiembesamaki, kupitia Mwanakwerekwe mpaka Amani ni barabara moja ambayo inatumika na watu wengi, hata viongozi wetu wakuu wa kitaifa wanatumia barabara hii pamoja na wananchi wengi ili kupata huduma, lakini maka nenda miaka rudi barabara hii imejaa michanga, taka pamoja na mazogo mengi ambayo hupelekea wakati mwengine kuleta adha kwa wananchi wanaoishi katika mazingira hayo lakini pia wale wanaotumia ile huduma.

a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaboresha na kuisafisha barabara hii hasa michanga na vumbi yanayokuwepo barabarani ili kutokomeza kwa miaka na miezi yote kwa siku za mbele zitakazokuja.

b) Katika masoko yetu kumekuwa kuna taka, vyakula na mambo mengi yanafanyika lakini pia masoko haya yamekuwa hapapigwi madawa wakati wa usiku baada ya huduma za uuzaji au kutoa hizo huduma kwa wananchi, ili kuondoa au kuboresha maisha ya watu.

   Sasa Je, Serikali itatumia njia gani kupiga madawa hasa kama njia ya *farmigation* ili kuboresha masoko haya na huduma ambazo zinapatikana katika haya masoko makuu hasa ya Mwanakwerekwe pamoja na soko la Darajani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa nakiri kwamba katika suala la masoko katika maeneo ambayo tumeyataja kwamba inawezekana hali hiyo uliyoizungumzia ipo katika masoko yetu katika Mabaraza yetu ambayo yametuzunguruka katika maeneo hayo, lakini naomba nichukue kama umetukumbusha jukumu letu na kwa kadri inavyokuwa inatokezea shughuli za usafi zimekuwa zikiimarishwa kwa kadri hali inavyowezekana.

Lakini kutokana na hali ya wananchi wetu baadhi ya wakati imekuwa ni vigumu katika kupokea maagizo mbali mbali ambayo yanakuwa tukipewa na taasisi zetu hizi na badala yake kupelekea kutumia nguvu kubwa na taaluma kubwa katika kuona basi hawataki kubadilika kwa kiasi fulani, lakini pamoja na hayo tutahakikisha kwamba hali ya usafi katika maeneo hayo inadumishwa wakati wote baada ya kuona kwamba tunatengeneza biashara, lakini pamoja na kulinda afya za wananchi wetu ili wasije wakapata madhara zaidi. Kwa hivyo nilichukue hili Mheshimiwa kwamba tutalifanyia kazi kwa kadri hali itakavyokuwa inaonekana inafaa.

Lakini vile vile suala la kurundikana kwa michanga katika barabara ya Kiembesamaki mpaka Amani hili bado nalo pia niseme kwamba ni ushauri au umetukumbusha wajibu wetu, hatujabaini ipasavyo kwamba hilo tatizo lipo lakini kama lipo basi tunakuhakikishia kwamba kwa vile ni jukumu letu tutahakikisha udhia wote uliomo barabarani tunaiondoa ili wananchi pamoja na viongozi wetu waweze kupita katika hali ya usalama zaidi bila ya usumbufu wa aina yoyote.

Nam. 5

Mafunzo ya Kompyuta kwa Wanafunzi

Mhe. Ali Khamis Bakari – Aliuliza

Naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuiboresha sekta ya elimu kwa kuwatoa Walimu maalum kutoka Nigeria kuja kufundisha masomo ya Sayansi Unguja na Pemba kama vile (Utaani, Wete, Chwaka, Tumbe, Konde Sekondari, Pandani, Mchanga Mdogo Sekondari na Kijichi Unguja).

(a) Je pamoja na jitihada hizo kwenye masomo ya Sayansi, kwa nini Wizara haiweki Walimu maalum wa kufundisha Kompyuta katika Skuli za Serikali ambazo hazina wataalamu hao.

(b) Wizara ina mpango gani wa kutoa mafunzo hayo ya kompyuta badala ya wanafunzi kumaliza masomo na kujiunga vyuo binafsi kwa kufuata huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake Nama 5, lenye sehemu (a) na (b).

Kwanza napenda kuanza kwa kutoa maelezo ya utangulizi.

Walimu wa kujitolea kutoka Nigeria wamekuja nchini kwa makubaliano Baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Nigeria, Walimu wa kujitolea 38 wa masomo ya Sayansi na Hesabati wapo nchini kwa mkataba wa miaka miwili wamepangiwa kazi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu; mjini na vijijini, Walimu 32 walifika nchini tarehe 19 Febaruari, 2015 na

mkataba huo unamalizika tarehe 18 Februari, 2017 na wataondoka kurejea makwao. Kuweko kwao kumesaidia sana kupunguza tatizo la Walimu wa masomo hayo katika ngazi ya Sekondari na Skuli nyingi zimenufaika na usomeshaji wao. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa somo la Komputa lina umuhimu mkubwa hasa kwa wakati huu ambapo dunia imepiga haatua kubwa katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. *TEHAMA* inatumika katika nchi nyingi kama nyenzo muhimu ya kufundishia na kujifunzia na kumwezesha mwalimu mmoja kufundisha wanafunzi wengi wakati mmoja na katika maeneo tofauti. Pia, matumizi ya *TEHAMA* yameweza kuwarahisishia wanafunzi kupata maarifa mapya na taarifa muhimu za kuwasaidia wanafunzi kupata maarifa mapya na taarifa muhimu za kuwasaidia katika masomo yao na hivyo kuweza kuongeza maarifa na ujuzi wao.

b) Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa somo la kompyuta linafundishwa katika Skuli zetu. Kutokana na umuhimu wake, Wizara imeandaa mitaala ya somo la *TEHAMA* kwa ajili ya elimu ya msingi kuanzia darasa la tano na kwa Skuli za Sekondari. Pia somo hilo linafundishwa katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu vyetu. Katika ngazi ya Sekondari, zipo Skuli sita zinazosomesha somo hilo. Skuli hizo ni Skuli ya Sekondari ya Biashara iliyopo Mombasa, Benbella, Mikunguni, Kiembesamaki na Mikindani kwa Unguja na Skuli ya Chasasa kwa Pemba.

   Wizara inakusudia kuanzisha usomeshaji wa somo hilo katika Skuli mpya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Matangazo ya Elimu na Skuli ya Muhammed Juma Pindua iliyokuwepo Mkanyageni Pemba. Skuli hizo tayari zimeshapatiwa walimu na kompyuta za kutosha kwa ajili ya kufundishia na kwa matumizi ya walimu. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kwa kuwatoa walimu hawa wa masomo ya sayansi na kuwaleta nchini ili kuendeleza zaidi nchi yetu kimaendeleo na kupata wataalamu zaidi, lakini yameachwa masomo ya art. Je, Wizara haiyoni tutakosa

baadhi ya wataalamu wa masomo ya *art* kwa mfano, wanasheria, wanadiplomasia hapo baadae.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Wizara ya Elimu bado haijapuuza somo lolote katika usomeshaji wake. Napenda kumuhakikishia kwamba katika masomo ya *art* yakiwemo historia, *geography*, na masomo ya lugha kiingereza, kiswahili na mengineyo, haya yanasomeshwa katika ngazi zote za serikali, sekondari ya kawaida na Sekondari ya juu na bahati nzuri walimu wa aina hii tunao wa kutosha hapa Zanzibar. Kwa hivyo hakuna tatizo hilo na masomo haya yanasomeshwa kwa uzito sawa na sisi Wizara tunapitia kuhakikisha kwamba masomo haya yanasomeshwa kwa sababu ndio msingi wa kupata wana taaluma wengine ambao hawatokani na fani ya sayansi, Wizara itaendelea kusomesha masomo haya.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Mhe. Spika, namuomba nimuulize swali la nyongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Je, Wizara ya Elimu imeshawahi kufanya tathmini juu ya wanafunzi wetu baada ya kupata elimu hii kutoka kwa walimu hawa wa kigeni na ni maendeleo gani yaliyopatikana kwa kuja kwa walimu hawa wa kigeni kutoka Nigeria.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Wizara ya Elimu tayari imeshafanya tathmini na tathmini inaonyesha kwamba walimu hawa wameleta mchango mkubwa sana katika masomo ya sayansi. Tathmini hiyo inaelezwa kwamba pia kuwepo kwa walimu wa Nigeria kuliweza pia kuwaathiri walimu wetu wa ndani kuweza kufanya kazi vizuri zaidi. Wameshawishika baada ya kuona wenzao namna wanavyofanya kazi na wao pia wameanza kuiga. Taarifa hizi tumezipata kutokana na ripoti ya walimu wenyewe wa Nigeria lakini pia na walimu wetu, kwa hivyo wamesaidia sana kujenga misingi ya kisayansi.

Lakini pia walimu hawa wamesaidia sana katika kutushauri sisi Wizara ya Elimu namna ya kufatilia usomeshaji wao wenyewe wa Nigeria tufanya nini ili kuweza kuona na wao wanawajibika kiasi gani, pia wametusaidia na ripoti zetu pia zimeonyesha kitu kama hicho. Lakini pia wameweza kusaidia baadhi ya sehemu kuhamasisha wale vijana kupenda kusoma sayansi kwa kuanzisha mashindano ya kisayansi, hasa Pemba wameanzisha kitu wanaita *annual science competition* katika Wilaya zote za Pemba. Ahsante

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ambayo sijaridhika nayo sana naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

a) Hivi haiyoni kwamba serikali kuleta walimu kutoka Nigeria ni kuitia gharama zisizokuwa za umuhimu serikali badala yake tu kuweza kuchukua walimu kutoka Tanzania Bara.

b) Naomba Mhe. Naibu Waziri atupe takwimu halisi kwamba tokea wafike walimu kutoka Nigeria kwa kiwango gani elimu yetu ya Zanzibar imepanda na kwa kiwango gani elimu yetu ya Zanzibar imeshuka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

a) Mhe. Spika, sisi tunahisi kwamba kuchukua walimu kutoka Nigeria ni suala ambalo linaumuhimu wa aina mbili. Kuna umuhimu wa kidiplomasia, yaani kujenga uhusiano na wenzetu, lakini pia kubadilishana uzoefu na mbinu katika kusomesha. Pia kuna umuhimu kwamba sisi hapa Zanzibar tunapeleka walimu Bara kutokana na wao pia wana upungufu mkubwa na ndio maana hata walimu wetu wengi au wanafunzi wetu wengi wanaohitimu hapa wanaajiri Bara na hilo unalielewa Mhe. Mbunge kwamba kule kuna tatizo kubwa zaidi kuliko sisi.

Kwa hivyo tunahisi kuendelea na utaratibu huu ni busara zaidi, lakini pia tunajaribu kuangalia mahitaji yetu. Kwa mfano sasa hivi ndio tumesema kwamba kesho kutwa tarehe 18 wanamaliza muda wao. Baada ya tathmini tuliyoifanya tutapunguza kidogo kutokana na kujitosheleza hasa tutawataka watusaidie sasa katika somo la *physics* na *mathematics*, *chemistry*, *biology*, tutakuwa tupo vizuri sasa hivi.

b) Unaposema takwimu halisi ya upandaji na kushuka kwa elimu labda utwambie kwa kutumia kigezo kipi. Kwa sababu kupanda na kushuka kwa elimu kuna vigezo vingi sana, sasa hatutoelewa ni kigezo gani unachotaka kwa mfano. Kunakigezo cha matokeo ya mitihani, kuna kigezo cha ubora aliyemaliza shule, soko linamuonaje muhitimu wa Zanzibar, soko la ajira la ndani, la Tanzania na jenginezo kwa hivyo kama hatujapata kigezo rasmi itakuwa ni vigumu kupata takwimu halisi.

Nam. 11

Uuzwaji wa Dawa za Kuulia Magugu kwa Wakulima

Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Aliuliza:-

Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwasaidia wakulima wake kwa kuwauzia dawa za kuulia magugu katika mashamba yao. Hata hivyo, dawa hizo kwa mwaka jana zilionekana kutokuwa na uwezo wa kuuwa magugu hayo.

(a) Je kuna utafiti wowote uliofanyika kugundua kinachosababisha magugu hayo kuendelea kuwepo pamoja na kwamba dawa imetumika.

(b) Je ni utaratibu upi Serikali inautumia katika ununuzi wa dawa hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 11 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mara baada ya kupokea malalamiko kwa wakulima hao dawa hiyo, ilifanyiwa majaribio na ikaonekana haifanyi kazi vizuri hapo ndipo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi baada ya kuliona tatizo hilo imewasiliana na taasisi ya utafiti ya viatilifu iliyopo Arusha *(Tanzania Pesticide Institution Arusha)* kwa kuzifanyia utafiti wa kina dawa hizo kwa lengo la kuona tatizo hilo linasababishwa na nini ili kuweza kuchukuwa hatua muafaka.

b) Mhe. Spika, utaratibu unaotumika katika ununuzi wa dawa hizo ni ule wa kutangaza TENDA na baadae Bodi ya ununuzi ya Wizara inazipitia na kuzifanyia tathmini tenda hizo kwa mujibu wa Sheria za Manunuzi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali langu lipo hapa,

a) Kwa sababu Wizara imekiri kama dawa hii baada ya kuifanyia utafiti waligundua kama haifanyi kazi vizuri kwa nini Wizara iliamua kuwauzia wakulima dawa hiyo.

b) Kama iliwauzia na haikufanya kazi naomba wakulima wale warejeshewe fedha zao ambazo walinunulia kwa sababu dawa ile serikali ilijua kama ni mbovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika,

a) Inapotangazwa tenda hii ya dawa inakuwa ule muda umeshafika na wakulima wanakuwa wanashindwa kustahamili kusubiri kwa hivyo, wanakuwa wanapewa. Halafu unapofanyika utafiti na wao baada ya kusikiliza malalamiko yao ndipo tukaamua kufanya utafiti huo na mpaka sasa hivi tuna lita 8,000 ambazo zipo Bambi zimekaa na huyu ambaye ameshinda tenda hajalipwa bado hata shilingi tunasubiri utafiti kutoka huko Arusha ili tuweze kumchukulia hatua muwafaka.

b) Kuhusiana na kurejeshewa fedha zake hizo naomba wasubiri tupate huo utafiti halafu baadae tutafanya utaratibu huo, ahsante.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Pamoja na kwamba dawa hizo hazifai kwa wakulima, lakini pia kuna sababu gani za kucheleweshwa kwa dawa hizo mpaka zikawa haziwafikii walengwa kwa wakati.

b) Ni utaratibu gani unaotumika kuuza au kugawa dawa hizo mpaka zikawa hazitoshelezi kwa wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika,

a) dawa hizo kutokufika kwa wakati sio suala letu kwa sababu mwisho wa siku dawa zinaishia vituoni na wakulima wenyewe hawaendi kuzifuata.

b) Unapotumia dawa hizi kwa kiwango kikubwa sana ile ledha ya kile kipando chenyewe ambacho wanaitia hiyo dawa kinaharibika ladha na ndio maana tunapunguza lita za kununua hizi dawa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuulizwa swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini alisema kwamba suala la kufika dawa kwa wakati sio suala lao kama Wizara ya Kilimo. Nilitaka anambie ni Wizara gani inayohusika kwa masuala haya ya dawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, sijasema kwamba sio suala letu, bali nimesema ni suala la wakulima wenyewe kuchelewa kwenda kuzifuata dawa hizo.

Nam. 34

Kusita kwa Zoezi la Usajili wa Nyumba na Viwanja

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilifanya kazi za usajili wa ardhi, nyumba na viwanja lakini kwa bahati zoezi hilo la usajili lilisita na halijaendelea tena hadi sasa.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuliendeleza zoezi hilo la usajili.

(b) Ni lini zoezi hili litaendelea tena.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimwia Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ilifanya kazi kubwa ya kutambua ardhi katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba. Kazi hii ilikua ikifanyika kwa msaada mkubwa wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (SMOLE) ambao ulikuwa unafadhiliwa na Serikali ya Finland. Mradi huo umemalizika muda wake mwaka jana na hivyo kufanya utekelezaji wa kazi hii kupungua kasi.

a) Hata hivyo Wizara inampango wa kuiendeleza kazi hii Unguja na Pemba kwa kutumia bajeti yake wenyewe na pia inaendelea kuwasiliana na wafadhili wengine kuona namna wanavyoweza kusaidia katika kuliendeleza suala hili.

b) Zoezi hili litaanza tena mwezi wa Machi mwaka huu.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Spika, nashukuru Mhe. Waziri kwa kunijibu maswali yake mazuri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Ili mwananchi aweze kusajili, ardhi, nyumba au shamba anatakiwa awe na vielelezo gani ili apatiwe usajili.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetengwa na Wizara kwa ajili ya kuifanya kazi hiyo usajili ambayo Mhe. Waziri amesema inafanyika hivi karibuni.

c) Na ni nyumba ngapi tunatarajia kusajili kwa kipindi hichi ambacho tunagemea kuzisajili kwa kipindi hichi cha mwezi Machi aliyonijibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika.

a) Naomba kwanza nizungumzie vigezo ambavyo vinatumika katika usajili ni kama hivi vifuatavyo:

- Awe mmiliki halali wa nyumba.
- Awe ni Mzanzibari na ana ZNID (kuwa ana kitambulisho cha Uzanzibari)
- Awe anatambulika na Sheha wa Shehia husika.

b) Fedha hizi zinatengwa kutokana na bajeti ya serikali na safari hii tunapata fedha kupitia Tume ya Mipango ambazo zitaweza kufanya kazi ya kumaliza eneo la Matarumbeta na eneo la Mpendae kwa nyumba ambazo zipo katika eneo kutokana na hali halisi ambayo masheha wameweza kuripoti idadi ya nyumba zao. Lakini siwezi kutoa idadi maalum, lakini najua walikuwa wanakwenda kwa mujibu wa zile nyumba ambazo zipo katika eneo.

c) Kuhusu nyumba ngapi kwamba zitasajiliwa. Kama nilivyosema kwamba sisi tunafuata kutokana na vile vigezo na sheha nyumba zake ambazo anazitambua ndani ya eneo lake. Kwa vile kipindi hichi cha Machi tunapoanza tunamalizia Shehia ya Matarumbeta ambayo imebaki kwa eneo la Jang'ombe lakini tunaanza na Shehia mpya ya Mpendae, kwa hiyo Masheha wa Shehia hiyo watakuwa na takwimu

sahihi ambazo sisi tunazitegemea sana. Ndio maana tunafanya kazi kwa karibu sana na Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ katika kukamilisha kazi hii.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza ambalo lina kitoto (a) na (b).

Mhe. Waziri katika majibu yako ulieleza kuwa mpango huu au usajili huu uliishia mwaka jana, lakini bado mnampango wa kuendeleza usajili huu. Lakini katika maelezo yako umekiri kwamba kuna Shehia za Unguja na Pemba ambazo huko nyuma ziliwahi kufanyiwa usajili huu. Mhe. Waziri mimi ni mmoja katika vijana ambao walishiriki kufanya usajili huu. nilishuhudia jinsi gani wananchi walipata tabu ambao wengine walikuwepo nje ya nchi wakarudi katika visiwa hivi kuja kufanya usajili huu na kuleta vielelezo. Lakini pia nilishuhudia gharama ambayo Serikali imetumia

Mhe. Spika: Mhe. Swali.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Sawa. Mhe. Waziri naomba nikuulize swali.

(a) Ni lini wananchi ambao wamefanyiwa usajili lakini hawajapatiwa hati ikiwemo Shehia ya Welezo watapatiwa hati zao.

(b) Ni kitu gani ambacho kimekwamisha kupatiwa hati hizo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza naomba niseme kwamba wale wote waliokuwa wamesajiliwa kwa awamu ya kwanza ambao bado hawajapatiwa kadi, basi kadi zile tayari zinaendelea kutayarishwa na nyingi tayari zishatayarishwa. Lakini kilichokwamisha kama nilivyosema tulikuwa tuna ufadhili wa Finland na ufadhili ule ukaisha kwa hivyo Serikali kwa wakati ule ilikuwa haina ile bajeti. Lakini sasa hivi tumepata fedha Serikali kupitia Tume ya Mipango ambalo zoezi lile linaendelea awamu kwa awamu. Kwa hivyo hawa waliokuwa bado hawajapewa naomba niseme si muda mrefu siwezi kusema ni lini si muda mrefu wataweza kupatiwa kadi zao za usajili.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Wakati wa zoezi hili Mhe. Waziri ni matatizo au

changamoto gani walizipata wakati wa kuendeleza zoezi hili katika Shehia mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, matatizo yako mengi hakuna kazi hata moja inayofanyika ikawa na faida bila kuwa na changamoto. Matatizo mengi ambayo yameweza kujitokeza wakati mwengine ni kupata ule umiliki halali wa yule ambaye mwenye nyumba, mwengine karithi lakini hana document hajafanya utaratibu labda wa mirathi unakuta matatizo mengine ambayo wakati mwengine Sheha pia hamtambui lakini mtu anasema yeye *owner* wa eneo. Kwa hivyo kuna matatizo kadhaa ambayo yalikuwa yanaweza kujitokeza katika maeneo. Lakini kwa kushirikiana na Masheha na majirani wakaazi wa maeneo basi walikuwa wakishirikiana katika kutatua matatizo hayo.

Nam. 52

Tija inayopatikana kwa Ukaguzi wa Gari Nje ya Zanzibar

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa kuhakikisha Zanzibar haiwi jaa kwa kuingizwa bidhaa mbovu kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kulinda maisha ya wananchi wetu wa Zanzibar.

a) Je, ni kigezo gani ZBS walichotumia kwa gharama za ukaguzi wa magari wa Dola 125 ambayo kati ya hizo Zanzibar inafaidika kwa kupata dola 25 na Kampuni ya Kigeni ikipata dola100.

b) Je, hatuoni haja ya ukaguzi huo ufanyike Zanzibar na kukusanya mapato yote ya dola 125 kama ilivyo kwa nchi nyengine ambazo hazina ukaguzi kwa kuongeza mapato kwa Serikali yetu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba nijibu kwa ruhusa yako swali la Mhe. Abdalla Maulid Diwani namba 52 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kupitia Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) iliamua kuanzisha mfumo wa Ukaguzi Ubora wa Bidhaa kutoka nje ya nchi kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini kwa

bidhaa zote zinazoingia Zanzibar yaani "Pre-export *Verification of Conformity (PVoC)"*

PVoC ni mfumo wa ukaguzi, uhakiki na uthibiti ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwamba zinakidhi matakwa ya viwango vya Kitaifa au Kimataifa kabla ya kuingizwa nchini.

Mhe. Spika**, k**atika utekelezaji wa mfukmo huu kwa vyombo vya moto vilivyotumika hasa magari, Kampuni ya *Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech* imeteuliwa kufanya ukaguzi wa gari zote zilizotumika ambazo zinatoka katika Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Kampuni ya EAA Co., Ltd kufanya ukaguzi kwa gari zote zinazotoka nchini Japan, Uingereza, HongKong na Singapore kwa niaba ya ZBS.

Mhe. Spika, Wizara kupitia ZBS imeamua kuanza ukaguzi kupitia mfumo huu kutokana na changamoto nyingi ambazo zinaikabili ZBS kwa muda huu, miongoni mwa changamoto hizo ni:-

- Ukosefu wa maabara na vifaa vya kisasa kwa kufanyia kazi za ukaguzi na upimaji kwa mujibu wa kiwango husika.
- Uchache wa wafanyakazi na wataalamu katika kufanya masuala ya ukaguzi na upimaji wa magari.

Mhe. Spika, Baada ya kutoa maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kwa mujibu wa Mkataba baina ya ZBS na mawakala hawa wa Ukaguzi wa vyombo vya moto iliamuliwa kwa uzoefu wa nchi nyengine zilizoanzisha utaratibu huo ndio maana zikawekwa gharama za ukaguzi kwa nchi za Falme za Kiarabu kuwa ni dola 125, Japan ni dola 130, Uingereza, Hongkong na Singapore kuwa dola 180. Gharama hizo ni kwa kila gari inayokaguliwa. Katika tozo hizo ZBS inafaidika na asilimia 30 (30%) kama ni *"Royality fee"* kwa kazi ya ukaguzi ambayo kwa asilimia mia moja (100%) inafanywa na wakala husika kwa niaba ya ZBS.

b) Haja ya kufanyika Ukaguzi huo hapa Zanzibar ipo na inazungumzwa na wadau wengi nchini na ili ukaguzi huo utekeleze kikamilifu ni lazima changamoto nilizoziainisha hapo juu zitatuliwe. Bila ya hivyo ni muhimu kuendelea na utaratibu

huu ili kuilinda nchi yetu kutokana na gari zisizokidhi matakwa ya viwango husika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b). Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri.

(a) Kutokana kwamba sasa hivi ZBS Amani tayari wana vifaa vya kukagulia magari kwa wale watu ambao hawawahi kukagua magari yao nje ya nchi wanakuja wanalipishwa na *fine*. Je, ni kwa nini tusisitishe zoezi hilo kule Dubai tukalifanya zoezi lote hapa Zanzibar ili ile dola 125 ikawa pato kubwa sana kwa Zanzibar.

(b) Vile vile kutokana na mkaguzi huyo je, ni vigezo gani vilivyopitiwa mpaka kupatiaka huyu mtu ambaye *Kilimanjaro Motors* ambaye anakagua magari kule Dubai wakati hakuna ukaguzi isipokuwa ni kujazia fomu lakini unampa dola 125.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

(a) Mhe. Spika, ni kweli inawezekana kwamba Amani viko vifaa kidogo vya kufanyia zoezi hili. Lakini vifaa vilioko Amani havitoshelezi, vifaa vinavyotakiwa viongezwe pamoja na maabara, vya pwani na sehemu nyengine. Lakini viliopo sasa hivi havitoshelezi. Lakini tuangalie upande wa pili vile vile moja ya masharti ya kuanzisha huu utaratibu wa *PVoC* ni hasa kulingana na utaratibu wa biashara uliopo katika ulimwengu wa sasa hivi na hasa ukitizama upande wa Afrika Mashariki. Ingelikuwa hizi bidhaa zinatumiwa Zanzibar peke yake pasingekuwa na tatizo kubwa sana. Lakini kwa sababu bidhaa hizi za biashara nyengine ni za biashara zinatakiwa zipite katika mipaka yetu na nje ya nchi ya Tanzania, basi lazima na sisi kama Zanzibar tuendane na utaratibu huu ambao ni wa kimataifa.

(b) Zoezi lililofanya kuchagua kampuni hii, tenda ilivyotolewa kulikuwa na makampuni ambayo yaliomba yaweze kufanya kazi hii na wakati ule katika viwango vyote ambavyo vilitakiwa ikiwemo kwamba uwe unakubalika kwa kimataifa, uwe na vifaa vya kutosha una mambo mengi ambayo yalikuwa yameorodheshwa, kutokana na utaratibu sio tu wa Zanzibar lakini hata TBS na vile vile upande wa Kenya na Uganda wana viwango vyao ambavyo wameviweka. Kwa bahati nzuri

huyu Jabal Kilimanjaro viwango vile alikuwa amevikamilisha ndio maana akachaguliwa.

Lakini vile vile jambo jengine linakuwa muhimu kwamba alisema Mhe. Mwakilishi kwamba labda hana vifaa kule Dubai anatumia tu makaratasi anaandika, katika mkataba tuliokuwa tumetia kati ya ZBS na hawa watu wetu ambao wanakagua, moja ambalo lilikubaliwa kwamba ZBS na timu ya Wizara waende wakaangalie maeneo haya yalivyo na jinsi hizi Kampuni zinavyofanya kazi. Kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi ni juzi tu ambao tumeruhusu watu wa ZBS kwenda katika kuangalia hali halisi ilivyo na mambo yanavyokwenda. Tukisharudi katika kufanya ziara hii tutafanya mapitio tena kuangalia hizi Kampuni jinsi zinavyofanya kutuwakilisha huko nje ya Zanzibar.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri maswali 2 ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha.

(a) Mhe. spika, lakini nilikuwa nataka kujua ni utaratibu gani umetumika kuipata hii Kampuni ambayo imepewa tenda ya kufanya ukaguzi Dubai.

(b) Je, ukaguzi huu unafanywa katika magari tu hautumiki katika bidhaa nyengine. Kwa sababu tumeshuhudia mitaa yetu ikiwa imezagaa mafriji ambayo chini ya viwango na imekuwa ikileta hali mbaya ya mandhari katika mitaa yetu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Wanu lenye (a) na (b). Kama nilivyosema nilivyojibu swali la kwanza kama kulikuwa na vigezo ambavyo vimeorodheshwa katika tenda ambavyo vimetizamwa kutokana na utaratibu wanaofanya TBS Bara, utaratibu wanaofanya Kenya na nchi nyengine za Afrika za Mashariki. Katika utaratibu ule na kulinganishwa na wengine ambao walikuwa wameomba ombi la kupata uwakilishi, Jabal Kilimanjaro wameonekana kwamba viwango vyake vya juu na ameweza kukidhi sehemu kubwa ya yale ambayo yameorodheshwa kwamba ndio *criteria* za kuweza kumpatia mtu afanye shughuli hii.

Kuhusu la pili ni kwamba utaratibu wa *PVoC* sio tu kwa magari, bidhaa yoyote au kitu chochote kitachoingia Zanzibar kinatakiwa kifanyiwe ukaguzi huko kunakotoka. Kwa hivyo mafriji na vitu vyengine kwa sababu tena inayogaiwa kwa upande wa magari Kampuni maalum zinaangalia vyombo vya moto sio

gari peke yake. Tumeanza na gari lakini baadae tutaingia katika vyombo vyengine vya moto.

Kwa upande wa vitu vyengine vya *electronic* na vitu vyengine nguo, vyakula na kadhalika, kuna Kampuni nyengine kwa mfano SGS hao ndio wamepewa kazi ya kusimamia kufanya ukaguzi wa vitu vyengine. Bahati mbaya Mhe. Spika, ni kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar wanazungumzia sana magari lakini haya mengine yanafanyiwa ukaguzi na hakuna malalamiko makubwa lakini bado inaonekana katika suala la magari ndio kwenye malalamiko lakini tutaifanyia kazi.

Kwa nini tukasema kwamba ukaguzi ufanywe kwa vitu vyote Mhe. Spika, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwa kumekuwa na utaratibu wa kuingiza vifaa ambavyo havikidhi haja na hasa hivi vifaa vikongwe vikiwa vya mafriji na vitu vyengine vya electronic. Wakati mwengine vinaagizwa vifaa vina madhara makubwa sana kwa watoto wetu kwa sababu kunakuwa vitu vya sumu katika rangi vinakuwa havitizamwi vinaingia. Kwa sababu pwani bado na mabarabara yetu hatujakuwa na uwezo mkubwa sana kukagua na kuweza kuingia ndani zaidi katika vifaa vilivyokuja ndio maana tukasema basi vifaa hivi vinavyokuja vitizamwe huko huko viliko. Vile vile vinapotizamwa kule viliko vinatupa nafasi kuondosha jaa hapa Zanzibar ukiangalia kuna maeneo mengi kuna vifaa vimetupwa lakini haviwezi kufanyiwa kazi vinasababisha vile vile kuharibu tabia nchi.

Kwa hivyo tulivyofanya hii *PVoC* inaturahisishia kuzuia vitu hivi kufika Zanzibar kwa sababu hatuna bado uwezo wa kuviharibu vifaa hasa vya electronic na vyengine vya *plastic*.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza moja lenye kifungu (a) na (b). Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilikuwa naomba kumuuliza swali (a), tunaelewa kwamba moja kati ya majukumu au majukumu makubwa ya taasisi hii ni kuweza kuchunguza ubora wa viwango vya bidhaa mbali mbali. Lakini tunaelewa vile vile kwamba taasisi hii ina upungufu wa baadhi ya maabara ambazo zingetumika katika kuchunguza viwango hivyo. Ningependa kumuuliza Mhe. Waziri ana upungufu wa maabara za aina ngapi katika taasisi hii (a).

Pili, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inapata maabara hizo ili kuweza kuona kwamba inakidhi viwango vya uchunguzi wa bidhaa mbali mbali na kuepuka gharama za kwenda kufanya uchunguzi Tanzania Bara.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli chombo chetu hiki cha kuangalia viwango vina upungufu wa maabara, maabara ambazo zinatakiwa wazifanyie utafiti na kuona kwamba viwango vinavyoingia vinakidhi haja ile ambayo tumetakiwa tuwe nayo hasa kwa kulinda maslahi na afya bora ya wananchi wetu wa Zanzibar. Huku sasa hivi kuna maabara ambayo wanaweza wakafanya baadhi ya shughuli kwa mfano kuangalia vitu vya electronic, kwa kuangalia baadhi ya vyakula lakini sio vyote kwa sababu wanategemea pia na hii Idara ya ZMFBA ya Zanzibar yaani kuangalia vyakula na vipodozi ya Zanzibar lakini pia kuna upugufu katika upande wa kuangalia vifaa vya electronic bado maabara hayajakamilika.

Kwa hivyo wana upungufu lakini kule kwengine upungufu wao sio mkubwa sana na kule kwengine upungufu wao ni mkubwa sana. Lakini bado wanapokuwa hawana nguvu hii ya kufanya kazi wanashirikiana kwa Mkemia Mkuu, wanashirikiana na hii ya vipodozi na vyakula Wizara ya Afya. Lakini pia vile vile wanashirikiana na TBS kuna baadhi ya vitu wanapeleka TBS. Kwa mfano suala zima la kuangalia uwezo wa vitu vya viungo hawajawa na uwezo huo wa kufanya kazi hiyo lakini bado wanategemea mfano TBS kuwasaidia na wanakwenda vizuri.

Kwa upande wa mkakati Serikali imetupatia bajeti mwaka huu kwa ajili ya kuongeza vifaa katika maabara na wameshaagiza sasa hivi wanategemea kati ya mwezi wa Machi na Juni vifaa vingi vya maabara vikaweza kufika hapa nchini na chombo hiki kikawa na uwezo wa kufanya kazi. Serikali imekuwa makini sana na hasa naomba nimshukuru Mhe. Rais nimpongeze sana Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuelewa sana umuhimu wa chombo hiki. Kwa kupitia kwake yeye tumepata fedha nyingi za kutosha kwa kuweza kuagizia kipindi hiki lakini natarajia kwa bajeti inayokuja tutaweza kuagizia vifaa vyengene vya kuweza kukifanya chombo chetu hiki kiwe vizuri zaidi.

Lakini pia tutajaribu kuzungumza na wafadhili kama wataweza nao kuweka mfano kama China wataweza kutusaidia nao vile vile kuongeza ubora wa chombo chetu hiki ili kifikie hali ilivyo vyengine. Lakini msisahau na mkumbuke kwamba chombo hiki bado ni kichanga huwezi kulinganisha na chombo chengine kwa mfano kama cha Tanzania Bara na nchi za jirani. Hiki ni kichanga lakini pamoja na hayo kinafanya kazi vizuri zaidi na kinajitahidi kwenda na wakati na kuweza kuwakinga wananchi wa Zanzibar wasipate madhara ya kutumia vifaa ambavyo havina ubora unaotakiwa.

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, nimesimama kwa kanuni ya 63 mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema neno. Nakwenda katika Kanuni ya 61(2)(c) kinasema hivyo:

"Mjumbe anaweza kutumia kompyuta mpakato au chombo chengine cha elektroniki ndani ya Baraza au Kamati".

Je, kwa nini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawana haki ya kuingia na simu zao humu ndani tukifika pale tunazuiliwa vifaa vyetu wakati Kanuni hii inaturuhusu tuingie navyo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hapo ulipoipiga huu utaratibu hauhusiani kabisa na *issue* inayoendelea subiri tumalize kipindi cha maswali halafu utaleta hiyo hoja yako nitaisikiliza.

Nam. 2

Kuhakikisha Ubora wa Vyakula Tunavyotumia

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Katika maisha ya hivi sasa tumekua tukiamini kwamba magonjwa ya kisukari, presha, na cancer kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na vyakula tunavyokula.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchunguza na kuhakikisha kwamba bidhaa za vyakula tunavyotumia vinakua na ubora wa kiafya ili tuondokane na maradhi hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 2 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maradhi ya kisukari, *pressure*, *cancer* ni maradhi yaliyomo katika kundi la maradhi yasiyo ya kuambukiza mbali na sababu nyengine maradhi haya husasabishwa na sababu kuu tatu zifuatazo:-

1) Utumiaji usio sahihi wa mlo wa kila siku
2) Uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe

3) Na kukosekana kwa mazoezi ambazo zote zinatokana na mfumo wa maisha yetu ya kila siku.

Wizara ya Afya kupitia Bodi ya Chakula, Dawa Vipodozi Zanzibar, imekuwa ikiwafanya ukaguzi na uchunguzi wa kina kwa bidhaa zote za vyakula zinazoingia nchini pamoja na zile tunazozizalisha ili kuhakikisha usalama wake kabla ya kwenda kwa mlaji. Aidha, Wizara ya Afya kupitia vitengo vyake mbali mbali ikiwemo Kitengo cha Elimu ya Afya, Kitengo cha Maradhi yasio ya kuambukiza pamoja na timu za afya Wilayani zinaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa upingaji bora wa mlo athari za sigara na pombe na ufanyaji wa mazoezi ili kujenga afya na kupinguza ongezeko la maradhi haya. Ahsante

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, nakubaliana na maneno yake lakini maradhi haya Zanzibar yamekuwa ni tishio kubwa sana, na nikiangalia maelezo aliyonipa naweza kusema kwamba watu wa Zanzibar kwa asilimia 80 kama sikosei hawanywi pombe, na pengine ni watu wengine ambao hawana starehe sana wanaenda kwa miguu na baskeli wanafanya mazoezi na pia chakula ni hicho hicho wanakula sana kile ambacho cha mihogo na ndizi, sasa mheshimiwa nilikuwa namuuliza swali la kwanza ambalo lina (a) na (b).

a) Ni kwamba labda amesema katika utaratibu wake amekwisha watembelea au ameshafikiwa na elimu watu 380 katika kupata elimu hii, na sisi Zanzibar tuko watu 1500 kwenda 2000 labda anaweza akatoa ufafanuzi kidogo tu wa kusema kwamba utumiaji sio sahihi wa mlo au unywaji wa pombe au mambo haya ya mazoezi.

b) Lakini swali la pili ni kwamba kuna utatanishi kidogo wa masuali ya *plastic* ikipata moto huwa inatoa kansa, hili suala sijui kama ni la kweli au sikweli lakini kama ni la kweli yake maji yanayoanikwa barabarani ambayo ni kunywa jee hayana madhara. Mheshimiwa naomba hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante, mheshimiwa kataka nimpe ufanunuzi kidogo kuhusu upangaji wa mlo.

Mhe. Spika, upangaji wa mlo mara nyingi tunapokula chakula chetu kwanza hatuli chakula kwa mpango maalum, yaani tunakuwa ni watu wa kula kila mara ukijitathmini unaweza kutoka nyumbani umwesha kunywa chai lakini mpaka jioni ukirudi nyumbani umeshakula mara nne au tano na bado ukifika nyumbani unaomba niwekewe chakula nile. Umekula urojo wewe, ukanywa

chai ofisini, ukanywa mambo mengine upangaji wa mlo ni kwanza nikupangilia vyakula unavyokula isiwe unakula stachi tu, uwe unachanganya pamoja na vyakula vyengine. Pia katika kula kwako basi vipitane visiwe ni vyakula unavyokula mara kwa mara.

Mhe. Spika, isitoshe tuna kawaida siye Wazanzibari au niseme binadamu unaweza ukala umechoka ukishamaliza kula chakula cha mchana penye mkeka pale pale unalala kwamba umechoka, haitakiwa ule halafu ulale. Ukishakula chakula *at least* upate masaa mawili ya kuzunguka ili chakula kile nacho kipate kufanya mzunguko wake katika mwili wako.

Lakini la pili aliniuliza *plastic* hazisababishi kuleta *cancer*. Kwa kweli mpaka sasa hivi hakuna uchunguzi ulochunguza ukagundua *plastic* zinaweza zikasababisha moja kwa moja uletaji wa *cancer*. Maji amesema katika chupa zile za *plastic* mheshimiwa nataka nikuthibitishie kwamba chupa zile za *plastic* zinazowekwa maji ya kunywa, kwanza huwa zimeshafanyiwa uchunguzi wa kutosha huko katika viwanda, lakini pia zinapoingia katika nchi yetu basi Bodi ya Chakula huwa inazichunguza na zimeshawahi kurudisha bidhaa ambazo ziko katika chupa au makopo ambazo hazina ubora. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Nikushukuru sana Mhe. Spika kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana yasio na ufasaha kwa wananchi wetu naomba kuuliza swali lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa sababu wakinamama wengi wanaotumia dawa za majira *Contraceptive Pills* wamekuwa na kulalamika sana wakipata magonjwa nyemelezi kama ya sukari, *pressure* na mengineyo. Je, serikali umeifanya utafiti wowote kubaini jambo hili.

b) Kwa kuwa moja katika mambo matatu Mhe. Waziri alipokuwa akiyataja alisema ni uvutaji sigara, na uvutaji wa sigara umeenea kila pahala serikali sasa iko tayari kupiga marufuku uvutaji wa sigara kila pahala na kuweka sehemu maalum za uvutaji huo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba radhi sana mjumbe swali la mwanzo sikulisikia vizuri, naomba radhi naomba aendelee kunieleza.

Mhe Spika: Samahani mwache ajibu waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe Spika naomba kwanza kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na ya kitaalamu na ambayo

yamesikika kwa wananchi wote kwa mafunzo haya aliyotoa na wananchi wote naamimi wameyafahamu, mimi nitaongezea kidogo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mpendae swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa kuna utafiti ambao umefanyika na ripoti yake ipo ambayo ipo katika kitengo cha *NCD Non Communicable Disease*, na nashukuru yeye Mhe. Dimwa ni mtaalam kwa masuala haya kwa hiyo anaelewa utafiti huo. Na utafiti huo mara mwisho ulifanyika mwaka 2014 na umo katika *Health Bulletin* ya kwetu Wizara ya Afya. Na kwa bahati mbaya naomba nilijulishe Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wa Zanzibar kwamba maradhi yote yanayoambukiza hivi sasa yanapungua *graph* lake linakuja chini, maradhi yanayoambukiza. Na maradhi yasioambukiza, yaani *Non Communicable Disease graph* lake linapanda, tuko katika asilimia 28 mpaka 30 tu tuko hapo sasa hivi. Na vifo vyote vinavyotokea ni kwa asilimia hiyo hiyo ya asilimia 28 mpaka 30.

Namshukuru Mhe. Suleiman Sarahan katika suala lake la msingi aliuliza swali zuri sana na akatoa takwimu yeye mwenyewe, kwamba asilimia 80 sijui kaipata wapi ya Wazanzibari hawanywi pombe wala hawavuti sigara. Mimi naamini asilimia kubwa zaidi ya hiyo naamini hivyo lakini bado haujafanyika uchunguzi katika eneo hilo. Lakini hivi sasa nataka kusema kwamba asilimia 38 ya vifo vyote vinavyotokea nikutokana na maradhi yasioambukiza pamoja na ajili za barabarani, ajali za barabarani siku hizi zinaingizwa katika fungu hilo hilo la maradhi yasioambukiza .

Pili, Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe. Dimwa kuhusiana na uvutaji wa sigara na unywaji pombe hivi sasa wizara imo katika mchakato wa mwisho kabisa wa kuja na ule muongozo, unaitwa muongozo wa kupiga marufuku kuvuta sigara *in public place* katika maeneo ambayo jamii ipo. Muongozo huo ukishakamilika tu basi utawasilishwa hapa katika Baraza lako tukufu na itatolewa kama ni amri ama sheria maalum kwamba maeneo yote yatapigwa marufuku kuvuta katika *public place*. Mfano, vituo vya daladala, ama hospitali, utaruhusiwa au mtu ataruhusiwa kuvuta sigara *in private* akiwa peke yake ili asiweze kumuathiri mwengine.

Lakini mheshimiwa naomba kuongezea hapo hapo katika hizi sababu kuu tatu zilizotolewa na Mhe. Naibu Waziri utumiaji usio sahihi wa mlo vyakula vyetu wanatuambia wataalamu wetu na madaktari, vyakula vyetu vya asili

tumeviacha. Kuna vyakula ambavyo vina afya kubwa sana na pia vinapunguza maradhi haya tunakula sisi mwezi wa Ramadhani hadi Ramadhani. Vyakula vile sasa hivi wenzetu nchi za nje Ulaya nchi zilizoendelea wanavichukua kutoka Zanzibar mfano maboga. Sisi maboga hatuli mpaka Ramadhani hadi Ramadhani, na maboga siku hizi ukienda hoteli yoyote ya kitalii ya kifahari unakutwa inaitwa *pumpkin soup* unapewa pale katika *starter*. Vitu kama vile sisi tumeachana navyo, mumunye inatengenezwa supu ya mumunye ukienda hoteli za kimataifa utakuta supu sisi mamumunye tunakula Ramadhani hadi Ramadhani, naomba sana turejee katika vyakula vyetu vya asili. *(Makofi)*

Vyakula vya asili vitatusaidia kuna matunda yametoweka Zanzibar kama vile zambarau sasa hivi unaziona chache, lakini zambarau zinapunguza kiwango kikubwa sana cha sukari ndani ya mwili. Zambarau ukila kama mtu mwenye sukari kinapungua kiwango chake, kuna matunda kama fuu, kama pilipili doria, matunda yote hayo tumeacha nayo naomba turudi kwenye *our traditionally foods*. Wali wa mtama na mengineyo mkate wa manda na kadhalika.

Ahsante Mhe. Spika *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante, mheshimiwa muda wa maswali utakuwa umekwisha lakini kwa kuwa swali limebakia moja naomba tulimalizie.

Nam. 102

Kushuka kwa Ubora wa Huduma Zantel

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Huduma za Mawasiliano ya Kampuni ya Zantel inazidi kudorora siku hadi siku kiasi ya kutokidhi haja ya kiwango cha matumizi kwa wateja wake. Wakati Waziri akifanya majumuisho kwenye kikao cha Bajeti 2016, alieleza kwamba ifikapo mwezi wa Agosti, 2016, Zantel watakuwa na mitambo mipya yenye kukidhi haja kwa wateja wake, na kwamba mitambo hiyo wameshairekebisha lakini hadi leo usumbufu wa mawasiliano ya Kampuni hiyo unaendelea.

(a) Je, serikali inajuwa kwamba kampuni ya simu ya Zantel huduma zake zimeshuka kwa kiwango kikubwa kulinganisha na zamani jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa wateja wanaotumia mtandao huo.
(b) Je, ni sababu gani inayopelekea kushuka kwa huduma za mawasiliano ya simu ya mtandao wa Zantel.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kuitaka Kampuni hiyo ifunge mitambo mipya ili iweze kukidhi mahitaji ya wateja wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 102 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli kwamba kiwango cha huduma za kampuni hii ya Zantel zimeshuka kwa wastani na sio kwa kiwango kikubwa kama inavyoelezwa, kwani bado faida inayochangiwa na kampuni hiyo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kubwa.

(b) Sababu ya kushuka kwa kiwango cha huduma ni uchakavu wa mitambo pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya wateja ambao hivi sasa wanamiliki vifaa vingi zaidi vya mawasiliano. Pia matumizi ya *internet* yamekuwa makubwa sana kuliko matarajio.

(c) Ili kutatua matatizo yaliyotajwa, kampuni ya Zantel iliamua kuweka katika mtandao wake wote, mitambo mipya Unguja na Pemba. Kazi ya ufungaji wa mitambo hiyo kwenye minara ya hapa Unguja ilikamilika katika mwezi wa Septemba, 2016 na kuanza kuhamishwa kwa mawasiliano kutoka katika mitambo mikongwe kwenda mipya kwa majaribio katika baadhi ya minara. Kufikia mwezi Disemba, 2016 zoezi hilo la majaribio ilibidi lisitishwe baada ya kutokea hitilafu kubwa katika mitambo na hivyo kurudishwa kama ilivyokuwa mwanzo huku Zantel wakitafutia suluhisho tatizo hilo. Mhe. Spika, hivi sasa tayari Zantel wameshapata ufumbuzi wa tatizo hilo na kazi imeanza rasmi Januari 30, 2017 na inategemewa kumalizika mwishoni mwa mwezi Aprili iwapo hakutokuwa tatizo lolote la kiufundi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwenye majibu yake kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la watumiaji kwenye Kampuni hii ya Zantel. Pia amekiri pia kuna uchakavu wa mitambo ya kampuni hiyo na pia amekiri kwamba kwenye majaribio yao ya awali walifeli ndio maana wakarudia tena mfumo ule. Mimi swali langu liko hapa.

Je, ana uhakika gani kwamba hii mitambo itakayofungwa ya mara hii haitafeli kama hiyo waliyoifanya kwenye majaribio. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli walipofanya hii kazi walikutana na changamoto tofauti, lakini hivi sasa washaangaza kazi na leo awamu ya mwanzo wanategemea kuimaliza na baada ya hapo kila awamu wanapozimaliza ziko *phase* 20 hizi lazima wafanye *test* na ile *test* baada ya kuona kwamba kiwango chake kinaridhisha ndio wanaendelea na awamu nyengine. Kwa hiyo, hii ndio njia pekee ya kuweza kujua kwamba wapi kuna tatizo ili tatizo lisitokeze tena. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Spika, na mimi ningependa kumuuliza swali dogo la nyonyeza lenye vifungu la (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa Kampuni ya Zantel inamilikiwa na kampuni binafsi, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ina hisa za 18% katika miaka hiyo, sasa katika hisa miaka nenda rudi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi leo haijawahi kupokea faida hata mara moja.

a) Je, serikali haioni muhimu wa kuweza kuuza hisa zao hizi kutokomea na hii kampuni na kuiwachia mkono ili wao waweze kupata cha kwao baada ya kuwa mmoja wa wamiliki kwa miaka yote.

b) Kampuni ya Zantel imepokelewa na Wazanzibari kama ni cha kwao katika miaka yote kwenda nyuma. Lakini hivi karibuni tumeanza kuona kwamba Kampuni ya Zanteli watu wengi waanza hasa kuwa line mbili, tatu lakini pia kuiachia mkono kitenda ambacho kinasabisha Kampuni ya Zantel kulipa pengine fedha ndogo katika ulipaji wa kodi. Je, serikali inatumia mbinu gani katika kuhakikisha kwamba Kampuni hii bado Wazanzibari wanabakia nayo kujua kuipokea kama ya kwao ili kuleta uzalendo na kuhakikisha fedha zote zinazopatikana zinabakia katika nchi yetu na visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwanza nataka kumwambia kwamba serikali inaendelea kupata hisa na si 18 ni 15 kama kawaida, na kama anavyojua masuala yote haya ya hisa yako Wizara ya Fedha lakini nataka kumwambia kwamba Zantel katika wachangiaji wazuri wa fedha katika mchango wa SMZ katika Serikali yetu.

Kwa mfano, mwaka 2015 Zantel hii ilichangia kupitia tunasema wenyewe *exercise duty* kupita *VAT* kupita *DSL* kupitia *payee* takriban bilioni 24, 2015. Na 2016 kweli imeshuka kidogo lakini wameweza kuchangia bilioni 22, kwa hiyo hapo unaona kwamba mchango wa Zantel ni mkubwa sana na kwamba

bado siye tunawashauri Wazanzibar kwasababu ni kampuni yao waendelee kuitumia kampuni hii. Kweli kama ulivyosema mimi nina imani kubwa sana kampuni ambayo inatowa viwango vya nafuu sana, Wazanzibar wataendelea kuitumia ndio maana Zantel inaendelea kuimarisha mitambo yake na kuna *phase* 20 nimesema ambazo za kuifanya mitambo yao iwe ya kisasa na nina imani baada ya muda mfupi madiliko yatapatikana. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Warday: Ahsante sana *Bisimillah Rahman Rahim.*

Mhe. Spika, mimi nitaomba kumuuliza maswali ya ziada yenye (a) na (b) Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

a) Kwa kuwa kampuni za simu wana utapeli ambao wananchi hawautambui. Swali langu la kwanza wanachaji zile pesa za muziki katika simu inapopigwa wanaopigiwa shilingi 150 au 180 kwa mwezi kwa kila mtu, na watu wengi katika jamii hawajataka lile suala ule muziki walipishwe wanautia *automatical* mtu anachajiwa mwisho wa mwezi anakatwa shilingi 180. Ukipiga hesabu karibia milioni 150 mpaka 230 inafaidika Zantel na mitandao mengine kila mwezi kwenye maswala ile miziki tu wanaochajiwa watu shilingi 150 au shilingi 180. Ni lini wizara yako itapiga faini suala hilo la utapeli ambao watu hawajataka suala la muziki au litatuletea ripoti ambayo itatujulisha wametumia njia gani za utapeli kuhakikisha kuingiza pesa kwa njia hiyo.

b) Mhe. Spika, kampuni za simu wana mtindo wa wizi utapeli tena narudia, mtu anatia shilingi 5,000 kadi ya simu elfu 10,000 matokeo yake hafla inakatwa elfu 3,000 bila mwenyewe kujulishwa au kujijua *automatical* inapotea kwa mazingira ya kutatanisha. Ni sababu zipi ambazo mitandao hii inatumia kutapeli watu kwa njia hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kwanza mimi nataka kumtoa wasi wasi kwamba mashirika haya yanaminika, ni mashirika ambayo yanafuatiliwa kwa karibu sana na *TCRA.* Kwa hiyo, mimi nina imani kubwa sana jambo la utapeli haliwezi kutokea katika mashirika haya, isipokuwa inaweza kutokezea mtu baadhi ya wakati bila ya kujitambua mwenyewe akaamua kujiunga na hayo mambo yanayoitwa muziki na baadae iwapo ataona anakatwa ana uwezo wa kuomba tena huduma kwa mteja akawaarifu kwamba mimi nimeungwa kimakosa naomba mnitoe wanampa utaratibu na yeye baadae anajitoa. Kwa hiyo, mimi namtoa wasi wasi na iwapo

kutatokea hilo tatizo la kukatwa pesa nyingi mtu kutokana na mazungumzo ambalo ni nadra kutokea basi nina imani kubwa sana huduma kwa wateja wanamrejeshea kiwango hicho kama kutatokea na matatizo yoyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha kwanza tuna tangazo la wageni, mgeni wa Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) ni Mzee Sukwa Said Sukwa. Karibu sana Mzee Sukwa, ameongozana na mtoto wake Mussa Sukwa.

Mzee Sukwa amewahi kuwa Mbunge kupitia Baraza la Mapinduzi mwaka 1978; mwaka 1980 aliwahi pia kuwa Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi, mwaka 1978 alikuwa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Vijana, Tanzania; mwaka 1984 alikuwa ni Afisa Idara ya *Organization* CCM Makao Makuu, Zanzibar; mwaka 1988 alikuwa Afisa ya Idara ya *Organization* Kitengo cha Bunge, Baraza la Wawakilishi na Serikali za Mitaa huko Dodoma; mwaka 1992 Katibu Mkuu UVCCM, Tanzania; mwaka 1998 Katibu wa Mkoa wa CCM, Tanga Bara; mwaka 2003 Katibu wa Mkoa wa CCM, Kusini Unguja; mwaka 2006 Mshauri wa siasa Ofisi ya Naibu Katibu Mkuu CCM, Zanzibar. Karibu sana Mzee Sukwa, karibu Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Baada ya tangazo hilo naomba kukusikiliza sasa Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nyengine tena baada ya kuona pale nilipotaka kuingiza mwanzo ilikuwa sipo, sasa naingiza pahala pake. Nimesimama kwa Kanuni ya 63, lakini zaidi nimekazia katika Kanuni ya 61, kifungu kidogo cha (2)(c) ambapo mjumbe anaweza kutumia kompyuta mpakato au chombo chengine cha kielektroniki ndani ya Baraza au kamati. Sasa naona fursa inaturuhusu wajumbe tufanye hivyo lakini sijui taratibu gani zilizofika katika Baraza lako hili tukufu kwamba tunanyang'anywa simu zetu pale nje kabla hatujaingia humu ndani ya Baraza.

Mhe. Spika: Ahsante mheshimiwa nadhani hicho kifungu ulichokisoma umetaja kompyuta mpakato ambayo nafikiri ni *laptop* hiyo pamoja na *IPAD*. Sina uhakika kama vyote vinazuiliwa lakini simu nadhani kifungu hicho hicho ambacho umekisoma 61 nafikiri (d) inasema mjumbe akiwemo humu ndani hatasikiliza redio, hatosoma kitabu chochote, gazeti au barua ila tu kama yahusu shughuli za mjadala na kwa idhini ya Spika. Sasa sina uhakika sana suala la matumizi ya simu kwa sababu itakuwa hairuhusiki pia kuja na simu

humu halafu kwa bahati mbaya ukaanza kuzungumza na simu humu ndani. Lakini naomba niipe serikali pia kidogo tuisikilize Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa na maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini imani yangu kwamba kama maelezo ambayo umeyatoa ni sahihi kabisa. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe kwamba amekwenda kwenye fasili ya 61, kifungu kidogo cha 2(c) ambapo angesoma fasili ya 61, kifungu kidogo cha 2(a) ambacho naomba nikinukuu Mhe. Spika.

> "Mjumbe au mtu mwengine yeyote ambaye ataingia na simu ndani ya ukumbi wa Baraza na akaitumia au ikasikika inaita au ikaingilia mawasiliano katika Baraza kwa namna yoyote ile anaweza kuamriwa na Spika kutoka nje ya Baraza kwa ajili ya kikao kinachoendelea".

Kwa hiyo, Mhe. Spika ukitizama mintaraf ya kwamba ukiingia na simu maana yake simu uizime. Sasa kwa msingi kwamba unaingia na simu ambayo imezimwa nadhani ni busara ukaiacha nje, kwa sababu ukiingia nayo humu ndani simu kwa namna yoyote utaitumia na utakapoitumia maana yake Spika akuamuru utoke ukose kikao, ukose kuwawakilisha wananchi wako ambao wamekutuma hapa ili Spika akunyime posho la siku. Nadhani busara hii ambayo tunayoitumia kama serikali na kama chombo chake Mhe. Spika kuzizuia simu nje tutakuwa tunatumia vizuri zaidi kwa utaratibu huu. Kile kifungu kinachozungumzia 61(2)(c) maana yake ni matumizi ya elekrotoniki sote tunajua tunatumia *IPAD, mini IPAD, Tablet, Laptop* zote zile unaweza ukatumia kwa kusomea taarifa zako ambazo hazitokuwa na maingiliano na mawasiliano ya mitandao ya Spika ama mawasiliano mengine ambayo tunatumia kwa ajili ya mawasiliano. Kwa hiyo, imani yangu kwamba kifungu kiko sawia 61(2)(a) kina haki ya kuendelea kutumika na hakuna mgogoro wowote Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi nadhani…

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mheshimiwa utaratibu.

Mhe. Spika: Endelea kubaki hatujamaliza hili mheshimiwa.

Waheshimiwa mimi nadhani tukubaliane suala la simu sote tunakubaliana kwamba si sahihi matumizi yake humu ndani. Suala la hizi kompyuta mpakato na *IPAD* kwa sababu hutapata kuzungumza nayo, lakini kama utaingia nayo kwa ajili ya matumizi ya shughuli zetu sisi humu ndani, nafikiri hilo tunaweza tukalifanyia kazi tukaona namna ambavyo tunaweza tukaliweka sawa. Kwa hiyo, nafikiri hili halina tatizo sana tuwekeni utaratibu tutaruhusu mtaingia na hizo *IPAD* lakini iwe tu kwa ajili ya matumizi ya shughuli ambazo tunazifanya humu ndani.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nakushukuru kwa ufafanuzi lakini pia nashukuru kwa ufafanuzi wa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye yeye ndiye ameweka mambo *clear* kabisa, na mimi *issue* yangu ilikuwa iko hapa hapa katika muongozo kuhusiana na matumizi ya simu katika Baraza.

Mhe. Spika, kama utasoma kifungu ambacho Mhe. Abdalla Maulid Diwani amekisoma kinasema mjumbe anaweza kutumia kompyuta mpakato au chombo kingine cha kielektoroniki ndani ya Baraza au kamati. Lakini pia kanuni hizi hizi za toleo la 2016 *very latest* inaeleza kanuni aliyosoma Mhe. Waziri kwamba kanuni zinakupa wewe *power* atakaye-*misuse* hii fursa ambayo imetolewa na kanuni hizi zetu ambazo ni mpya kabisa una haki ya kum-*punish according to* kanuni. Sasa Mhe. Spika, muongozo ambao ninataka kuomba ni kwamba tunaendesha taratibu za Baraza kwa busara, ama tunaendesha taratibu za Baraza kwa kanuni ambazo tumejiwekea kama muongozo wa kuendesha taratibu zetu katika Baraza.

Mhe. Spika, jengine wewe ndio una *power* ya Baraza hili, kwa sababu wewe ndiye mmiliki wa hili Baraza na wewe ndiye mkuu wa hili Baraza. Sasa haipendezi kuwa una-*transfer power* zako kupeleka kwenye *government*, wewe ni muhimili Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante nimekufahamu Mhe. Wanu maana yake ilikuwa ni muendelezo tu wa hili hili, serikali pia ni sehemu yetu sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, yanapokuja mambo kama haya wana haki na wao kutoa mchango wao kuhusiana na masuala yanayohusu kanuni au sheria ambazo tunazitumia humu ndani. Kwa hiyo, nafikiri hilo nilikuwa nimeshalimaliza kwamba tutaruhusu zile kompyuta mpakato pamoja na *IPAD* lakini zitumike kwa ajili ya hizi shughuli zetu na nitakuwa na haki ya kumzuia mtu au kumtoa kama ambavyo inaagiza kanuni, wala halina tatizo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nanyanyuka na kanuni hiyo hiyo ya 61 (2)(a), mjumbe au mtu mwengine yeyote ambaye ataingia na simu ndani ya ukumbi wa Baraza na akaitumia na akasikika inaita au ikaingilia mawasiliano katika Baraza kwa namna yoyote ile anaweza kuamriwa na Spika kutoka nje ya Baraza au kwa ajili ya kikao kinachoendelea…

Mhe. Spika: Mhe. Nadir samahani suala hili ndio hili hili ambalo…

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mimi mheshimiwa…

Mhe. Spika: Lako wewe ni jengine?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ndio.

Mhe. Spika, tusifichane mawaziri wote humu ndani wana simu na wakisachiwa hata sasa wanazo, sisi tuna wananchi na tuna majimbo wao wengine hata majimbo hawana, wana simu na wasachiwe sasa hivi. Haiwezekani mawaziri waingie na simu wawakilishi wasiingie na simu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Nadir.

Mheshimiwa hizi kanuni zetu zina-*apply* kwa watu wote hata wao, kwa bahati mbaya sana mimi kama Spika sijamshuhudia waziri yeyote akiwa na simu,

Baadhi ya Wajumbe: Wanazo, wanazo, wanazo! *(Makofi)*

Mhe. Spika: Kama atakuwa anayo ameizima haisumbui shughuli zetu.

(Hapa baadhi ya Wajumbe wakipiga makofi kwa sana na kupiga kelele)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tusikilizane, naomba tusikilizane.

Mimi kama Spika kwenye kiti sijamshuhudia waziri akitumia simu, na nikiliona hilo sitaliruhusu na nitamtoa nje hata kama ni waziri, sijashuhudia kwa macho yangu nikimuona waziri anatumia simu wakati tunaendelea na vikao vya Baraza nitamtoa nje kama ninavyomtoa mjumbe mwengine yeyote.

Baada ya hayo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Spika ili aje achukue kiti. Naibu Spika, karibu.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2016

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa kuweza kuchangia na kutoa maelezo machache katika baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuzitoa.

Mhe. Spika, na mimi niungane na wajumbe wenzangu kwanza kuishukuru Kamati inayosimamia Viongozi Wakuu…

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa naomba utulivu, tumsikie uzuri Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Lakini sambamba na hilo pamoja na hotuba fupi iliyowasilishwa na Mhe. Waziri naomba kuchangia katika mswada huu wa Sheria wa Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, ziko baadhi ya hoja nyingi ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wajumbe sambamba na hizo tuanze na maana Waheshimiwa Wajumbe wengi waliomba kupata tafsiri ya neno uchaguzi ambapo katika sheria hii kusoma katika sehemu ya utangulizi, kifungu cha 2 hakijaja na *clear definition* ya neno uchaguzi. Lakini katika sheria hii kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati walipendekeza kwamba ni vyema tukaipata ile tafsiri ya neno uchaguzi kama ambavyo imeelezewa katika sheria ya uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1988. Kwa maana hiyo, niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba kilichofanyika hapa ni kuendelea kuitumia tafsiri ya uchaguzi iliyokuwepo katika sheria ya uchaguzi ya mwaka 1988 hata katika mabadiliko yetu ya uanzishwaji wa sheria ya Ofisi ya Tume ya Uchaguzi tuliona ni busara tukaweza kufanya hivi.

Mhe. Naibu Spika, lakini hapo hapo katika sehemu ya utangulizi bahati nzuri tena Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati waliweka sawa, lakini katika sehemu ya uchaguzi wa marejeo kwa maana neno “uchaguzi” mwisho kabisa kifungu

(e) kulikuwa kuna sehemu inasema uchaguzi wa marejeo ambayo wajumbe wengi waliomba kupata maana yake.

Mhe. Spika, maana halisi ya uchaguzi wa marejeo tizama katika tafsiri ya Kiingereza neno hili uchaguzi wa marejeo tumelipata katika maana mbili. Maana ya kwanza tunaipata Kiingereza tunasema tutakuwa tuna "*runoff election"* lakini maana ya pili tutakuwa tunasema tunapata *rerun election*. Hizi maana zote zina maana gani kwa Kiingereza lakini maana hizi mbili zimebeba *content* moja ya Kiswahili. Ukizungumzia *concept* ya *runoff election* ni ile aina ya uchaguzi ambao uchaguzi umekamilika katika hatua zote na *stage* zote mpaka kufikia siku ya mwisho ya watu kwenda kupiga kura. Lakini ikapelekea tu baada ya matokeo mshindi hakupatikana yawezekana kuwe kuna makubaliano kwamba mshindi apatikane kwa asilimia, kama asilimia 51, ikitokea mshindi hajafika asilimia 51 itapelekea uchaguzi ule Kiingereza unatambulika kama *runoff election* yaani itabidi uchaguzi ule uje urudie tena maana mshindi bado hakupatikana.

Lakini tutakuwa tuna maana ya pili inayosema hii itakuwa inaitwa *rerun election* ambayo hii yenyewe Kiswahili chake sambamba kama tunavyosema uchaguzi wa marejeo, lakini ni uchaguzi ambao umefanyika lakini imetokea kuwa na mapungufu ya *technicality* ama kutokamilika kwa baadhi ya mambo ama hatua ikapelekea uchaguzi kuharibika. Inapotokea vile ndio maana ukaona ipo sababu sasa ya sheria hii kuja na kifungu maalum kitakachoweza kusema katika aina hizi za uchaguzi tunaposema uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, uchaguzi wa Diwani, uchaguzi mdogo sambamba iwe na kifungu maalum kitakachosema kuwe kuna uchaguzi wa marejeo.

Aidha, kesi zote hizi mbili zitakapotokea ni vyema tukaweza kuwa na *specification* ya *session* ambazo tunazo. Tutakuwa tuna mifano husika ambayo imeshawahi kutokea katika Taifa letu hata mwaka 2000 Mkoa wa Mjini Magharibi ulifanya uchaguzi maalum kutokana na kwamba na zile *effect* ambazo zilitokea ndani ya Mkoa husika ikapelekea uchaguzi wa kura za Rais kurudiwa katika Mkoa ule. Sasa mwanzo sheria yetu haikuwa ikituongoza hivi, sasa tumeona ni vyema kile ambacho tulikuwa tukikifanya ni vyema tukatumia kama utaratibu wa sheria nyengine za Ofisi ya Uchaguzi zilivyo na sisi kuweza kuweka kifungu hiki cha uchaguzi wa marejeo.

Mhe. Spika, pia niseme kulikuwa kuna hoja nyingi sana za wajumbe lakini ilikuwepo hoja kwamba sheria hii inaifanya Tume ya Uchaguzi kutokuwa yenye kujitegemea.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza sana katika hoja hii, lakini tukirudi katika Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 119(9) na (12) kinasimama sawiya kujibu hoja zote ambazo zinaiweka Tume ya Uchaguzi kuwa ni kama chombo, ambacho hakitegemei na hakisikilizi uamuzi wa mtu mwengine yeyote zaidi ya maamuzi yake ambayo itakuwa inaweza kuyatoa.

Mhe. Naibu Spika, nikinukuu katika Katiba ya Zanzibar,Kifungu cha 119(12) kinasema:

"Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au Idara yoyote ya serikali, au maoni ya chama cha siasa".

Kwa kauli hii inaifanya Tume ya Uchaguzi kuwa ni chombo chenye kujitegemea na chombo ambacho kitakuwa kina mamlaka yake tofauti na ambavyo baadhi ya Wajumbe walikuwa wakifikiria au kama vile ambavyo wamekuwa wakitushauri.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha 18 cha mswada huu ambapo nashukuru wajumbe wengi wameweza kukisemea hiki na ambacho kimezungumzia suala la kuwepo kwa Sekretarieti ya Tume, ambayo itakuwa na jukumu la kuisaidia Tume katika utekelezaji wake wa majukumu ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika hili waliomba kuwa zile kurugenzi ambazo zitaanzishwa ndani ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi ni vyema sifa zao ziweze kuwa *initiated* na kutajwa moja kwa moja katika sheria hii. Pia tuseme kwa sababu kurugenzi hizi zitatengenezwa na Tume yenyewe, na kila kurugenzi itakuwa na sifa zake, lakini inawezekana ikawa na kurugenzi zaidi ya tatu au nne. Kwa maana hiyo, itakuwa ni busara kila kurugenzi ya Tume hii kama ambavyo mswada huu ulivyosema katika kifungu cha 33, kwamba mwisho wa siku waziri atakuja kutunga kanuni ambazo zitakuwa ni miongoni mwa vitu vitakavyokuwa vinakwenda sambamba katika miongozo. Sasa namna ya kurugenzi zitakavyotoka sifa zake zote zitaunganishwa katika kanuni ili kuweza kupunguza baadhi ya mambo ambayo tunaamini hayatakuwa na tija kubwa sana kuwepo moja kwa moja.

Jambo jengine Waheshimiwa Wajumbe waliomba sana kuwepo kwa tafsiri ya baadhi ya maofisa ama *senior officers* ambao wamezungumzwa katika kifungu hiki.

Nataka tuwaambie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba maafisa hawa wengi watakuwa ni wale ambao wanatokana na Utumishi wa Umma kama sheria ilivyo, hata uajiri wao umetokana na sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa maana hiyo, tafsiri zake zote zinapatikana katika sheria ya Utumishi wa Umma kama ambavyo itakuwa imeelezwa katika kifungu cha Sheria hiyo, kidogo kimenitoka kifungu chenyewe, lakini Sheria ya Utumishi wa Umma imeeleza baadhi ya hizi sifa zao.

Pia nipende kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba yapo baadhi ya mambo mengi ambayo wameyagusia, natumai Mhe. Waziri atakapokuja kutunga kanuni hizi mengi yatakuwa yamezingatiwa.

Vile vile niende katika kifungu cha 20 ambacho wako baadhi ya Wajumbe walipendekeza baadhi ya maneno yarekebishwe. Tunakubaliana na baadhi ya Waheshimiwa akiwemo Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Miraji Khamis Mussa na Waheshimiwa wengine ambao walipendekeza hili neno 'usajili' libadilike na badala yake iwe ni 'kuandikisha'. Hili tumelizingatia, ushauri wao tumeupokea ni kama ambavyo kamati pia ilipendekeza neno hili likabadilika kutoka kwenye usajili wa wapiga kura na iwe kuandikisha wapiga kura.

Sambamba na hilo katika kifungu cha 22 ambacho pia baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe waliweza kuzungumza kilikuwa kinasema hivi, naomba kunukuu.

Kifungu cha 22 kinasema kwamba:

"Kwa ajili ya kuhakikisha uhuru wa Tume na uwazi wa Afisi, Afisa isipokuwa yule aliyeteuliwa na Rais, hatohamishwa bila ya ridhaa ya Tume".

Mhe. Naibu Spika, hapa tutambue kwamba maafisa wote waliokuwepo katika serikali wanaongozwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Serikalini. Sheria ambayo pia inatoa mamlaka kwa baadhi ya maafisa kuweza kuhamishwa kutoka idara moja kwenda katika idara nyengine.

Pia ukiisoma sheria hii ya Utumishi wa Umma katika kifungu cha 65 kimeeleza fika kwamba unapotaka kumhamisha mtendaji mmoja kutoka sehemu moja kwenda katika sekta nyengine inataka pia, pamoja na ridhaa ya afisa husika, lakini ikitokea kwamba hakukuwa na ridhaa ya kutosha ndio pale kama ambavyo Mhe. Miraji Khamis Mussa alijaribu kusema ni vyema ridhaa hii tukamuachia Katibu Mkuu Kiongozi, lakini endapo ikitokea baadhi ya maafisa wake hawakuwa wameridhiana suala la kuhamishwa kwa afisa yule, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa na *room* ya moja kwa moja sasa kuweza kumhamisha

mtendaji huyu kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 65 cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, pia twende katika kifungu cha 23 ambacho baadhi ya Wajumbe waligusia kinachosema kwamba: "Afisi itakuwa na bajeti yake maalumu kwa fedha ambazo zitaidhinishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi ya afisi. Lakini zilikuwepo hoja kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa nini kifungu hiki kisiwekwe sambamba na kile kifungu cha 11, lakini ni vyema tuwaambie Waheshimiwa kwamba tukitizama mdorongo wa kifungu cha 11 kiko katika Sura ya Tatu ambayo hata *heading* yake iko katika uanzishwaji wa afisi na kazi zake. Lakini kifungu hiki cha 23 kiko katika sehemu ya fedha. Hivyo ni vyema tukawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba watukubalie katika vifungu hivi ni vyema vikaendelea kubaki sehemu tofauti, kwa sababu mwisho wa siku kila kimoja kitakuwa na majukumu yake kama ambavyo imeainishwa katika mswada wetu huu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo tuseme kwamba kifungu cha 23 kiko katika sehemu ya fedha tafauti na kile kilichokuweko katika kifungu cha 11.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha 32(1) na (2) ambacho kinasema: "Malipo ya Wajumbe wa Tume yatalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kiwango ambacho kitaamuliwa na Rais".

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba Wajumbe wa Tume wanateuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 119, ingawa wajumbe hawa mwanzo walikuwepo katika sheria hii lakini sasa kukaleta mgongano kidogo wa kisheria baina ya sheria hii na Katiba, sasa ndio maana ikaonekana ipo haja ya kuiachia mamlaka kikatiba, lakini ukisoma katika sheria yetu ya uchaguzi kifungu cha 133 kimeainisha wazi kwamba, Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi watalipwa mishahara yao na posho pamoja na mafao mengine kama itakavyoamuliwa na Rais kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo, kilichofanyika hapa katika mswada wetu huu wa Sheria ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi ni kuwa kilichokuwepo katika Sheria ya Tume ya Uchaguzi lazima kiende sambamba na kile kilichokuwepo katika Katiba, na ndio maana kilichokuwepo hapa tumejaribu kwenda sambamba na Sheria ya Tume ya Uchaguzi ambayo tayari ilishaelekeza namna gani wajumbe hawa watakuwa wakipokea malipo yao kwa mujibu wa kazi ambazo watakuwa wamezifanya.

Mhe. Naibu Spika, tukirudi nyuma kidogo katika kifungu cha 4 kinachoelezea Tume itakuwa na majukumu yafuatayo: Hapa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wengi kati yao waligusa pamoja na kuwepo kwa muundo wa Tume ya Utumishi katika Tume ya Uchaguzi. Sasa tukubaliane nao Waheshimiwa kwamba hata na sisi tunaona ipo haja ya afisi hii ya Tume ya Uchaguzi kuwa na muundo wa utumishi ambao utaweza ku-*govern* baadhi ya mambo yao na majukumu ya kila siku; ndio maana baadhi ya Waheshimiwa walipendekeza kwamba katika kifungu hiki kwa sababu kutakuwa kuna kifungu 4(1) lakini hata katika kifungu 4(2) ambacho kimesema: "Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume itatekeleza majukumu yake kwa kufuata Katiba, Sheria na misingi ya demokrasia na utawala bora".

Tunashukuru *concern* ya baadhi ya Wajumbe ambao wamependekeza, nasi tunaungana nao katika hili kwamba, katika kile walichokisema kuwa tuongeze kifungu kimoja kidogo ili kije kiwe 4(2) halafu 4(3) ndio hii ambayo 4(2) kama ilivyokuwepo hapa, ambacho kitasomeka, "Kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao, Tume itaandaa na kuweka na kupendekeza muundo wa Tume ya Utumishi na watendaji wake utakaozingatia sifa na majukumu ya kila mtendaji".

Mhe. Naibu Spika, tumeona ni vyema jambo hili pia likaongezwa likaweko katika sehemu hii kwa dhamira ya kuleta ufanisi uliokuwa bora kwa watendaji wetu hawa wa Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mikubwa ambayo wameiwasilisha sambamba na kuitengeneza sheria hii kuwa bora zaidi. Pamoja na hayo nakubaliana na wazo lililotolewa na Mhe. Rashid Makame Shamsi kwamba katika Sehemu yetu ya Kwanza kwenye kifungu cha 2 ambacho ni sehemu ya utangulizi katika ufafanuzi ni vyema maneno haya yawe katika *alphabetical order*, kama utaratibu mwengine uliokuwepo katika sheria. Bahati mbaya ukisoma mswada wetu ambao umetoka kwa lugha ya Kiingereza wenyewe tafsiri au ufafanuzi huu upo katika *alphabetical order*, lakini katika Mswada huu wa Kiswahili kutokana na uharaka uliokuwepo haukuwa *arranged* ile *alphabetically*. Kwa maana hiyo, wazo hilo Mhe. Mjumbe tutakuwa tumelizingatia na tutalifanyia kazi.

La pili, ni kwamba ilikuwepo hoja ya fidia hasa kwa wajumbe ambao watakuwa wamepata kadhia kwa namna moja au nyengine katika utekelezaji wa majukumu yao, ima iwe katika kipindi cha uandikishaji au iwe katika wakati wa uchaguzi. Kama ambavyo Wajumbe wa Kamati pia walishauri katika hili na sisi tumekubaliana nao kuwa watumishi ambao watakuwepo ama

wajumbe, yeyote atakayepata tatizo lolote akiwa katika majukumu yake haya tumeona sasa ni vyema sheria hii ikaja ikampa fidia. Kwa sababu katika kipindi cha nyuma uzoefu unaonesha wako baadhi ya watendaji wa Tume ya Uchaguzi ambao wamepata madhara katika utendaji wa kazi zao ama uwajibikaji wa majukumu yao na hawakuwa wakipata chochote kwa mujibu wa sheria. Sasa tumeona sheria hii itakapokuja itawalinda hata pale ambapo watakuwa wakipata madhara kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, jengine ukisoma katika kifungu cha 29(1) ambacho kinasema kwamba:

"Mtu yeyote ambaye-

(a) kwa makusudi atamzuia mjumbe wa Tume au Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Tume kutekeleza majukumu yake; au

(b) kwa makusudi ataharibu mwenendo wa mkutano wa Tume..."

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba haya yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyatoa mengi yao yamezingatiwa, lakini mengi yao baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walijaribu kuyazungumza yote, yameainishwa katika sheria yetu ya Tume ya Uchaguzi. Ni vyema tu Waheshimiwa Wajumbe wakafahamu kwamba kilichokuwepo hapa ni kutoa ule mgongano mkubwa wa kisheria uliokuwepo baina ya sheria ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi sambamba na kifungu cha 119 cha Katiba ya Zanzibar, ndio maana yamefanyika mabadiliko haya makubwa katika uundwaji wa sheria hii ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, tuseme kwamba mengi ambayo Wajumbe wameyazungumza wametu-*alert* hasa katika sheria ya Tume ya Uchaguzi ambayo mengine yako sawa, lakini na pia tumeshauriana na kuona kwamba ipo haja baadae kuja kuitizama upya sheria yetu ya uchaguzi ili kuja kuifanyia maboresho mazuri zaidi yatakayokwenda sambamba na Katiba yetu ya Zanzibar, lakini pia itakwenda sambamba na sheria yetu hii ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme baada ya kusema hayo machache na kwa ufupi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ni vyema tukawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe watuunge mkono kuipitisha sheria hii ambayo itakuwa na manufaa na mustakabali mwema katika taifa letu, kila ifikapo wakati wa utekelezaji wa haya ambayo tutakuwa tumeyaainisha. Kwa sababu kupita kwa sheria hii tutaendelea kuwapa nguvu wenzetu wa Tume lakini pia itaweza kutoa adhabu.

Mhe. Naibu Spika, pia Wajumbe wengi walizungumzia suala zima la waangalizi wa ndani na nje kama ambavyo sheria imeainisha. Ushauri wao ni mzuri tunauchukua na tutauzingatia. Lakini sambamba na hilo sheria hii imependekeza adhabu, lakini tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambao nao pia walipendekeza zaidi baadhi ya adhabu na wengine kufikia kusema kwamba adhabu ni ndogo ziongezwe. Sisi Wajumbe watakachokiamua kwamba adhabu zile ni ndogo ziongezwe tutakuwa tayari ili kuweka mambo haya yote kuwa katika hali ya usawa.

Mhe. Naibu Spika, zile indhari nyengine ambazo wamezisema kuhusiana na waangalizi zote tutazichukua...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nashukuru zinanitosha. Sasa nasema kwamba tutazichukua na Mhe. Waziri atakapokuja kutunga kanuni zake basi kanuni hizo zitakuja, na muongozo mkubwa na ufafanuzi zaidi katika baadhi ya mambo haya ya uangalizi katika kipindi cha uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena kusema naunga mkono hoja kwa mswada huu, kwa sheria hii kupita na tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe watusaidie kwa pamoja ili sheria hii ipate kupita na kufanikisha na kuleta utekelezaji bora wa majukumu ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu katika kikao hiki.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia uniruhusu niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa namna ambavyo siku zote wanashirikiana na serikali na kusimamia vizuri shughuli zao ili tuweze kufanikisha yale malengo ya kuwahudumia wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Aidha, shukrani maalumu nizitowe kwenye Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambayo imefanya kazi nzuri katika kutoa michango yake na katika kusimamia mchakato mzima wa kuiwezesha sheria hii iwe bora zaidi, nashukuru sana. *(Makofi)*

Pongezi maalumu nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote. Lakini nimshukuru sana Makamu Mwenyekiti kwa uwasilishaji mzuri kwa taarifa na maoni ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hoja yetu hii imechangiwa na wajumbe 39. Katika 39 hao, 33 wamechangia kwa maneno na wajumbe 6 walichangia kwa maandishi. Kwa hivyo, naomba wote niwashukuru na kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu niwatambuwe Waheshimiwa Wajumbe waliochangia mswada huu wa sheria. Kwanza nianze na;

1. Mhe. Bi Panya Ali Abdalla — Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Miraji Khamis Mussa
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Asha Abdalla Mussa
6. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
7. Mhe. Omar Seif Abeid
8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Machano Othman Said
10. Mhe. Mohammed Ahmada Salum
11. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini
12. Mhe. Suleiman Makame Ali
13. Mhe. Mussa Ali Mussa
14. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
15. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
16. Mhe. Mussa Foum Mussa
17. Mhe. Hidaya Ali Makame
18. Mhe. Salma Mussa Bilal
19. Mhe. Shehe Hamad Mattar
20. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
21. Mhe. Yussuf Hassan Idd
22. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
23. Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud
24. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

25. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
26. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
27. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
28. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
29. Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
30. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
31. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
32. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
33. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri naomba utambuwe mchango wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid amenileta mchango wake wa maandishi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Rashid Ali Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa michango ya maandishi ni;

1. Mhe. Ussi Yahya Haji
2. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
3. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
5. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
6. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
7. Mhe. Miraji Khamis Mussa
8. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo

Sasa Mhe. Naibu Spika, wamefikia Wajumbe 41 baada ya kuwataja hao.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimshukuru sana kiongozi wetu wa shughuli za serikali hapa Barazani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ambaye yeye ndiye mwenye ofisi hii, kwa maelekezo yake na muongozo wake na kutuwezesha sisi tuliokuwa chini yake kufanyakazi zetu vizuri. *(Makofi)*

Pia nichukuwe fursa hii kumshukuru na kumtambua Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, na watendaji wote wa wizara yangu kwa namna wanavyotupa mashirikiano makubwa.

Shukrani maalumu ziende kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, wajumbe wake na Mkurugenzi na watendaji wote wa Tume ya Uchaguzi kwa kazi kubwa waliyoshirikiana nayo katika kukamilisha mswada huu mpaka ukafikia mbele ya Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, shughuli za uchaguzi wa Zanzibar zina historia ndefu sana na zimeanza muda mrefu, tokea kabla ya Mapinduzi, baada ya Mapinduzi na wakati wa mfumo wa chama kimoja na wakati huu wa mfumo wa vyama vingi. Kwa hivyo, katika miaka ya 1980 tulikuwa na sheria ya Tume ya Uchaguzi ambayo ilikuwa inaendana na mwelekeo wa mfumo wa chama kimoja, lakini baada ya kuanza kwa mfumo wa vyama vingi, ndio maana mnamo mwaka 1962 kwa sheria namba 9 iliundwa maalumu sheria ya Tume ya Uchaguzi iendane na matakwa hayo ya mfumo wa vyama vingi, na tokea wakati huo mpaka hii leo ndio sheria ambayo tulikuwa tumetumia.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na mabadiliko makubwa ya Katiba ya Marekebisho ya Nane, imeonekana ipo haja ya msingi ya kufanya marekebisho katika chombo chetu hiki cha kusimamia shughuli za uchaguzi. Kwa hivyo, ndio maana serikali kwa makusudi ikaamua kufanya mabadiliko haya ya marekebisho ili yaendane na matakwa ya Katiba, lakini pia kuongeza ubora wa sheria yetu ili iweze kusimamia vizuri shughuli zetu za uchaguzi ili ziweze kukidhi haja ya wakati wa sasa. Kwa hivyo, ndio maana tukaamua kwa makusudi kuleta sheria hii.

Na mimi nawashukuru sana wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa namna ambavyo wameichangia na kuiboresha na kufikia hatua nzuri. Naamini sasa tutakuwa na sheria iliyokuwa bora zaidi itakayosimamia mambo yetu vizuri zaidi na itakayoweka mipango mizuri ya kuendeleza chaguzi zetu zinazokuja. Kwa sababu chombo hiki ndicho kina mamlaka ya kusimamia uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, wengi wetu katika michango hapa wakati tunachangia tulikuwa tunachanganya kati ya Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi.

Tume ya Uchaguzi ndio chombo makhususi cha kusimamia shughuli za uchaguzi, lakini chombo haswa kinachosimamia shughuli za utawala, bajeti yenyewe na mambo mengine yanayohusiana na uchaguzi. Lakini sheria ile ya

uchaguzi yenyewe inasimamia mchakato mzima wa uchaguzi, kuanzia uandikishaji, uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, taratibu za kupiga kura, taratibu za kuhesabu kura, taratibu za kutangaza matokeo na kadhalika.

Kwa hivyo, sheria ya uchaguzi ndio inayotupatia viongozi mwisho wake. Sheria ya Tume ya Uchaguzi hiki ni chombo kinachosimamia kwa ujumla wake, kwa maana ya ofisi, kwa maana ya rasilimali watu, kwa maana ya bajeti na kusimamia shughuli za uchaguzi ziende vizuri. Kwa hivyo, naamini Waheshimiwa Wajumbe, tutakuwa tumeelewana vizuri, kuelewa kwamba Tume ni chombo kinachosimamia shughuli za uchaguzi, na sheria ya uchaguzi ndio hasa inasimamia mchakato mzima wa uchaguzi. Wajumbe wengi wetu hapa maoni yao yalilenga zaidi kwenye sheria ya uchaguzi. Lakini sio vibaya tumepata mawazo hayo na pale tutakapokuja kufanya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi yatasaidia, na wakati huo ukifika, basi naamini kwa umahiri wa wajumbe watazidisha kuichangia zaidi na pia katika mwelekeo huo tutapata sheria iliyo bora zaidi wakati ukifika. Lakini kwa leo tunazungumzia sheria ya Tume ya Uchaguzi ambayo ndio tunayoizungumza na ambayo tunaitaka iwe bora zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka niendelee tena kuishukuru sana kamati kutokana na michango yake, ambayo kwa njia moja ama nyengine imeboresha mswada huu wa sheria.
Mimi nataka niseme mbele ya Baraza lako tukufu kwamba yale maoni na marekebisho ambayo Kamati wameyawasilisha katika jadweli lao, sisi kwa upande wa serikali tunakubaliana nayo kwa asilimia mia kwa mia. Kwa maana hiyo yatakuwa ni sehemu ya sheria hii, na hata vile vifungu ambavyo wameamua kuviondoa tunakubaliana navyo. *(Makofi)*

Kwa mfano, kifungu kile cha 15(2) ambacho kimezungumzwa sana hapa na Waheshimiwa Wajumbe, akiwemo Mhe. Dk. Sira Ubwa, tayari yale mawazo ya Mhe. Dk. Sira na baadhi ya wajumbe wengine yalikwisha kufanyiwa kazi na kamati yetu. Kwa msingi huo basi, kifungu kile cha 15(2) kinaondolewa na kinabakia kifungu cha 15 peke yake ambacho kinakidhi haja ya maelezo yale. Kwa hivyo, tunawashukuru sana Kamati kwa mtazamo wao mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na masuala ya majengo ya ofisi za Tume ya Uchaguzi. Waheshimiwa Wajumbe wamelizungumzia sana hili kwa upana wake, eneo la ofisi za Tume ya Uchaguzi, kwa maana ya Makao Makuu pamoja na za wilaya.

Nataka niwahakikishie wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba kutokana na ziara iliyofanywa na Mhe. Rais wetu katika Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi pale Maisara Zanzibar. Mhe. Rais tayari ametoa maelekezo mazuri sana, yanayohusiana na kuimarisha majengo yale, yanayohusiana na kuupa umiliki majengo yale kuwa ya Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo Tume ilikuwa ina majengo mawili tu pale mwanzo walikuwa wakiyatumia. Sasa hayo mawili kwa taratibu zinavyoendelea watayamiliki yatakuwa ni mali yao, na bado jengine la tatu ambalo liko jirani pia maelekezo yametoka ili nalo liwe chini ya Tume ya Uchaguzi. Sio kwamba kupewa tu, lakini pia kuna maelekezo ya namna ya kuyakarabati majengo hayo, ili yaendane na dhamira na haja ya Tume yenyewe, ili Tume yetu ya Uchaguzi iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi na katika mazingira yaliyo bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, juu ya hivyo bado kuna maeneo mengine pale pale inaonekana pia kwa mtazamo wa serikali watapewa Tume ili wazidi kuendeleza kuwa na eneo kubwa zaidi la kujiimarisha kwa shughuli zao za Tume ya Uchaguzi. Lakini sio hayo tu Mhe. Rais pia ameshatoa maelekezo ya namna gani Tume ya Uchaguzi iweze kuwa na ofisi zake za wilaya. Maelekezo hayo yameshatolewa na tayari mimi na Mhe. Waziri anayesimamia mambo ya ardhi tumetakiwa kulisimamia jambo hili, ili mwisho wa siku Waheshimiwa Wajumbe wa Tume ambao wataweka ofisi zao katika ofisi za wilaya, basi na ofisi za wilaya nazo ziwepo ziweze kufanyakazi zake kwa mujibu wa mahitaji ya Tume yenyewe.

Pia kulikuwa na malalamiko ya Tume kuhusu magari. Mhe. Rais pia ameshatoa maelekezo kuhusu magari kwa Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, kwa ujumla wake Tume imewekewa utaratibu mzuri wa kuweza kufanyakazi zake na kuwa na mawasiliano mazuri katika shughuli zake. Naamini Wajumbe wetu wa Tume, pamoja na watendaji wa Tume watakuwa wameridhika sana na mtazamo huo wa serikali, kwa nia ile ile ya kuwawezesha wafanye shughuli zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo limezungumzwa sana katika kikao hiki ni suala la wagombea kujitangazia matokeo.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kwa sheria ya sasa ya uchaguzi namba 11 ya mwaka 1984 kifungu 42(5), kinakataza kabisa kabisa kwa mgombea kujitangazia matokeo. Kwa hivyo, ni kinyume na sheria, na unapofanya hivyo utakuwa umefanya kosa na adhabu inapaswa kutolewa kwa

mujibu wa sheria. Kwa msingi huo ni lazima tufikie mahala sote tuamini kwamba kujitangazia matokeo ya uchaguzi, ni jambo ambalo linaweza kusababisha mtafaruku mkubwa, linaweza kuvunja amani ya nchi yetu na umoja wetu, na ni jambo ambalo sio zuri hata kidogo. Kwa hivyo, lazima kama Wazanzibari wenye imani na nchi yetu tufikie mahala tuheshimu sheria na kufuata taratibu ili kuepukana na vitendo vyote ambavyo vinaweza kuhatarisha amani ya nchi yetu, usalama wetu na umoja wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo kama ile sheria adhabu yake kwa sasa ni ndogo, basi wakati utakapofika katika kufanya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi, tutaweza kuliangalia zaidi na tuitazame adhabu ile, tukiona ni ndogo ili tuifanye iwe ni kubwa zaidi na tuweze kusimamisha kwa mtu yeyote yule mwenye nia ya kujitangazia asifanye hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la waangalizi wa uchaguzi, wale wanaopotosha ukweli, ama wanaoandika taarifa za uongo, ama taarifa zao wasioziwasilisha kwenye Tume ya Uchaguzi. Kwa sasa ipo sheria, umewekwa utaratibu wa kisheria ambao kwenye mswada wetu huu ulikuwa unaonesha kwamba adhabu iwe faini isiyopungua milioni 3 na isiyozidi milioni 5. Lakini sasa sisi tunapokea ushauri kwa wajumbe ambao walitaka tuongeze adhabu. Sisi tunafikiria sasa adhabu iongezeke pia kiwemo na kifungu kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka 5, au zote adhabu mbili kwenda kwa pamoja. Kwa hivyo, pale tutafanya marekebisho ili kuongeza hizi adhabu kwa msingi wa kutaka nidhamu na zile taratibu zifuatwe, ili waangalizi wanapokuja nchini kwetu kutaka kuangalia masuala ya uchaguzi, basi wafuate taratibu zilizowekwa kwa msingi wa kuepuka mambo yote ambayo yanaweza kupotosha ukweli wenyewe, au kuhatarisha amani na usalama wa nchi yetu.

Vile vile tunafikiria na ninaamini Waheshimiwa Wajumbe mtatuunga mkono, kwamba tutaongeza kifungu cha 6 kitakachosema kama ifuatavyo.

Kifungu cha 6

"Mtu yeyote au taasisi yoyote itakayotiwa hatiani, hatoruhusiwa kuomba tena kuwa muangalizi wa uchaguzi wa Zanzibar katika kipindi cha miaka 10"

Wanasheria watakiweka vizuri zaidi. Lakini hii yote ni kuongeza adhabu ili wale ambao wanakuja kuwa waangalizi wafuate taratibu na sheria zilizopo.

Pia tutaweka katika Kanuni zetu utaratibu ule ambao uliopendekezwa sana na Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame kwamba wasiwe wanajiamulia wao kituo cha

kwenda kuangalia, bali Tume yenyewe ndio ipendekeze maeneo gani waangalizi hao waende.

Vile vile na mkazo kwa upande wa Pemba ufanyike. Kwa sababu hawa waangalizi wengi wanaokuja kutoka nje walikuwa na maeneo maalumu kwa hapa mjini tu. Sasa utaratibu kwamba Tume ndio itawapangia, ukiambiwa wewe uende Chokocho utakwenda Chokocho, ukiambiwa uende Kisiwapanza utakwenda Kisiwapanza, ukiambiwa uende Kojani utakwenda Kojani, ni Tume yenyewe ndio itaamua, ukiambiwa uende Makunduchi utakwenda Makunduchi. Utaratibu huo sasa tutauweka kwenye kanuni ili kuepuka matatizo ambayo yamejitokeza ambayo yameleta athari kubwa katika chaguzi zetu. Nyote ni mashahidi kwamba matatizo makubwa ya Zanzibar yanaanza mara baada ya matokeo ya uchaguzi ama wakati wa uchaguzi wenyewe.

Kwa hivyo kila jambo ambalo Wajumbe walilisema hapa walikuwa wanalisema kwa nia njema, kwa dhamira njema kuepukana na migongano na matatizo yanayojitokeza katika kipindi cha uchaguzi na baada ya uchaguzi, yapo maelezo yaliyotolewa na wajumbe kwenye msingi ya kwamba mabango ya wagombea kuna watu wanayaharibu mabango hayo ya wagombea, ipo adhabu katika sheria ya uchaguzi inayoelekeza wanaoharibu mabango ya wagombea, lakini hata hiyo adhabu kama tutaiona ndogo wakati ukifika tutakapofanya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi nayo tunaweza kufanya mabadiliko ya kuongeza adhabu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna ushauri kwamba jina la Tume liongezwe kutoka jina la sasa la Tume ya uchaguzi wa Zanzibar na liwe jina la Tume ya Uchaguzi na kugawa mipaka, jambo hilo halitowezekana, kwa sababu jina lile la tume ya uchaguzi linatokana na matakwa ya Katiba, hivyo tutaendelea kuheshimu matakwa hayo ya katiba na jina litabakia hivyo hivyo Tume ya uchaguzi ya Zanzibar, kwa sababu msingi wetu sote hapa ni kuheshimu katiba, na ndio dira kuu ya sheria zetu, kwa msingi huo naamini waheshimiwa Wajumbe hata wale waliotaka jina liongezeke watakubaliana nami kwamba tusimame na jina la sasa. Kwanza jina lenyewe linapendeza hivyo lilivyo lakini pia ni matakwa ya kikatiba.

Vile vile kuna ushauri umetolewa kuhusu wanaotoa ruzuku au kusaidia shughuli za uchaguzi hapa Zanzibar wasiingilie mambo ya ndani ya uchaguzi wa Zanzibar ni kweli kabisa ushauri huu ni sahihi na sisi tunaupokea na tutakaa na wenzetu wa Tume kuzidi kuwaeleza, katika kanuni ambazo Waziri atazitunga baadae basi moja iwe ni jambo hili nalo lipewe mkazo maalumu, hatuwezi kuingiliwa katika masuala yetu ya uchaguzi, kwa sababu hata sisi

ikitokea kuchaguliwa kwenda kuwa waangalizi wa nchi nyengine tunafuata sheria zilizoko pale na taratibu zilizopo pale, sio kuingilia mambo ya ndani ya nchi, hayo hayawezekani.

Sisi tuna taratibu zetu, kuna utamaduni wetu, kuna sheria zetu, kwa hivyo inabidi ziheshimiwe wale wanaokuja kutaka kutusaidia tuungane nao, acha tuungane nao kwa kutusaidia lakini si kwa kuamua mambo yetu ambayo tayari yapo katika misingi ya kikatiba na kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Tume hili ni suala la kikatiba, lipo tokea kifungu cha 119(1) n (2) cha katiba, kwa hiyo hayo ni mambo ambayo vile vile waheshimiwa wajumbe tungeendelea kuyaheshimu.

Vile vile napokea ushauri wa Mhe. Hassan Khamis Hafidh maarufu *(Diaspora)* ambaye alizungumzia kile kifungu cha 11(2)(a) kuhusu suala la kushtaki na kushtakiwa kwa Tume tunakubaliana naye na kifungu kile sasa tuna ki- *drop*, kwa maana hiyo kitakuwa kimeondoka. (*Makofi*)

Kuhusu suala la vitambulisho vilivyokaa kwa muda mrefu zaidi ya miezi sita, zaidi ya miaka vipo pale nakubaliana na ushauri uliotolewa, ni kweli lazima kuwe na utaratibu baada ya kukaa na vitambulisho hivyo, muda mrefu uwepo utaratibu wa kuviharibu, huwezi kukaa na vitambulisho milele wenyewe hawakujitokeza kwa wakati maana yake wenyewe hawapo au ilikuwa ni mbinu na njama za kutengeneza mtu vitambulisho viwili vitatu kwa majina tofauti, kwa msingi huo ndio maana wanashindwa kuvichukua, lakini mwenyewe hasa aliyekuwa mhalisia mwenye kitambulisho chake hawezi kukaa zaidi ya miaka miwili mitatu bado hajenda kuchukua kitambulisho chake. Utaratibu huo tutaweka muda maalumu ambao mwananchi awe amechukua kitambulisho chake na baada ya hapo basi tutaweka utaratibu utakaotusaidia kuvifuta hivyo ambavyo havijachukuliwa.

Suala la kuharakisha kutunga kanuni tunakubaliana kabisa kabisa kwamba jambo hili ni jambo zuri, mara baada ya sheria hii kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mhe. Rais basi kuharakisha kutunga kanuni itakuwa ni moja katika wajibu wetu, na nataka kuwahakikishia Waheshimiwa tutafanya hivyo mara utakapomalizika ule mchakato wa kisheria.

Kusikiliza maoni ya wananchi wakati wa kugawa majimbo huo ndio utaratibu wa siku zote wa Tume kusikiliza maoni ya wananchi wakati wa kugawa majimbo, lakini sio kila maoni au ushauri unaotolewa na wananchi utakuwa ndio huo huo utawafaa Tume katika kufanya maamuzi yao. Msingi ni kusikiliza

maoni ya wananchi na ushauri unaotolewa, lakini Tume sasa wanapima ni vipi vya kufanya mambo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Kuhusu malipo ya fidia. Ilikuja hapa je watendaji wale wa muda na watendaji watapata haki iliyosawa na wenzao katika malipo ya fidia. Ni kweli kwamba watendaji wote watakaoshiriki katika shughuli za uchaguzi wakati ule wamo wanafanya kazi za Tume, kwa hivyo nao wote watakuwa wanapata fidia, wale wa muda na wa kudumu. *(Makofi)*

Afisa za uchaguzi wa Wilaya, Afisa uchaguzi wa Wilaya ndio atakuwa afisa mkuu wa uchaguzi katika Wilaya husika, na kwa msingi huo ikiwa jimbo au majimbo katika Wilaya yeye ndio atakuwa msimamizi mkuu wa shughuli hiyo, kwa hivyo yeye atakuwa na dhamana ya kusimamia shughuli katika Wilaya husika. Atakula kiapo kwa mujibu wa sheria yetu, alichofanya sasa atakula kiapo mbele ya hakimu wa Mkoa.

Kuhusu wale ambao hawana uwezo wa kupiga kura lakini hapa limezungumzwa kwamba kuna watu vijana kabisa wana afya zao, wazima, wanajua na wana uwezo wa kupiga kura lakini kwa sababu tu ya mbinu za kisiasa hufanya mbinu kwamba lazima upigiwe kura na mtu fulani, ili kuamini kwamba mtu huyo kura yake ataitia kwa mahitaji unayoyataka wewe. Ukweli tuwaachie wananchi waamue viongozi wao wanaotaka kama mwenye uwezo wa kupiga kura huyo akapige kura yake, kwa wale ambao ni wagonjwa au wana sababu za msingi kwa hivyo maafisa wanaosimamia shughuli za uchaguzi ndio watatoa majibu katika kituo husika kwamba huyu anafaa kupiga kura mwenyewe na huyu inafaa apigiwe kura, ili kuwapa uhuru wa kufanya maamuzi yao. Si vizuri watu kuwalazimisha au kuwafanyia mbinu hizi na hizi asipate fursa yake ya kidemokrasia na ya kikatiba ya kuchagua kiongozi anayemtaka, jambo hilo sio jambo zuri sana.

Kwa hivyo kura ni haki ya mtu, ni wajibu wa mpiga kura mwenyewe kwenda kupiga kura yake. Kwa hivyo elimu itatolewa zaidi kuelimisha wananchi wetu waelewe umuhimu na thamani ya kura yake.

Kuhusu maslahi ya watendaji wa Tume na wafanyakazi wa Tume. Hawa ni wafanyakazi wa umma, kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri alilieleza vizuri jambo hili kwa vile ni watumishi wa umma maslahi yao yatakuwa chini ya Sheria ya Utumishi wa umma, na kwa sababu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbali mbali za kuimarisha maslahi ya utumishi wa umma na hivi karibuni nyote mmesikia Mhe. Rais ameshatoa muongozo hata wa kima cha chini kwamba kuanzia mwezi wa nne hapa kima cha chini cha Mshahara

kitakuwa ni shilingi laki tatu, haya yote ni kuona namna gani watumishi wa umma wanaangaliwa vizuri na kadiri ya uwezo wa Serikali yetu basi hatua kwa hatua suala la mishahara na maslahi mengine ya utumishi wa umma yatakuwa yanasikilizwa.

Mimi naamini sana kwamba watendaji wa Tume watapenda sana kupata fursa hii ya Sheria ya utumishi wa umma. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila mmoja wetu anapata maslahi vizuri na maisha yanakwenda vizuri.

Kuhusu suala la elimu ya wapiga kura nawahakikishia waheshimiwa Wajumbe jambo hili ndio mtazamo mkubwa wa Tume ya uchaguzi, na ni mtazamo wa Serikali kwamba wananchi wapate elimu ya mpiga kura, ili waweze kuelewa haki zao za msingi za shughuli nzima au mchakato mzima wa kupiga kura pamoja na kujua kabisa elimu ya uraia ili waweze kufanya maamuzi vizuri wakati wa uchaguzi. Kwa hivyo ushauri huu tunaupokea na tunaufanyia kazi hasa ule ambao ulitolewa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu akielezea kwamba ni vizuri kabisa kwa Tume kushirikiana na taasisi za elimu hususan Wizara ya Elimu katika kutoa elimu hiyo, naona ni ushauri makini na ni sahihi, tunaunga mkono suala hili.

Kuhusu siri na usalama wa mpiga kura ni jambo la msingi sana, naunga mkono sana jambo hili na tutalichukua tulifanyie kazi tuhakikishe kwamba kura ya mtu ni siri na usalama wakati anapopiga kura. Ni kweli kuna baadhi ya watu huwa wanawalazimisha wananchi ni lazima wawapigie kura huo sio msingi wa uchaguzi, msingi wa uchaguzi huru na haki kila mmoja atumie haki yake kuamua kiongozi anayetaka sio mambo ya kulazimishana. Kwa hivyo bado Serikali itashirikiana sana na Tume ya uchaguzi kuhakikisha usalama wa wapiga kura wetu, usalama wa wananchi wetu na siri inakuwepo katika mchakato mzima wa uchaguzi, kwa hivyo ushauri huu tunaupokea na tunaendelea kuufanyia kazi.

Suala jengine ambalo kubwa na limezungumzwa sana ni suala la faini na adhabu katika sheria hii. Waheshimiwa Wajumbe ni kweli ukitizama unaweza kuona adhabu iliyomo humu na faini zilizomo humu ni ndogo, lakini kwa upande mwengine adhabu inatolewa kutokana na kipimo cha kosa lenyewe, na kwa kupitia wanasheria wetu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wameona kwamba adhabu zilizotolewa na hizi ambazo tumezifanyia marekebisho zinakidhi haja kwa hali ya sasa. Kwa hivyo ni vyema tukaanza kama yalivyo marekebisho na zilivyopendekezwa, na pale ambapo tutaona katika kufanya hii shughuli yenyewe tukiona hizi adhabu hazikukidhi haja tunaweza kuleta hapa kwa marekebisho, lakini tunaamini sana kwamba adhabu zilizotolewa hizi

zinaweza kabisa kabisa kukidhi haja ambayo imeonekana ndani ya sheria yenyewe, kama kutakuwa na suala lolote la kuhitaji adhabu za ziada basi Mhe. Naibu Spika, hatutochelea kufanya mabadiliko ya sheria ili tuyalete hapa, lakini mimi naamini na kama wanasheria wetu walivyotushauri kwamba jambo hili linaweza kusaidia, kwa maana adhabu zilizokuwepo pale na zilizofanyiwa marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya na Waheshimiwa Wajumbe naomba nisirudie kusema maneno mengi mbele ya Baraza lako tukufu, bali nirudie kusema kwamba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na naamini wataupitisha mswada huu kwa maslahi ya taifa letu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe naomba kutoa hoja ili tuendelee na hatua nyengine zilizopangwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja wale wanaoafiki hoja hiyo wanyooshe mikono, wasioafiki, wanaoafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kupitisha Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi na Naibu Waziri katika kuchangia niliomba tafsiri ya ufafanuzi wa Mhuri na nembo, sikuyasikia na ndani ya mswada huu hivi vitu vimeelezwa naomba majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ndio kwanza tumeanza kifungu cha kwanza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Tuendelee Mheshimiwa nasubiri kifungu cha pili kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Umeelewa hiki ni kifungu cha kwanza hamna tafsiri hapa, subiri mpaka kifungu cha pili ndio utakuja kuitafsiri.

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika.

Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kurejea maelezo, kwa sababu yalishasomeka nilikuwa na haraka tu ya kujibiwa kunako muhuri na nembo nilichangia na nikadai ufafanuzi wake, kwa sababu yamesomeka kwenye mswada huu hawakunipa maelezo naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa kwa kuwa jambo hili limetajwa katika Sheria ya tafsiri Sheria Namba 7 ya mwaka 1984 hiyo ndio maana ya tafsiri ya Nembo na Muhuri.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kusomeka kwenye sheria lakini hapa tunaandaa chombo ni bora tukaelekeza maelezo yetu tafsiri hii ya nembo na muhuri ikapatikana kwenye sheria isiwe wazi kama hivi, kwa sababu nembo ziko nyingi. Sasa naomba Mhe. Waziri ukubaliane na hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli jambo la kisheria na limetafsiriwa kama ilivyo kwenye sheria, na kwa sababu jioni hii tunakuja kusoma mswada mwengine unaohusiana na nembo, bendera na kadhalika. Naamini mambo haya yatapata majibu vizuri, kwa sasa tungeheshimu ile sheria iliyopo tukenda kama vile ili tuweze kuendelea. Namuheshimu sana Mhe. Miraji Khamis Mussa na nakubaliana na maoni yake lakini huo ndio utaratibu, siwezi kuzidisha zaidi kwa sababu nina mambo ya kisheria.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti Mswada ujao unazungumzia bendera na nembo zitakazotumika za taifa. Hapa tunazungumzia nembo na muhuri wa Tume sasa tusichanganye hizi habari za nembo tutakayokuja kuijadili jioni na muhuri tunaoujadili sasa, ni kukubaliana tu kwa tafsiri ya nembo na muhuri tuiandike kuwa itapatikana kwenye sheria ya uchaguzi basi ndio tumemalizana na hili, hapo tu mimi ndio ninapotaka tukubaliane na Mhe. Waziri si jambo jengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nadhani Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameeleza vizuri, kama unapotaka kutafsiri sheria vizuri inabidi kwanza usome Sheria ya Tafsiri Nam.

7 ya mwaka 1984, litizame ndani ya sheria ile mna maneno gani ambayo tayari yameshapewa tafsiri. Kuna maneno ambayo tayari yameshapewa tafsiri huna haja ya kuleta tafsiri yako nyengine ambayo tayari imeshatafsiriwa. Sasa nadhani Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amelieleza vizuri jambo hilo na ningedhani ingetosha kwa mchango ambao ameutoa Mhe. Waziri.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kidogo yana muelekeo, na kwa leo nitaruhusu tuendelee kwa sababu hiyo sheria aliyoitaja sijaipitia, basi sitokuwa na *evidence* ya kuendelea. Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu 2 Ufafanuzi

Sura ya Pili

Kuanzishwa Majukumu na Uwezo wa Tume

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Muundo wa Tume Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 4

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri alipokuwa anatoa maelezo katika kifungu cha 4(3) nilisema tukiongeze na kisomeke, kifungu cha 4(3) alisema kuna nyongeza ambayo itasomeka kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume itaandaa na kuweka na kupendekeza muundo wa utumishi kwa watendaji wake watakaozingatia sifa na majukumu ya kila mtendaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana sana na Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa kukubali kwanza Tume kuwa na Muundo wa Utumishi unaojitegemea hasa kwa kuzingatia ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja yako.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nataka kwenda kwenye hoja, lakini ni lazima niseme ili wenzangu waweze kunifahamu, maana hoja haiji tu kama sijajaribu kutoa na maelezo kidogo. Maana vyenginevyo sote tuwe tunaishi kwa wahyi, mimi niishi kwa wahyi, huyo ninayemwambia aishi kwa wahyi, ndio atakuwa anajua nini ninachokisema.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunapitisha vifungu, nenda kwenye hoja ambayo unahisi hapa kwamba umeomba marekebisho yafanyike na sio maelezo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na kunipeleka kwa kasi, lakini ninachotaka kukisema kile kipengele kwanza nakubali mawazo ya Serikali lakini sio kwa utaratibu kama kinavyosomeka kipengele kile. Nina wazo na naomba Waheshimiwa Wajumbe wanikubalie. Wazo langu ni kwa ajili ya utekelezaji bora kwa majukumu yake Tume itakuwa na muundo wa Utumishi kama ifuatavyo, tuuweke kabisa ule muundo wa Utumishi hapa wakati tunatunga Mswada wa Tume ya Utumishi kuliko kuiachia Tume ya Utumishi iende ikaandae, tutakapofika pahala tunaiwachia Tume ya Utumishi, tutarudi kule kule.

Mimi mapendekezo yangu ya huo muundo nilimuachia Mhe. Waziri, naomba sasa tukubaliane na yale mawazo ambayo nimempa. Mhe. Mwenyekiti, nataka hayo majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kifungu cha 17(1) kinaeleza vizuri "Tume kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma itaanzisha kurugenzi za afisi kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake." Kwa hivyo hata hilo jambo unalolizungumzia tunaweza tukalizungumzia tutakapofika kwenye eneo hili la 17 utapata kidogo kulizungumza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sijamfahamu vizuri Mhe. Waziri kwa sababu hapa tulipokuwa tunajadili kifungu tunachoongeza mimi nilikuwa napingana nacho kuwepo vile, na marekebisho ninayotaka kuyafanya ili tukiondoka hapa tuondoke vizuri. Sasa akinipeleka kule maana yake kwamba nikubali hili ambalo limeongezwa hapa. Sasa ni vyema akatae hapa hichi ninachokisema mimi, aniahidi kwamba tutakapofika huko tutakiingiza kule. Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa nataka ahadi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, akizungumzia kifungu cha 4 kinazungumzia kwamba Tume itakuwa na majukumu yafuatayo, kwa hivyo zile kazi zake, majukumu ya kazi za Tume.

Kwa hiyo hapa huu sio muundo, tukifika kule Namba 17 tutazungumzia huo muundo alioushauri yeye, kama tukiona unafaa sawa, lakini kama tukiona haufai tukifika huko tutasema, lakini hapa ni vizuri tukakiachia hichi kifungu

kwa sababu kimejitosheleza sana, tukianza kuchomekea hivyo tunaweza kupata matatizo katika haya.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba unilinde sana kwa kitu ambacho ninachokisema, maelezo ya Naibu alipokuwa anajibu naomba nirejee kuyanukuu "Kwa ajili ya utekelezaji bora wa Tume na majukumu yake Tume itaandaa, maana yake tukikubali hapa kuwa Tume itaandaa hapa ndio itakuwa tumemalizana, hatuwezi kujadili muundo tena ndani ya Baraza hili. Sasa nasema hichi tukirekebishe kiwe wazi, tusubiriane huko anakonipeleka mimi ili nipate kuja kuchangia. Ukilipitisha hapa maana yake ndio tumemalizana, ndio shida yangu tu. Maana tukisema kwamba itaandaa Tume maana yake tena mimi nisinyanyuke tena kuja kutoa muundo. Muundo tukiutoa hapa huko mbele hichi kifungu kiwe kimekufa au tupo tayari kurudi nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate majibu na ahadi ya serikali kwa hichi ninachokisema, tukiruhusu kupitisha kifungu kilichoongezwa ina maana mimi kule kunako muundo nisiinuke tena, hili jukumu tutakuwa tumeshaiachia Tume, vyenginevyo kwa dharura hii tujadili huko kwenye muundo kama hatukukubaliana tuje hapa katika kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji kuna mawili kama Mhe. Waziri hajakubaliana na wewe kwa hilo ambalo unalitaka inanilazimu nipigishe kura kwa ambao wanakuafiki wewe, kwa wasiokuafiki, tutaendelea kwa sababu tunataka kuendelea hatuishii hapa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Sawa Mhe. Mwenyekiti, naomba unilinde sana. Ninachosema kifungu hichi mantiki yake tukikipitisha hapa ina maana tayari huo muundo aliyoniahidi Mhe. Waziri siwezi kuujadili tena. Maana vyenginevyo tuandae muundo ili kifungu hichi kiondoke ndio mantiki yangu mimi. Sasa akiniahidi twende mbele halafu tuje tujadili kama alivyoniahidi mapema itakuwa kiti chako hakinilindi. Vyenginevyo hichi tukiacha kukijadili tuje tukijadili kwa dharura yake tujadili huko mbele halafu tupitishe hichi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Miraji Khamis na nimefahamu majibu ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameyatoa.

Anachozungumza Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba utakapoanza Sura ya Tatu ndio unaingia kwenye Afisi ya Tume ya Uchaguzi na unapoingia kwenye Sura za Afisi ya Tume ya Uchaguzi kule ndio kutakuwa

na muundo wa hiyo Afisi iweje, kuna Mkurugenzi, kuna nani, na kuna kifungu cha 17 kimeshaeleza utaratibu wa hizo Kurugenzi zitakavyokuwa.

Sura ya Pili kinaanzisha Tume ya Uchaguzi pamoja na majukumu yake ya uchaguzi. Sasa utakapofika kwenye kuanzisha ile Afisi ya Tume ya Uchaguzi ndio tuzungumzie hiyo miundo ambayo Mhe. Miraji ambayo anaitaka, tutakapoitia hapa haitokuwa nafasi yake, ndio jawabu ambalo amekuwa akilitoa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji umeshasimama zaidi ya mara tatu, hatuwezi kujenga hoja na ukajenga tena hoja, tukubaliane hapo, tukubaliane kwamba tunaendelea na hilo ambalo unalitaka wewe tutalizungumzia kwenye muundo na sio kwenye majukumu ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuyataka hayo ambayo unanilazimisha nielekee, nilipo mimi, sisi tupo kwenye Muundo wa Tume ya Utumishi sio Muundo wa Tume kama ambapo Mwanasheria Mkuu ananipeleka. Muundo wa Tume upo kule, mimi sina tatizo nao. Muundo wa Utumishi ndio tunajadili kifungu ambacho kaongeza Naibu Waziri, tukubaliane hivyo tu, kama mnakotaka kunipeleka nyinyi ndio *wrong* zaidi kuliko nilipo mimi, maana kule kuna muundo wa Tume, hapa kuna muundo wa Tume ya Utumishi ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, lizingatie sana hilo, mimi sina nia mbaya lakini ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza namuomba tu Mhe. Miraji ulisome vizuri hili jalada kwa maana ya kwamba gazeti ili tuweze kufahamu mantiki ya kile ambacho kilichokusudiwa. Ukisoma Sura ya Pili kuna vitu vitatu ambavyo vimeshughulikiwa katika Mswada huu ni

- Kwanza kilichozungumziwa ni kuanzishwa kwa Tume yenyewe ya Uchaguzi, ambapo ukisoma kuanzishwa kwake maana yake kifungu cha 3 kinazungumzia kwamba masharti ya kuanzishwa kime- *refer* na Katiba.

- Pili ni majukumu ya Tume, majukumu ya Tume maana yake ni yale yanayokwenda kutekelezwa, ndiyo hapa katika *marginal note* imeandikwa Kazi za Tume.

- Uwezo wa Tume ambapo ukisoma kuanzia kifungu cha 7 kinaeleza ule uwezo wenyewe wa Tume yale ambayo itakuwa na mamlaka ya kuyafanya.

Sasa unapozungumzia suala la Tume ya Utumishi katika sura hii maana yake hii Sura nzima tu-*reframe* upya kitu ambacho hakipo. Msingi wa Sura hii ni kuanzishwa kwake, majukumu yake na uwezo wa Tume. Sasa katika mfumo wa Utumishi maana yake ni lazima tutafute Sura nyengine ambayo itaweza ku-*refer* hicho ambacho tunakitaka, hicho ambacho anakisema. Ukiingiza hapa maana yake hichi chote sura nzima hii unaibadilisha yale maudhui yake.

Maudhui ya hapa ni kuanzishwa kwa Tume ambapo imeanzishwa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba. Majukumu yake ndio hizi kazi ambazo zimeelezwa. Lakini na uwezo wake wa Tume kipi ambacho kitakuwa na uwezo wa kufanya, kukodisha jengo, kuendesha kura na hayo ndiyo yameelezwa hapa. Sasa katika kifungu hichi, Sura hii ukiingiza suala la Utumishi wa Tume utakuwa unaingiza sio sehemu stahiki.

Nadhani maelezo ambayo yametolewa na Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba tutakapofika katika kifungu cha 17 anayo haki ya kusimamia hoja yake, ambapo kwa mujibu wa mapendekezo ya serikali jalada limeeleza wazi kwamba mapendekezo ya serikali Utumishi huu uendelee kubaki kama sehemu ya utumishi wa umma kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 ndiyo mapendekezo hayo. Sasa kuendelea kulazimisha kwamba tubadilishe sura, maudhui yote kwa sababu ya jambo moja ambalo haliendani na sura, sidhani kama ni sahihi Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 4	Kazi za Tume Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 5	Uwezo wa Tume Kusimamia Mikutano ya Kampeni Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 6	Uwezo wa Kutaka Habari Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 7	Uwezo wa Tume Kutumia Jengo au Eneo Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 8	Uwezo wa Kuanzisha Kamati za Ushauri
Kifungu 9	

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kifungu 9(5) Mhe. Mwenyekiti, "Mtu yeyote au taasisi yoyote itakayofanya uangalizi wa uchaguzi bila ya kibali cha Tume itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi milioni tano."

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia mimi nafikiri humu ndani kila mtu anajua *cost implication* ya uchaguzi. Sasa hapa tumeangalia faida ya pesa tumeacha kuangalia ule uchaguzi ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasema kwanza hapa kunako neno "kosa" liwe "kosa la jinai" halafu huyu mtu atozwe faini kama ilivyo lakini na kifungo, atakapofanya ukaguzi akatangaza *data* alizopata ametuchafulia uchaguzi mzima, tusimwachie mtu huyu kirahisi, uchaguzi ni kitu kikubwa katika nchi ya Zanzibar na nchi nyengine yoyote duniani. Kwa kumtoza pesa tu milioni tano, kuna watu humu wana pesa zaidi ya milioni tano, wapo tayari kufanya wanavyotaka ili kuharibu uchaguzi. Hapa lazima mtu atoe faini na aende ndani na kesi hiyo tuiweke iwe ni ya jinai. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mimi na ndugu yangu Mhe. Hassan tunazungumza lugha moja. Anayoyasema mimi nakubaliana nayo sana, atakayepotosha taarifa zetu, kuharibu uchaguzi wetu, umekuja hapa kama muangalizi kwa hivyo tumesema hivi licha ya faini tumeongeza na kifungo hapa. Tukasema kifungo hichi tutakiongeza ikaweko na adhabu ya kifungo na baadaye ukishatiwa hatiani tumesema kwa kipindi cha miaka 10 mtu huyo sasa hataweza tena kuja hapa kufanya shughuli za uangalizi. Hapo labda tutoe adhabu ya kifo, lakini haya yaliyopo yanatosha sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini Kiswahili nilichokisema hapa "Tume itakuwa ametenda kosa" Mimi nimesema "jinai" hapa imewekwa "kosa" hapa, ni maandishi tena ni sheria, tunaipitisha sisi Baraza la Wawakilishi, tunapoiacha hivi kosa hatuja-*criminalize* kuifanya jinai bado. Kwa hivyo mimi hoja yangu iwe kosa la jinai, halafu na kifungo lakini tukiiachia hivi itakuwa bado.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis, hiyo siyo hoja ambayo umekuja nayo mwanzo, hiyo nyengine sasa unayoizungumza. Hoja ya mwanzo umesema kuhusu kuweka na kifungo, hujasema kuhusu kosa la jinai.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Yote niliyasema Mhe. Mwenyekiti, na nafikiri watu wamenisikia wote. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ukishasema kifungo tayari kosa la jinai. Kwa sababu *civil case* haina kifungo, mkienda kushtakiana kwa madai, hapo ukishafungua jinai tayari umekwisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis, tunaendelea.

Kifungu 9	Uwezo wa Kuruhusu Waangalizi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 10	Uwezo wa Kutunga Kanuni na Miongozo Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 11	Kuanzishwa kwa Afisi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 12	Muhuri Pamoja na Nembo ya Ofisi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 13	Mkurugenzi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 14	Sifa za Mkurugenzi
Kifungu 15	Muda wa Utumishi wa Mkurugenzi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 16	Kazi za Mkurugeni Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 17	Kurugenzi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 18	

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba katika Kifungu cha 18 kinataja Sekretarieti. Katika kuchangia niliomba zile sifa za Wajumbe wale wa Sekretarieti tuziainishe kama ambavyo tumeziainisha za Mkurugenzi ndani ya Mswada huu. Lakini majibu ya Waziri yakaja kwamba sifa zile zitakuja kuainishwa kunako Kanuni zao, kitu ambacho kinaanza kutoa mashaka, kwa nini Mkurugenzi Mkuu kaainishwa hapa, sekretarieti na kurugenzi zikaainishwe kwengine. Sasa nilikuwa nataka sifa zile kama ambavyo tulipendekeza katika kuchangia basi zitajwe za sekretarieti kwa wale watakaoingia ndani ya sekretarieti lazima waanze na *level* ya *degree*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti hizi kwa kuwa hizi sifa tayari hawa wanakuwa nazo na wao watu wa Tume kuwategemea na ile kurugenzi yenyewe, wao ndio wanajua sifa na sifa gani ya kuchukua mtumishi wa umma akaja hapa akafanya kazi pale. Kwa hivyo sifa zitakuwa zimo *within* hawawezi tu kwamba wewe utaletwa hapa hutimii sifa, kwa sababu kila kurugenzi itakayopendekezwa itajulikana mahitaji yake atajulikana mtu wa sifa gani anakuja hapo anapewa hiyo kazi kutokana na sifa hiyo ambayo anayo. Haji tu hivi hivi, sasa utakwenda kumchukua mpiga makoongo huko umlete haiwezekani, atakuwa yule mwenye sifa ya kurugenzi hiyo kwa mujibu wa mahitaji ya Tume ndio atakuwepo hapo kwa sababu huwezi kumuwekea kwa sababu atategemea kurugenzi gani hiyo, sifa gani ipi inaanzishwa lazima tuendane na vile vigezo vinavyokubalika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe.Mwenyekiti, sisi tunajadili afya na katika huo utumishi wametuainishia mkurugenzi sasa kurugenzi nyengine sifa zake zikae pembeni, kurugenzi moja sifa zake zije humu. Yaani katika utaratibu wa kawaida hatuwezi kwenda hivyo na nimuombe tu Mhe. Waziri kifungu hiki mimi nikiachie sheria gani iliyozipa mamlaka kurugenzi hizi na sifa zipi ambazo zipo kwa sasa zinazotumika kwa hizi sekretarieti au kurugenzi nyengine ambazo nazitaka tuziainishe leo ili kuboresha utendaji wa Tume, maana tumepata vitu vingi sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe anajenga hoja kwenye kifungu cha 18 na hoja yake ni kwamba kwa nini sifa za kurugenzi zisitajwe hapa. Lakini angeanza kusoma vizuri na kwa busara kwenye kifungu cha 16 na 17 angepata maudhui mazuri zaidi ya kumsaidia kumuongoza kwa namna gani ambavo mswada haukuainisha hizi sifa. Naomba tu nijaribu kunukuu Mhe. Mwenyekiti, kusoma sura ya 17 amezungumziwa mkurugenzi, ambaye yeye katika utendaji kazi wake atakuwa na nafasi ya kutafuta wasaidizi. Sasa wasaidizi wametajwa katika kifungu cha 18, kurugenzi hizi maana yake zilizokuwepo hapa ni katika utendaji kazi kwa mujibu wa mazingira yatavyokuwa, mkurugenzi atapendekeza kwa Tume, Tume kwa kuzingatia mazingatio ya muda ulipo na mahitaji yao ndio atamteua huyo mkurugenzi.

Sasa mkurugenzi kwa mfano ukisema leo awe na master ya MBA lakini kwa wakati huo au kwa mahitaji yao, Tume haioni kama humu kuna umuhimu kuwa na mkurugenzi huyo maana yake mkugenzi utakuwa umepoteza sifa. Lakini mahitaji ndio yatakayomuongoza mkurugenzi kupeleka mapendekezo yake kwa Tume ili Tume iweze kufanya uteuzi. Kifungu ambacho kinaongoza utaratibu huo ni sheria mama, sheria nambari 2 ya mwaka 2011 Sheria ya Utumishi ya Umma ndio inayotoa muongozo wote wa namna gani ya kuteua sifa na mambo yote yanayohitajika katika watendaji wa Serikali katika nafasi za uteuzi na utendaji mzuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Ni mara ya mwisho nasema ushasimama mara tatu hiyo ndio mara ya mwisho.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ya mwisho sawa lakini wakati nitapata kusema itakuwa ishanitosha.

Mhe. Mwenyekiti, naridhika sana na maelezo ya Mhe. Waziri Issa Gavu kwa kunipeleka kwenye hivyo vifungu ambavyo vinatoa wajibu wa mkurugenzi kuanzisha kurugenzi lakini hajaambiwa aanzishe na sifa za hizo kurugenzi

wenyewe akanipeleka kwenye kunako Sheria ya Utumishi wa Umma na ndio pale nilipokuwa nasema nyuma huko katika kudai ile *autonomy* ya Tume kwa mujibu wa Katiba tuliyoiweka ndio tukatafuta ule muundo. Sasa leo hii kama zile sifa tutakapowapa Tume yao ya Utumishi au muundo wao wa Utumishi kwa maana watazingatia vile vigezo lakini kulikuwa kuna haja na hapa kuwepo kwa zile sifa ambazo tukishaanzisha hicho chombo chenyewe ambacho tumewapa mamlaka basi tuwape na sifa zao au tuandike tu atafuatana na sifa zile za utumishi wa umma. Maana yake tayari tushabariki sisi kuanzisha kwa muundo na ile Tume ndogo ya Utumishi ndani ya Tume hii ya Uchaguzi. Nilikuwa nataka maelezo ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji umeambiwa mara mbili ninafikiri kila aliyesimama hapa amezungumzia kifungu namba 17 hebu kisome vizuri kifungu namba 17 kinavyoeleza:

"Tume kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma itaanzisha kurugenzi na afisi kama inavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, inatosha hiyo kabisa kutoa maelezo kwamba sekretarieti itakuwa na muundo gani na sifa gani.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina haja ya kupingana lakini kama nimesoma shule ya Kinyasini na ninakawia kufahamu, Tume itazingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, itaanzisha kurugenzi maana yake ni mamlaka ya kuanzisha kurugenzi, mamlaka ile ya utumishi haijazunguzwa hapa lakini tuendeleeni watakuja kuona wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ameuliza hapa Mhe. Mwenyekiti, kwamba sheria gani ambayo inatuongoza, tumemjibu kwamba sheria nambari 2 ya mwaka 2011, Sheria Utumishi wa Umma ndio inayotuongoza na ile sheria imeeleza vizuri, unapozungumzia maafisa waandamizi kwa maana kwamba kurugenzi na wengineo wameelezwa humu watu angalau wenye shahada ya kwanza, wawe watu angalau wenye uzoefu usiopungua miaka 10 na mengineyo. Sasa tumeona hakuna haja ya kuyarejea yote wakati sheria ile mama inaongoza Utumishi wa Umma imeshatoa muongozo ni haja tu ya kukaa. Kwa hivyo ndio maana alipotaka sheria tukamtajia na kwa bahati mbaya hakuwahi ku-*refer* yeye mwenyewe.

Kifungu 18	Sekretarieti
Kifungu 19	Kuanzishwa kwa Afisi ya Uchaguzi za Wilaya pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 20 Kazi za Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 21 Watumishi wengine
Kifungu 22 Uhamisho wa wafanyakazi wa Tume

Sehemu ya Nne

Masharti ya Fedha

Kifungu 23 Bajeti
Kifungu 24 Fedha za Tume pamoja na marekebisho yake
Kifungu 25 Afisa Mhasibu
Kifungu 26 Hesabu na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27 Ripoti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 28 Fidia ya Ajali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 29 Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 30 Kinga kwa maafisa wa Tume pamoja na marekebisho yake
Kifungu 31 Kutoa Taarifa za Afisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32 Malipo ya Wajumbe na Maafisa wa Tume pamoja na marekebisho yake
Kifungu 33 Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 34 Kufuta na kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ametoa hoja wale ambao wanakubaliana na hoja wanyooshe mikono, wale wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ya mwaka 2016 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi niwapongeze sana kwa kuupitisha mswada huu, sote tunaelewa vizuri sana, lengo kuu lilikuwa ni nini lakini hata hivyo mswada huu namna gani utavyoweza kusaidia katika chaguzi zetu nyengine zijazo.

Waheshimiwa Wajumbe, muda tulionao sasa hivi tumebakiza kama nusu saa, kwa hivyo ninafikiria kwamba tunaweza kuahirisha sasa hivi mpaka jioni saa 11 kwa ajili ya shughuli zitakazo kuja hapo jioni. Waheshimiwa Wajumbe ninaahirisha mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.30 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Mwenyekiti(Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwanza nichukue fursa hii kwa kuniruhusu kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo ya Taifa Nam. 1 ya mwaka 1985, na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya mwaka 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

Madhumuni

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, madhumuni ya mswada huu ni kufuta Sheria ya Nembo ya Taifa Nam. 1 ya mwaka 1985, na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya mwaka 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ili iendane na mahitaji na mazingira ya sasa na ya baadae.

Aidha, kutokana na kutokuwepo kwa sheria inayosimamia wimbo wa taifa wa Zanzibar, mswada huu pia unaweka nafasi ya kuingiza suala la wimbo wa taifa wa Zanzibar na wimbo maalumu wa mashujaa wa Zanzibar katika sheria inayosimamia alama za Taifa.

Historia

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, Sheria ya Nembo Nam. 1 ya mwaka 1985 inayotumika sasa ilianza kutumika mwaka 1985 baada ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuidhinishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na usimamizi wako uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha, baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 hadi mwishoni mwa mwaka 2004, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa

ikitumia Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa matumizi mbali mbali ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona umuhimu wa kuwa na bendera yake yenyewe, ilitunga sheria ya bendera Nam. 12 ya mwaka 2004 ambayo ilianza kutumika mwaka huo huo baada ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuidhinishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tangu ilipoanzishwa mwaka 2004 hadi hivi sasa sheria hiyo inasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar unatumika bila ya kuwa na muongozo wa kisheria unaoelekeza namna bora na sahihi ya matumizi yake, na hivyo kukosa sehemu mahsusi ya kufanya rejea iwapo kutatokea tatizo.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, baada ya serikali kufanya mapitio ya sheria za nchi mbali mbali yenye mazingira yanayofanana na ya kwetu kama vile Seychelles imebainika kwamba utambulisho wa alama za nchi ikiwa ni pamoja na Bendera ya Nchi, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa umeanzishwa na kusimamiwa na sheria moja.

Umuhimu wa Mswada huu wa Sheria

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na kasoro zilizobainika katika muonekano na matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa, imeonekana kuna haja na umuhimu mkubwa wa kuwepo sheria itakayoainisha utaratibu wa muonekano na matumizi sahihi ya alama hizo za Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa kasoro hizo ni kama ifuatavyo:

a. Kuwepo kwa sheria mbili tofauti zinazosimamia alama muhimu za Taifa na kusimamiwa na mamlaka tofauti.

b. Kuwepo kwa Wimbo wa Taifa ambao hauna maelekezo ya kisheria yanayoulinda katika hali zote.

c. Kutokuwepo kwa maelekezo ya kisheria juu ya mchanganyo wa rangi za bendera na nembo ambako kunapelekea kuwepo kwa Bendera na Nembo ya Serikali zenye mchanganyo tofauti wa rangi.

d. Kutokuwepo kwa maelekezo ya kisheria juu ya matumizi sahihi ya Bendera, Nembo na Wimbo wa Taifa.

e. Kutokuwepo na mfumo wa kisheria wa makosa na adhabu yanayosimamia utekelezaji wa Sheria ya Bendera na Sheria ya Nembo ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, mswada huu wa sheria pia ni muhimu kwa kuwa umeweka utaratibu mzuri zaidi wa kisheria wa kutengeneza na kutumia kwa usahihi Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

Sehemu Kuu za Mswada huu

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, mswada huu umegawika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo:-

i. Sehemu ya Kwanza, ambayo inahusika na utambulisho wa jina fupi la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika katika Mswada huu wa Sheria.

ii. Sehemu ya Pili, ambayo inaelezea Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar pamoja na matumizi yanayofaa na matumizi haramu ya alama hizo za nchi. Aidha, sehemu hii inaelezea uwezo wa waziri wa kutunga kanuni, kusamehe na kutoa adhabu.

iii. Sehemu ya Tatu, inayoelezea makosa, adhabu, kufuta na misamaha juu ya matumizi mabaya ya sheria hii.

Masuala Muhimu Yaliyozingatiwa

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, ili kuwa na sheria itakayokidhi mahitaji ya nchi yetu katika utengenezaji na matumizi ya alama hizi muhimu kwa Taifa, mambo mbalimbali yamezingatiwa ikiwemo:

a) Kuwepo kwa sheria moja inayosimamia alama za Taifa (Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar).

b) Kuwepo kwa vifungu vya sheria vinavyoelekeza matumizi sahihi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

c) Kuwepo uwezo wa waziri anayehusika na kutunga Kanuni zitakazosimamia alama hizi za Taifa.

d) Kuwepo vifungu vya makosa na adhabu kwa watakaokwenda kinyume na sheria inayopendekezwa kuanzishwa.

e) Kuwepo kwa jadweli/viambatanisho katika sheria vinavyofafanua muundo na vipimo sahihi vya Bendera ya Zanzibar na ala (*note*) za Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalum wa Mashujaa wa Zanzibar.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liujadili Mswada wa Kufuta Sheria ya Nembo ya Taifa Nam. 1 ya Mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na kushauri ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurudia kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Simai Mohammed Said (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wetu napenda kutoa hotuba hii ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya mwaka 1985, Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar ya mwaka 2016 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutujaalia sote uzima na afya njema na tukamudu

kukutana tena leo, kwa lengo la kuendelea kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wetu.

Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya 2004, na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar ya 2016 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kutupa katika kutelekeleza majukumu yetu. Hakika mashirikiano yao yamekuwa ni chachu ya ufanisi katika kukamilisha kazi hii uliyotuagiza ya kuchambua na kuupitia mswada huu muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu na watu wake. Sambamba na hilo naomba niwashukuru na kuwapongeza wadau mbali mbali waliojitokeza kuungana nasi katika kuupitia na kutoa maoni yao kwa lengo la kuufanya mswada huu uwe bora zaidi, hakika fikra na mawazo yao yametusaidia sana kupata uelewa na hatimaye kuweza kufikia lengo letu.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki hata kidogo iwapo nitamaliza hotuba hii bila kutoa shukurani kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa umoja na bidii zao katika kazi zetu, jambo linalopelekea kutekeleza kazi zetu vizuri sana na hatimaye mswada huu kuuchambua ipasavyo. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe
5.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
6.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
7.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
8.	Ndg. KassimTafana Kassim	Katibu
9.	Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo sasa naomba nijielekeze katika mswada moja kwa moja.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar ya 2016 na mambo mengine yanayohusiana na hayo, una lengo la kufuta Sheria ya Nembo ya Taifa Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam. 12 ya 2004 na kutunga sheria mpya itakayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na wimbo wa Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inakubaliana na madhumuni ya kuletwa kwa mswada huu kwani uwepo wa sheria hii ambayo itakusanya vitu vyote katika sheria moja itakuwa wepesi katika utekelezaji wake. Aidha, uwepo wa sheria hii utatambua uwepo wa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ambapo hapo awali haukua na sheria maalumu iliyokuwa inausimamia, sambamba na wimbo huo wa Taifa. Kamati inakubaliana na kutambuliwa kwa wimbo maalumu wa mashujaa wa Zanzibar ambao pia ni kielelezo cha uhuru na uzalendo kwa Zanzibar uliotokana na mashujaa kupoteza roho zao kwa ajili ya kuikomboa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapendekeza kwamba licha ya wimbo wa Taifa wa Zanzibar na wimbo maalumu wa mashujaa kuwemo katika sheria hii, ni vyema serikali kupitia Wizara ya Elimu kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa nyimbo hizo muhimu kwa Taifa zinatumika katika skuli zote za Zanzibar, kwani inaonekana wanafunzi na kizazi cha sasa kwa ujumla hawana uelewa mzuri juu ya wimbo wa taifa ambao ni historia kwao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupitia kwa makini mswada huu, Kamati imependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuufanya uwe bora zaidi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni pamoja na kifungu cha 2 ambapo katika tafsiri ya maneno “Bendera ya Zanzibar” maneno “Taifa ya Serikali ya Mapinduzi ya” yaliopo baina ya neno “ya” na neno “Zanzibar” yanafutwa. Sababu ya kupendekeza marekebisho haya ni kwamba Bendera ya Zanzibar kwa ujumla wake ni kielelezo cha nchi na sio serikali kama inavyosomeka katika mswada huu.

Aidha, Kamati imependekeza kifungu kipya cha 6 kitakachosomeka 6(1), kutakuwa na wimbo maalum wa ukombozi na kuwaenzi mashujaa wa Zanzibar ambao maneno yake ni kama yanavyoonekana katika jadweli la nne la sheria. Sababu ya marekebisho hayo ni kuutambua wimbo wa mashujaa katika sheria hii pamoja na kuuwekea utaratibu wake katika Jadweli la IV.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo mengine yaliyofanywa na kamati katika jadweli Nam. 1 ambapo kamati imependekeza kufutwa kwa viashiria vya rangi za bendera, na badala yake viashiria hivyo viwekwe kwenye Kanuni. Sambamba na hilo, katika jadweli la II yanaongezwa maneno "rangi za nembo ya Serikali ya Zanzibar zitashabihiana na rangi za Bendera ya Zanzibar" mwisho wa maelezo ya nembo hiyo.

Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba ijapokuwa rangi halisi za Nembo ya Serikali hazijatajwa katika Jadweli hili basi ni vyema japo zikatajwa kuwa zitakuwa ni zile zile zilizomo katika Bendera ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika jadweli la III Kamati iliona upo umuhimu wa kuwepo na viashiria vya ala za sauti ya muziki wa wimbo wa Taifa (*notation*) ambapo kamati imependekeza ala hizo ziwepo katika Kanuni ili kuepusha uwezekano wa watu kuja kuupiga wimbo huo vile wanavyotaka wao, bali wafuate utaratibu huo utakaowekwa na Kanuni.

Kwa upande wa adhabu zilizowekwa kwa ajili ya makosa yanayohusiana na kuikashifu bendera, kamati imekubaliana na kuwepo kwa vifungu vinavyoonesha adhabu kwani hapo kabla hakukuwa na vifungu vya kisheria ambavyo vitawatia hatiani wenye kufanya makosa ya kuikashifu bendera. Mfano kwa kuichana, kuichoma moto na kadhalika, lakini kwa sheria hii sasa mtu yeyote akitenda makosa yanayohusiana na hayo ataingia makosani kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na mapendekezo hayo kamati pia imefanya marekebisho ya uchapaji kwa baadhi ya vifungu ambayo yameoneshwa katika waraka wa mapendekezo ya marekebisho ya kamati ambayo naamini kila Mjumbe tayari amepata nakala yake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Aidha kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini. Hivyo, nawaomba wauchangie mswada huu, washauri, na wakosoe na hatimae waupitishe mswada huu muhimu kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naunga mkono mswada huu na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako sasa napenda niwe mjumbe wa kwanza kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, na mimi nikupongezeni kwa hotuba yenu na sasa nimekuruhusu uwe mtu wa kwanza kuchangia mswada huu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nianze kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambapo mimi nikiwa kama mtetezi wao ndani ya Baraza hili la Wawakilishi na pia kuwa sauti yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kwanza nachukua nafasi hii kuipongeza serikali kuja na mswada huu. Niipongeze pia wizara husika na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuja kuleta mswada huu kwa haraka kwani mswada huu kwa kweli umekuwa ni jambo muhimu sana, na naamini hata wananchi wa visiwa vyetu wamekuwa na shauku kubwa kuweza kujua mambo mengi ambayo yanatokana na mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi sitakuwa na mengi lakini ningependa kuzungumzia katika kifungu cha 7 ambacho kinazungumza ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki Nam. 7 kwa kweli kisheria kipo sawa sawa, lakini bado kifungu hiki Nam.7 kinahitaji maelezo ambapo Mhe. Waziri wakati atakapokuja kutunga hizo Kanuni basi ieleweke. Kwa sababu lengo la mswada huu ni kuibua pia hamasa kwa wananchi ili kuleta uzalendo, kutambua utaifa wao na nchi yao, kuipenda nchi yao na kuleta umoja na mshikamano kwa wananchi wote Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Wazanzibari mara nyingi hupenda kukusanyika, wakati mwengine tumeona kama wakati wa shughuli mbali mbali za serikali lakini pia shughuli za kitaifa, wanaweza wakatokea kwa pamoja wakaamua kutumia bendera yetu kutengeneza fulana, kutengeneza bendera zao ndogo ndogo kwa pesa zao wenyewe. Lakini inawezekana katika michango watakayopeana moja kwa moja wakaingiwa na hofu wakati wana kusudio la kujenga umoja wao na kutimiza majukumu yao. Pia kuonesha jinsi ujasiri wao waliokuwanao jinsi wanavyoipenda nchi yao. Haya yanaweza yakatokana na kutokufahamu tu, unapokisoma hiki kifungu Nam. 7(a) ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia

bendera ya Zanzibar kama (a) inavyosema, kuwa kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kinachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona sasa hivi huko mitaani wanatengeneza fulana na jezi za Zanzibar, wananunua watu mbali mbali na hizi kwa kweli pia zimekuwa zinapendwa hata na wageni ambao wanakuja hapa Zanzibar, sio watalii hata ndugu zetu wanaotoka Tanzania Bara wananunua jezi hizi. Hivi sasa utakuta kuna jezi za watoto wadogo zenye alama ya bendera ya Zanzibar pamoja na jina lenyewe la Zanzibar.

Sasa kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri anapokuja kufanya majumuisho mambo madogo madogo kama haya ayatolee ufafanuzi vizuri ili waandishi wa habari waweze kuyafahamu. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kufahamu ni makosa yepi ambayo mtu hawezi kutumia ikiwa ni *trademark*, ikiwa kuweka alama ya bendera nje ya bango lako la kibiashara au endapo unaamua kutengeneza fulana huko China au Dar es Salaam, au uende kwa *printer* mwengine kutengeneza bendera ya Zanzibar kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ile bendera inazidi kutambulika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu ni wazalendo. Mimi niseme kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote hapa kama wakiwa na pesa zao za kutosha mfukoni basi watakuwa tayari kutengeneza fulana za bendera ya Zanzibar kuwapa wananchi wao. Lakini inawezekana pia ikaleta sintofahamu kwa wananchi pamoja na sisi kwa ujumla.

Kwa hivyo, mimi naomba kwa sababu michango yangu mingi nimetoa katika kamati na jengine bado nilipozungumza kwenye suala hili nilitolea hofu na nikamwambia Mhe. Waziri, pamoja na Wajumbe kwamba katika hili bado mimi nataka nipate taarifa kamili. Basi nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa mapana kabisa ili Wazanzibari wamsikie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni na niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mawaziri wote kwa kutega masikio yao na kunisikiliza kwa makini hususan Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunijaalia nafasi hii nami nichangie katika Mswada ulio mbele yetu unaohusu masuala muhimu ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu mimi naanzia na nambari 7, hapa ndipo nilipoangalia sana. Mswada huu unaposema kwamba," ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali au Wimbo wa Taifa". Mimi nipo zaidi hapa penye bendera ukiambatana na hiki kifungu (a) na (b), "kwamba endapo kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kitachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza".

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aangalie sana katika kifungu hiki au aje atupe ufafanuzi zaidi pale ambapo kuna bidhaa, mfano hapa Zanzibar tumezalisha kwa kutumia rasilimali zetu na leo tunazipeleka nje. Kwa hivyo, bidhaa ile kama ni kampuni ikaamua kuweka sehemu ya matangazo yake pale kuweka alama ya bendera ya Zanzibar kujua kwamba bidhaa hii inatokea Zanzibar, hivyo kama hili tunasema kwamba itakuwa ni makosa basi tuliangalie tena upya au Waziri atakapokuja atoe ufafanuzi jinsi ya matumizi ya alama kama hiyo. Kwa vile itatuepusha kuona kwamba nchi yetu na sisi tunaitangaza kama vile ambavyo leo Mzanzibari akifika nchi yoyote ile hata hapo Tanzania Bara kwa lugha yake tu anajulikana huyu ni Mzanzibari. Kwa hivyo, bidhaa ile ambayo tunatoa hapa tukaipeleka huko tukaweka bendera yetu pale pembeni kama nchi nyengine ambazo wanafanya, basi naona ni utambulisho pamoja na kutambulisha bidhaa kwa alama ile, lakini pia tunaitambulisha nchi yetu kwamba Zanzibar nayo imefikia hatua hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 7(b) "kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza, kuzalisha inayouzwa au inayotolewa kwa ajili ya mauzo". Halikadhalika kwa mfano, sisi ni wazalishaji wazuri wa karafuu tena yenye ubora, kwa hivyo sijui itakuwa vipi kama tunaambatanisha katika *package* ya karafuu na baadae katika chombo kile tukaweka alama hii kwamba hii ni karafuu inatoka Zanzibar. Kwa sababu bendera hii sio ya nchi nyengine ni ya Zanzibar. Je, itakapofika kufanya hivyo ikawa mtu huyo atakuwa ndani ya makosa namuomba Mhe. Waziri aje atueleze pindi ikitokezea hivyo ataweza kufanya nini?

Katika kifungu hicho hicho cha 7(c) naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja mimi na wenzangu Waheshimiwa Wajumbe tupate maelezo katika kifungu hicho anaposema kwamba ni kinyume na madhumuni yaliyoidhinishwa na waziri, kwamba, "kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza au kuzalisha kwa mtu kufanya hivyo kinyume na madhumuni yaliyoidhinishwa na Waziri". Hapa naomba ufafanuzi zaidi, Mhe. Waziri atakapokuja tupate ufafanuzi.

Vile vile niendelee katika kuchangia kifungu nambari 8 cha Mswada huu kinachosema, "Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni ya masharti ya sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, leo nchi yetu ina umoja wa kitaifa lakini hatujui baadae itakuwa vipi na Rais au Waziri atakayekuwepo katika madaraka hayo aliyopewa atakuwa na mwelekeo gani, anaweza akatumia madaraka yake haya akaweza hata kubadilisha baadhi ya mambo ambayo amepewa kisheria. Kwa hivyo, naona madaraka ni makubwa katika nafasi hii kuachiwa Waziri peke yake ni vyema na hapa tupaangalie vizuri tuone kwamba aweze kushauriana na wenzake kwanza ndio baadae yatoke maamuzi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kifungu nambari 9. Vile vile hapa kwa mtazamo wangu naona pia Waziri mamlaka aliyopewa ni makubwa, ni bora jambo hili asiliamue yeye apeleke Mahakamani kwenye maamuzi ya mwisho badala ya kuamua hivyo. Sababu ya kusema hivyo, Waziri anaweza kama ninavyosema akawa pengine ni mtu wa chama chake na akaona kwamba hawezi kumuadhibu kwa hiyo akaitumia fursa hii kuwa yeye ndiye muamuzi wa mwisho. Ni vyema suala hili likapelekwa Mahakamani kwa muono wangu mimi.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni machache ambayo niliona kwa sasa niyachangie na mimi nashukuru sana na wenzangu niwaachie na wao waendelee kuchangia kwa Mswada huu ambao ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Ahsante Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Welezo kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu muhimu ulioletwa na serikali wa Nembo, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Ukombozi.

Mhe. Mwenyekiti, leo nimefurahi sana kuona serikali kutambua *symbol* zake kwamba tuweze kuzifahamu kisheria kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuliko yote lililonifurahisha zaidi leo kwamba tunatunga sheria muhimu ya wimbo wa ukombozi, wimbo ambao wana Mapinduzi uliowakomboa wakwezi na wakulima, wimbo wa Sisi Sote. Watoto wote waliozaliwa miaka ya 1990 wamekuwa hawaujui wimbo wa ukombozi ati kwa sababu tunaambiwa vyama vingi vya siasa. Sasa unajiuliza swali, hivyo vyama vingi vya siasa kweli vimekuja kutuondoshea historia yetu ya Mapinduzi

ambayo tumejikomboa na kuleta demokrasia ya mtu mweusi kwa Zanzibar? Mapinduzi yaliyoondosha unyonyaji na udhalili wa hali yote ile.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua fursa hii kuunga mkono maelekezo ya Kamati kwamba lazima katika sheria hii uwemo na wimbo wa ukombozi, wimbo wa "Sisi Sote Tumegomboka".

Mhe. Mwenyekiti, kuuweka wimbo wa sisi sote katika sheria hii ni kuwafanya na kuwaambia vizazi vijavyo nini maana ya Zanzibar. Zanzibar imetoka wapi, iko wapi na inakwenda wapi. Hakuna asiyejua dunia nzima kwamba Zanzibar ni nchi iliyopatikana Kimapinduzi na sio nchi iliyopatikana kwa bendera shusha, bendera pachika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia. Ukienda katika nembo ya Serikali na wimbo wa Taifa wa Zanzibar. Nembo ya Serikali itakuwa inachukua kwamba ni nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama inavyojieleza katika Jedwali ya 2.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukienda kipengele cha 7 kinasema, "Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo:"

Kwanza ningependekeza itiwe na neno 'wimbo wa ukombozi', iwe 'Bendera ya Taifa na Nembo na Wimbo wa Ukombozi' uwekwe kabisa. Lakini pia tukiangalie kifungu nambari 7(f).

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho tumekiwekea bendera ni marufuku. Mimi kwa mfano nina kampuni nazalisha maji, maji yangu nimetaka kutia jina la nembo ya kampuni lakini pia kwa sababu ya utamu wa yale maji yanayotoka Zanzibar nikawa nahisi niweke na bendera ya Zanzibar, sio nembo ya serikali bali ni bendera ya Zanzibar. Mimi sioni tatizo Mhe. Mwenyekiti, kuitumia bendera ya Zanzibar katika bidhaa inayotoka Zanzibar. Nchi nyingi duniani kama Sweden, Marekani na Canada katika bidhaa zao walizonazo wao tu wanazitumia bendera zao za taifa kwa sababu ku-*symbolified* kwamba bidhaa hii inatoka Canada, bidhaa hii inatoka Marekani.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mwengine dunia nzima karafuu nzuri na bora tunazo sisi Zanzibar, sasa kama kwenye mafuta yetu ya karafuu tutaamua kuweka bendera ya Zanzibar kweli iwe kosa? Jambo hili naomba tulitizame tena tusiweze kuchanganya baina ya Nembo ya Serikali na Bendera, kuichanganya bendera ni kosa.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu (f) kinasema, "Kama mapambo au mambo ya sanaa". Kwa mfano, Mhe. Abadalla Maulid Diwani anataka kuowa Mzungu, Mzungu haijui bendera ya taifa ya Zanzibar kaamua katika harusi yake kupamba kuweka bendera tupu za Zanzibar kuiambia jamii, kuiambia dunia mimi ni Abdalla Diwani kutoka Zanzibar na *symbol* yangu hii kuna tatizo Mhe. Mwenyekiti? Kwa maana hiyo, hili tuliangalie katika kupiga marufuku, tusipige kila kitu marufuku bendera ni *symbol* ya taifa. Kwa hivyo, bendera sio nembo bendera ni kielelezo kwamba mimi ni nani na ninatoka wapi na hii ndio *symbol* yangu. Najua kuitumia nembo ni marufuku lakini si kutumia bendera na bendera tumekuwa tunaitumia katika mapambo ya serikali, mapambo yetu binafsi ya shughuli ambapo pengine tunatumia bendera kwa sababu ndio *symbol* yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napendekeza neno marufuku likae katika namba 4(2), nembo ya serikali itakuwa ni kuchukuliwa hapa ndio hilo neno 'marufuku', lakini katika nambari 7 bendera neno 'marufuku' liondoke tusipige marufuku kwa kuitumia bendera kwa kila mambo, lazima tuiangalie tena.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora kwa madhumuni ya masharti ya sheria hii. Mheshimiwa ukweli usiofichika Katiba ya Zanzibar inaruhusu kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa unapomuachia Waziri atunge kanuni Mwenyezi Mungu apishie mbali, tumepata wizara kapewa Waziri ni Hizbu, waziri ambaye hayatambui Mapinduzi, sasa leo unamuachia Waziri huyo kutunga kanuni ambazo zitam-*favour* kwa mtizamo wake na itikadi yake.

Mhe. Mwenyekiti, tusimuachie Waziri Katiba ya Zanzibar iko *very clear* inaruhusu Serikali ya Mseto, leo *Alhamdulillah* tunae Waziri Mhe. Juma Ali Khatib, yeye ni Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum lakini anayatambua Mapinduzi, tunae Mhe. Said Soud Said naye ni Waziri lakini anayatambua Mapinduzi na anayathamini na kujua kwamba ndiyo yaliyomuokoa Mzanzibari. Lakini tunaweza tukawa na Wizara ya Waziri Hizbu hayatambui Mapinduzi. Tumeyaona tulikotoka, unamuachia kutunga Kanuni ya bendera, kutunga Kanuni ya nembo Mhe. Mwenyekiti, hili haliyumkiniki tusimuachie Waziri tuipeleke BLM ndio ikaamuliwe kutunga kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, wengi ni risasi anapokwenda BLM kutakuwa hakuna Hizbu watupu watakuwepo tu watu wenye kuyajua Mapinduzi na kuyathamini na watakuwa Mahizbu hawatakubaliana nao. Kwa hivyo, tusimuachie Waziri kutunga kanuni hizi atatuumiza.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda nambari 9(1) "Waziri anaweza kwa kuzingatia masharti na makubaliano kuweka masharti kama atakavyoona inafaa, na kwa maandishi, kumsamehe mtu yeyote, au tabaka la watu au kitu chochote au aina ya vitu vyote au masharti yaliyomo katika kifungu cha 7 cha Sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, nitaisema kwa Kiingereza *'This is a blunder'*. Hiki kifungu kiondoshwe kabisa. Tumetunga sheria halafu mamlaka yote tumekwenda kumpa Waziri asamehe, wameshatoka watu washaichoma bendera yetu, washai-*fake* nembo halafu tumekwenda kumuachia Waziri yeye ndio asamehe, haya nasema tena vile vile, kama tumepata Waziri Hizbu na waliofanya ni Hizbu, wenzake si atawasamehe wote. Sasa kuna maana gani sisi ya kukaa hapa tukatunga sheria? Waziri Hizbu, waliochoma bendera Hizbu wenzake si atawasamehe siku zote. Kwa maana hiyo, Mheshimiwa hiki kifungu kiondoke hakitufai kabisa kije kifungu cha nambari 9(2) ndio kikae, hiki kiondoke kabisa hapa hakifai kuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar narudia tena Katiba inaruhusu kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, serikali ya kuchanganya kwa hivyo vitu vyengine hivi tunavyoweka tujue tunatoka wapi, tupo wapi na tunakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hiki kifungu kiondoke.

Mhe. Mwenyekiti, inazungumzwa jinai halafu inazungumzwa pesa, kwa mfano kifungu cha 10. Tuangalie ukweli na uhalisia wa dunia ulivyo, tunaposema ikithibitika atatozwa faini isiyopungua fedha za Kitanzania shilingi milioni moja na si zaidi ya shilingi milioni kumi, mimi nasema wazi wazi atai-*abuse* bendera au nembo ya Zanzibar, *okay*, lakini iwe *both* achezee faini achezee na kifungo na kifungo ndio kitangulie pesa iwe mwisho, tusiweke kila kitu pesa tu tuweke heshima ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona China hapo kama utai-*abuse* bendera ya China hapo zamani ulikuwa unanyongwa, siku hizi kutokana na ulimwengu umeendelea unafungwa nafikiri miaka 15 kama sikosei. Kaichezee bendera ya Iran Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa hata kuikiuka au kuichezea kwa njia yoyote huthubutu kwa sababu ni nchi ya Kimapinduzi. Kaichezee bendera ya Marekani, kama ukiichoma moto na ukithibitika unakwenda ndani miaka mitano kama sikosei sheria yao inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa tumetanguliza pesa hatukutanguliza nchi, naomba tutangulize kifungo adhabu ya mwaka mmoja na isiyozidi mitano halafu apate na faini. Kusudio langu Mhe. Mwenyekiti apate vyote, afungwe na atozwe faini

maana yake nini? Maana yake ni kwamba tunaweka heshima ya bendera yetu, na hatutowi nafasi kwa mtu yeyote kuichezea na kuikejeli bendera na nembo yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nchi ambayo imepatikana kwa Mapinduzi matukufu ya Januari 1964. Mimi ninasema Zanzibar haikupatikana kama ilivyopatikana nchi nyengine kwa bendera shusha bendera pachika, Zanzibar tumepindua, kwa maana hiyo mambo yake mengi yote lazima yawe maamuzi ya kimapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. Mimi naunga mkono hoja ya Mswada huu pamoja na mabadiliko yake kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Jimbo la Welezo. Sasa nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, akifuatiwa na Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kuuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Namba 1 ya Mwaka 1985, na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2004, na Kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayosimamia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya Mwaka 2016, na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza serikali kwa sababu kila kitu kina sheria yake na kila nchi zina taratibu zake. Katika dunia hii bendera ni kielelezo cha nchi, wimbo wa taifa ni kielelezo cha nchi lakini nembo ni kielelezo cha serikali. Pia wimbo maalum kwa Zanzibar ni kielelezo maalum kwa jambo maalum ambalo limetuweka humu ndani kuwa leo tunasimama hapa baada ya kutokea. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa kuliona hili linafaa na wakati huu mzuri tuliokuwa nao hasa tukizingatia kwamba sote tuliokuwemo humu tuna imani ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ni halali. Naamini Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wote waliokuwemo humu, sijui na siamini kama kuna mmoja ambaye atakwenda kinyume na Mapinduzi ya mwaka 1964 ambaye hayatambui. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa dhati kabisa, kwa kuona kwamba pana haja ya kuweka vitu ambavyo vitatuelekeza vizuri sisi na wageni wetu wanaotoka nje, pamoja na vizazi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, bendera ni haki ya nchi lakini bendera ni haki ya mwananchi. Ndio maana kwa wenzetu Mhe. Mwenyekiti, tuliokuwa wanariadha au wana michezo mbali mbali, kwa mfano wakiondoka timu ya *basketball* hapa Zanzibar, wakiondoka timu ya riadha, wakiondoka timu ya mpira wa miguu au hata mchezo wa *badminton* kama wanakwenda nje kushindana basi watapewa bendera ya nchi yao yaani taifa lao. Kwa hivyo, nasema bendera ina matumizi maalum kwa kazi maalum. Kwa hivyo, bendera ni kielelezo tosha kwamba Zanzibar alama yake ni hii hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2008 kama sikosei Zanzibar ilishiriki *challenge* Uganda, na mimi nilikuwa kiongozi wa timu ya taifa wakati huo, tulikuwa tuna wimbo wa taifa na bendera ya Zanziabr, sio ya Muungano, ya Zanzibar inapeperushwa pale. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kile ni kielelezo tosha kwamba wimbo wa taifa wa nchi ya Zanzibar, lakini pia bendera ya taifa ya Zanzibar kwa wakati huo na pia mpaka leo inaendelea.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba bendera ni alama ya kwanza kujua huyu ni taifa gani. Ombi langu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kuna masharti mengi ambayo yamewekwa kwa kuilinda bendera yetu na kuipa heshima bendera yetu, lakini pia zinatokea fursa maalum. Kuna na wanamichezo wanacheza michezo mbali mbali, wanapocheza michezo ile hutaka kuvaa bendera yao au kufanya usanii kwa bendera yao. Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia waziri husika pawe na kanuni maalum zitakazotungwa kuwa bendera hii inaweza kutumika wakati gani na kwa kazi gani. Yaani bendera inajulikana ni kielelezo cha nchi, lakini pia ni kielelezo cha taifa letu, lakini timu ikitoka inawakilisha taifa pale, kwa wasanii haya yanajitokeza. Kwa hivyo, naomba kanuni zitakapotungwa ziwaangalie na wao kwa mambo yao ambayo yanastahiki huko waliko.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa kuna mchezo mchafu juu ya bendera zetu. Sasa hivi tuko kimya tunakwenda na mambo yetu shwari hapa, kuna watu wanaleta kejeli kama kudhihaki. Kuna watu wanaziweka bendera ya *Afro Shirazi Party*, bendera ya Muungano, bendera yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini wakati huo wakifanya maandamano yao wanajijua wenyewe, basi huwa ile bendera ya Mapinduzi wanaizonga isionekane, maana hawaitambui, lakini wanaichukua kama kuikejeli. Kwa hivyo, mimi naomba hii sheria iliyowekwa, Mhe. Waziri naomba sana utusikilize. Mhe. Mwenyekiti, sisi ni wajibu wetu kusema na kuelekeza, kama panatokea tatizo la aina hiyo, basi wanaohusika wachukuliwe hatua kali ili iwe ni fundisho kwa wengine. Utawasikia wengine wanasema tunataka nchi yetu wee! tunataka nchi yetu, sijui ipi. Mimi najua nchi yetu ndio hii ya Zanzibar na bendera yetu tunaiheshimu ni hii hapa iliyokuwepo.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye mambo ambayo yanafaa katika Mswada huu, yote yanafaa lakini ambayo yameleta faraja ni wimbo wa taifa. Wimbo wa taifa Mhe. Mwenyekiti, ni kielelezo tosha kama nilivyotangulia kusema hapo mwanzo na unakubalika kwamba huu ni wimbo wa nchi fulani. Kwa hivyo, naomba tu kwamba wimbo huu uwe na sehemu maalum kwa kazi maalum, sio kila pahala. Unakwenda pahala fulani unakuta wimbo unapigwa kiajabu ajabu, inakuwa hadhi na heshima ya wimbo ule haipo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili la Wawakilishi linapofunguliwa siku ya mwanzo hupigwa wimbo wa taifa, na tukifunga Baraza mwisho kuahirisha unapigwa wimbo wa taifa. Kwa hivyo, hivi ni vielelezo maalum kwa kazi maalum vinakubalika, lakini pia kwenye sherehe zetu mbali mbali. Lakini wengine utakuta tu pengine Mungu ibariki Zanzibar, sijui nini inakuwa kidogo haileti maana. Kwa hivyo, vielelezo vilivyowekwa hapa ni vizuri juu ya kuuweka vizuri wimbo huu na kuipa heshima yake nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine zuri ni kwamba kuna wimbo maalum ambao ni wimbo wa kumbukumbu tulikotoka. "Sisi sote tumegomboka kwa ndugu zetu waliopotea". Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba wimbo huu utolewe vyema na uelekezwe kama ulivyoelekezwa maskuli yote, yaani skuli za serikali pamoja na skuli za binafsi. Wimbo huu uwaelekeze wanafunzi wetu na uwaeleweshe madhumuni na sio vibaya pakiwa na tafsiri, kwa sababu watoto wadogo watakuwa wanaimba tu, "sisi sote tumegomboka," kwa nini hawajui. Lakini waelezwe kwamba tumegomboka kutokana na kitu fulani.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo ningependekeza sana kuwe na jambo maalum ambapo kwenye historia za nchi za wenzetu. Kwa mfano, China ukenda utamkuta Mao Tse Tung popote utakapokwenda, ikiwa katika viwanja au kwenye maeneo mbali mbali, yule kiongozi ndiye aliyeleta ukombozi katika nchi yao. Kwa hivyo, na sisi kwetu sio vibaya, ningeshauri sana na ninamuomba sana Mhe. Waziri tujaribu kuweka picha za Marehemu Mzee Karume katika skuli zetu zote, ikiwa unaingia ofisini pale unamuona ili watoto wetu wamjuwe ni nani aliyegomboa nchi hii hadi kufikia hii leo tulipo.

Nasema haya Mhe. Mwenyekiti, kuna vijana wengi hasa Rais wa mwanzo wa Zanzibar hii hawamjui kwa sura, kwa kuwa keshatangulia mbele ya haki haidhuru, lakini picha ni kumbukumbu nzuri zinatosha. Kwa hivyo, ningeomba tu kiongozi wa mwanzo wa nchi hii Marehemu Mzee Abeid Aman Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi amin, ziwepo picha zake katika maskuli au taasisi muhimu za nchi yetu iwe ni kumbukumbu ya kukumbuka

kwamba hii "sisi tumegomboka" kwa kitu gani ambacho kilicho mbele yake kinamuonesha yeye, sio vibaya. Hata na wale Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi la mwanzo wakawekwa katika alama mbali mbali iwe ni kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, hili nasema kama ni kitu muhimu sana. Leo tumepindua nchi yetu hii, nashukuru tumesimama hapa. Lakini vijana wengi narudia tena, wanafunzi wengi hawamjui Marehemu Mzee Karume kwa sura, na wakati picha zake nzuri zimo zimehifadhiwa vizuri, tunaomba zitafutwe njia zozote ziwekwe na zionekane picha zake.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu nembo ya serikali ambayo ni kielelezo tosha na hiki hakitakiwi kufanyiwa masihara, serikali yoyote ina nembo yake. Kama vilabu vya mpira kuna Yanga, kuna Simba, kuna Maji Maji na nyenginezo. Hii yote Mhe. Mwenyekiti, ni ishara kwamba hii alama inafaa na inaheshimiwa. Kwa hivyo, kwa kuwa imeletwa katika sheria hii na imefanyiwa marekebisho mazuri. Mimi naomba tu kwamba nembo hii itumike vizuri na itumike kwa manufaa ya serikali yetu, na chochote cha alama ya serikali yetu kiwemo ili kuelezea kwamba nembo hii ni kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi nafikiri hilo halina matatizo na zuri linafaa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme tu kwamba maelezo mengi yameelezwa katika Mswada huu, na ni maelezo mazuri ambayo yanafaa, marekebisho ni jambo la kurekebishwa. Lakini pia sehemu ya tatu kuna mambo mengine ya makosa na adhabu. Katika mambo haya yote niliyozungumza yana sheria na kanuni zake. Kama kuna makosa adhabu iliyowekwa itumike, na kama kuna makosa ambayo yanastahiki yakufanywa zaidi yaongezwe, lakini tujuwe tu kwamba sheria ni yetu sote, yeyote anayekwenda nayo kinyume imkamate na imdhibiti, isije kumuonea aibu mtoto wa fulani au shemegi yake fulani hakuna. Mimi naomba sana suala hili tuliangalie kwa maslahi ya kulinda bendera yetu, kulinda wimbo wa taifa wetu pamoja na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba baada ya hayo machache naunga mkono Mswada huu wa Sheria wa Marekebisho haya, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuyachangie na tuipe uwezo serikali yetu kwa matumizi mazito ya bendera, wimbo wa taifa, nembo pamoja na wimbo maalum. Kwa hivyo, baada ya hayo nasema tu kwamba mimi mwenyewe nimeridhika na naunga mkono kwa asilimia mia moja, pamoja na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele ambao wanataka maendeleo katika nchi hii na usalama wa nchi yao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kwa mchango wako. Sasa namuomba Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo), akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Mwinyihaji Makame ajitayarishe.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Mswada huu kwa jioni hii ya leo, ikiwa Mswada huu ni miongoni mwa Miswada bora ambayo iliwasilishwa Barazani katika kipindi hiki ambacho tunaendelea kutoa maoni yetu kwa maslahi ya nchi yetu na vizazi vyetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia niwapongeze Kamati ya Viongozi Wakuu kwa mchango wao juu ya Mswada huu ambao wametoa mapendekezo yao na marekebisho yao mbali mbali katika kuchangia na kuona kwamba kuna mambo yanafaa na yaliyokuwa hayafai yaondolewe, katika kuboresha nembo zetu, wimbo wetu wa taifa pamoja na bendera.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika sehemu zangu ambazo nimekusudia kuchangia ili nitowe lile ambalo nimeliona na mimi niweze kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 7 ambacho wenzangu walikwisha kuchangia, lakini naomba nitie msisitizo, kinasema;

Kifungu cha 7

"Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo:

a) Kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kinachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza"

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kuna wajasiriamali ambao tumewaona wakishona viatu, lakini baada ya kushona viatu vile mikanda walioifanya kwenye viatu vile wanatumia nembo ya bendera. Lakini vile vile kuna wengine wanashona mikanda ya suruali, nao hawa wanatumia nembo ya bendera. Je, Mhe. Waziri wajasiriamali hawa sikuona kifungu ambacho labda waliwekewa kwamba wao baada ya kutengenezwa sheria hii kutakuwa na kifungu ambacho ama watakapofanya mambo haya ya kuweka alama au kutumia nembo hii ya bendera, itawafanya wao waweze kuwa na... *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia katika ukurasa wa 240 kifungu cha 8 (2) (o) ambacho kinasema;

"8 (2) (o) Katika uchapishaji na uzalishaji"

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia sasa hivi tunatunga sheria ambayo itasaidia kuweza kuweka masharti bora na kiwango bora cha bendera yetu. Lakini kule Pemba kulikuwa kuna sehemu ambayo bendera yetu inapatikana. Kwa mfano, sehemu ya Mkuu wa Mkoa, pale ukifika ilikuwa ndio unapeleka pesa yako shilingi 60,000 baadae ndio unapewa bendera. Lakini sasa hivi kumejitokeza wale wajasiriamali ambao wanazitengeneza hizi bendera na kutumia zao sijui kama ni za ukili au za vipi, halafu baadae ndio tunaanza kusema kwamba bendera zetu zinachakaa na rangi zetu tunazozifanya sizo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi napata wasi wasi kwamba tunaboresha mambo, lakini tatizo sheria baada ya kwishakuzitunga katika kuzisimamia tunakuwa kidogo tuna uzito.

Kwa hivyo, mimi niendelee kutoa mchango wangu kwamba Mhe. Waziri aangalie ni watu gani ambao wanastahiki kupewa huu ushonaji wa bendera au uzalishaji wa bendera iwe hapo zikitakikana kwenye ofisi yoyote au kwa taasisi yoyote basi iwe zinapatikana sehemu maalum ambazo zimewekwa kwa watu hawa kuweza kuzitumia na isiwe kwamba kila mtu aliyekuwa anajua kuchora ama kuzizalisha anafanya tu. Ndio vile ambavyo kwamba kila siku tutakuwa tunaendelea kutunga sheria na kusema kwamba bendera imechakaa au imefanyaje, kumbe vitambaa vinavyotumiwa havina ubora.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili hili suala la vitambaa, tumeona kwamba pengine mtu anaweza kwenda dukani akakata kitambaa akaona hiki kimefanana wacha nikashone bendera na niweke katika sehemu zangu nifanye biashara. Kwa hivyo, nimuomba Waziri na hili nalo alisimamie aone kwamba kuwe na utaratibu maalum wa kuweka hivi vitambaa ambavyo vitasaidia katika upatikanaji wa hizi bendera zetu ambazo zina ubora. Isiwe tena mtu anakwenda dukani kipo kitambaa kimefanana na njano ile au bluu ile aweze kuchukua tu na kushona bendera.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sehemu ya tatu kuhusu makosa na adhabu. Katika kifungu cha 10 kimesema;

Kifungu cha 10

"Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote au kubadilisha neno lolote au kuchapisha maandishi yoyote kwa nia ya kukashifu au kudharau au kukejeli Bendera ya Zanzibar, nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar atakuwa ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini ya fedha".

Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu mimi niseme hii adhabu ni ndogo kwa mfano mwaka jana tulishuhudia kule Micheweni kulikuwa na bendera inasemekana ni bendera ya chama, kulitokezea vurugu mimi sikuwepo lakini nasikia kwamba bendera ile ya chama ilichanwa tuliona wale ambao wameichana ile bendera jinsi gani walivyopata matatizo. Kwa hivyo hii bendera ya chama tu watu walipata matatizo seuze hii bendera ya Serikali ambayo ya kitaifa watu wote wanayo. Kwa hivyo hicho kifungu kimesema kwamba mtu huyu atakayefanya tendo hili kinyume na sheria atatozwa faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha mwaka mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hichi kifungo na hii adhabu mimi naona ni ndogo kwa jambo hili la kitaifa ilikuwa angalau mtu huyu atozwe kiasi cha shilingi labda pengine milioni ishirini au kifungo cha maisha. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, watu wanaweza wakenda kuichukua bendera wakaichana au wakaikejeli kwa njia ambazo wanazitaka wao baadae watu hao hao wakaona mimi kwa faini ambayo imewekwa au kwa kiwango hichi mimi naweza kujitetea. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hichi kifungu kiongezwe hii adhabu ni ndogo sana kwa mtu kama huyu ambaye atakejeli.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa wa 240 katika kijifungu:

> "(k) Matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika Skuli za Umma na Skuli za binafsi."

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia baadhi ya skuli zikiwepo za binafsi na hata za Serikali kwa mfano mimi pale nyumbani katika jimbo langu Chwaka/Tumbe ni skuli kubwa ambayo ilijengwa na Wachina tena ambayo kuna wanafunzi wa vidato tofauti tofauti ambao walikwenda pale kama michipuo. Na wengine kwa mfano Skuli ya Tumbe ambayo ndio kubwa lakini huu wimbo sasa hivi hauimbwi na vile vile hata kielelezo hichi cha hii bendera hakipo, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri ingawa jana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu alitwambia kwamba ameshatoa madodoso na msisitizo kwa baadhi ya skuli kwamba huu wimbo wa taifa uendelee kuimbwa.

Lakini vile vile kuwekwe sheria maalum na kifungu maalum ambacho kitawafanya watu hawa wakuu wa skuli pamoja na wasaidizi wao pale ambapo itapita skuli kuwe na ukaguzi maalum, pengine Jumatatu watu wanakwenda skuli waangalie wanafunzi je, asubuhi walipofika baada ya kupanga *assembly* huu wimbo umeimbwa? Je, hii bendera katika maskuli ipo au haipo kwa sababu zile sehemu nyeti wanafunzi wanapata kujua na kuangalia. Kwa sababu mimi wakati nasoma tulikuwa tunasomeshwa rangi za bendera kwa hivyo unaweza

ukamuuliza mtu swali bendera wakati mwengine anapopanga *assembly* anaiona anapata ile angalau kujibu, lakini haipo kwa hivyo mwanafunzi yule atabakia tu kusikia zile rangi za bendera ambazo yeye mwenyewe atakuwa hana uhakika kama ndizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi nimekusudia kusema hayo niliyoyaona katika kuchangia kwangu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na nawaomba waheshimiwa wenzangu tuuchangie mswada huu ambao una umuhimu na vigezo tosha vya nchi yetu kwa manufaa ya Zanzibar na sote kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia mswada huu, lakini mimi kwanza nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Chake Chake ambao ni mji wa pili wa Zanzibar, pia napenda kusema kwamba katika kuchangia kwetu hili suala letu la wimbo wa taifa, nembo ya Serikali na bendera ya Zanzibar hivi vitu si vipya katika nchi yetu na ni vitu ambavyo kila mmoja anavielewa. Lakini nimefurahi sana kwa Serikali kuleta ufafanuzi zaidi ambao kwa kweli unaweza kuwafahamisha watu ambao wengine ufahamu wao ni mdogo ama ukawa bado hawaufahamu kutokana na umri wao.

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kuangalia sana upeo halisi wa sheria yetu hii ni kwamba nimeona katika kifungu cha Namba sita ambacho kinasomeka bendera ya Zanzibar, nembo ya Serikali na Wimbo wa taifa wa Zanzibar vitatumika katika maeneo ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria. Hii Nambari sita imesomeka vizuri lakini mimi kwa hapa naona ungekuwa na mchanganua wa kila nafasi baina ya bendera, baina ya nembo na wimbo vikawa katika mwelekeo ambao utakuwa una masharti maalum, kwa sababu kila jambo katika hapa linatumika katika vitu ambavyo anaweza kulitumia mtu katika maelekezo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu nam. 7 cha Sheria hii kinasema ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia bendera ya Zanzibar, nembo, wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo. Ni mambo mengi ya kibiashara na kila kitu sasa wimbo kama wimbo matumizi yake yako tofauti, wimbo kuna watu hufurahi tu katika vikundi wakaweza kuimba wala si pahala pa sheria wala si pahala popote lakini kwa furaha zao na kwa mapenzi yao wakaweza kuimba. Haya ni mapenzi sasa tukianza kuwafanyia watu sheria kubwa ya kuwabana jambo hili ina maana hata kulifanyia mazoezi basi linashindikana maana yake kawaida ya nyimbo ukiifanyia mazoezi unaweza ukaikosea mwenzako atakurekebisha ilimradi tu maudhui yake yawe yamefanana.

Sasa Mheshimiwa ningeomba sana tubague bendera, bendera kwa kweli kama itabakia kuwa na ugumu fulani ambao utatishia mpaka mtu kuiogopa basi hata ndani ya gari yako itashindwa kuingiza mle ndani kwa sababu hili jambo bendera unawaona wenzetu wanavyokwenda kwenye michezo, sasa sisi sijui kanuni zetu zitatufanya vipi mwengine atajifunga kama analilalia utakuja kumwambia unailalia bendera, mwengine atajifunga kilemba utamwambia unajifunga kilemba, mwengine atajifunga msuri. Sasa bendera ni alama hii alama kwa madhumuni maalum ni utambulisho wa eneo au ni utambulisho wa kile kitu ambacho umekwenda kukikusudia pale. Sasa nilikuwa napigania sana kuonyesha umuhimu wa kubagua sheria zake baina ya nembo, wimbo na bendera, kwamba tukiviwekea vikwazo kwa pamoja itakuwa ni tabu katika matumizi kama hayo.

Sasa nichukue nafasi hii Mheshimiwa kwamba kwa vyovyote tuweze kuvibagua kwa sheria zake na umuhimu wake ili tuwapunguzie watu kuwa na joto wakati wa kuvitumia vitu vile, huu wimbo, bendera na nembo na tuweze kuweka mchanganuo hasa inatumika vipi au mambo gani, sasa wengine wanatengeneza fulana ambayo ukiitizama unaiona bendera. Sasa sijui itakuwa ni marufuku kuvaa fulana kama hiyo au sijui itakuwaje, sasa ningeomba Mheshimiwa kwamba utakapokuja kutuletea habari hizi uweze kutufungulia kwamba fulana itakayofanana na bendera itakuwa ni marufuku au inakuwaje, maana yake bendera ndio tunayozungumza ni rangi na kuna fulana zinafanana kabisa na bendera sasa hapo ningeomba hilo.

Lakini pia ningeomba sana Mhe. Waziri suala la bendera kwa upeo huu ambao tunautumia basi ikapewa upeo mpana sana ikatumika sana bendera ya Zanzibar katika kujitangaza hasa watu wetu wa timu zetu wanapokwenda kwenye michezo ya nje unawakuta kila mtu anavaa fulana yake. Mimi ningeshauri Mheshimiwa timu za taifa zinapokwenda nje hata kama ni msewe basi zikavalishwa bendera ambazo ni rangi za fulana ambazo mtu akituona anajua wale wanatoka sehemu fulani. Hivi karibuni tu hapa walikuja timu za Taifa zilipita *Airport*, nembo kabisa za fulana zao ni bendera zao lakini sisi tukiiwekea vikwazo sana tutaogopa sana, sasa katika hili nilikuwa nachangia zaidi kwamba tuzibague tusiziwekee sheria moja zitakuwa kidogo zina ugumu fulani. Maana yake wimbo unaujua unavyoimbwa bendera unaijua inavyotumika na nembo unaijua inavyotumika hili nilikuwa nalisema sana kwamba liangalie upeo halisi wa mambo haya.

Lakini pia Mheshimiwa nakuja kwenye upande wa Waziri suala la bendera likimaliza hapa limemaliza upande wa kumpa tena kurekebisha haupo, maana

yake huku nimeona kwamba baadhi ya mambo mengi yanamalizwa na Baraza la Mapinduzi. Bendera ikishakufanywa na kanuni zake na zikimaliza kama kutatokea haja ni moja kwa moja kwenye Baraza la Mapinduzi kule kule hakuna nafasi ya Waziri, Waziri ni mwanasiasa anaweza kwa *interest* zake akafanya analotaka mwenyewe. Kwa hivyo ningeomba kwamba hapa Waziri abakishwe kuwa Waziri kwa sababu nimeona kuna vifungu hapa vyengine mpaka mtu anapokosea eti Waziri ana uwezo wa kusema kwamba kifungu Na.9 kinasema Waziri anaweza kwa kuzingatia masharti na makubaliano yaliyowekwa masharti kama atakavyoona inafaa na kwa maandishi kumsamehe mtu yeyote au tabaka la watu, kitu chochote au aina ya vitu vyote au masharti yaliyomo katika kifungu cha saba cha sheria hii.

Mheshimiwa hapa ina maana Waziri anapewa nafasi mtu atakapokosea atakapofanya mambo wakati hili ni suala la nchi Waziri anaweza akamsamehe, anaweza kutoa kibali fulani mimi hapa naona kwamba tunazunguruka sana hii sheria kila mmoja anafahamu umuhimu wa nchi, anafahamu umuhimu wa bendera, anafahamu umuhimu wa nembo, anafahamu umuhimu wa wimbo wa kitaifa sio wa kuchezewa habari ya kusamehe, Waziri mimi ningeona kwamba hii habari haipo. Mimi nataka nikwambie Mheshimiwa sisi tuko katika mkondo wa Serikali ambazo za vyama vingi tumeshayaona mengi yamejitokeza, kuna moja humu sijaliona limefikia wapi na ambalo linatendeka sana katika vifungu vyote ambavyo tumeboresha sijaona.

Mheshimiwa sisi wakati wa uchaguzi tunakuwa na mashaka sana watoto wanaotumiwa au watu wanaotumiwa wakati wa uchaguzi ni watoto wa umri chini ya miaka 14 ambapo anaambiwa nenda kaichane au kaitie moto ile bendera hatukuwakea vikwazo watoto ama kitu gani ambacho hapa kinaweza kikafanyika, lakini hatokuja mtu mzima kuichoma bendera anajua yeye atafungwa atatuma watoto watakwenda kuzichoma. Sasa hili nilikuwa nataka muliangalie hasa Waziri aangalie hapa utakapokuwa katika maelekezo yako ulitizame mara nyingi sana chaguzi zetu tukifanya watoto ndio tunaowatumia, sasa je, hata mtoto kawekewa mipango humu ya kuheshimu hichi kitu kwa hivyo hili nilikuwa nalizungumza sana.

Lakini pia nije tena nazungumzia kwamba katika masuala mengine tumempa nafasi sana Waziri wa Elimu kushughulikia masuala haya, lakini mimi nataka niseme kwamba Wizara ya Elimu ndio muhimili mkubwa wa wanafunzi na maskuli ambayo takriban sio ya Serikali mpaka ya binafsi, lakini Mheshimiwa nataka nikwambie bado ziko skuli ambazo za Serikali hazijakuwa kamili katika wimbo huu kwa sababu ya siasa yake tu ya rohoni hasa akiwa mwalimu Mkuu. Na skuli ambazo ni za binafsi ndio kabisa anasema hana muda watoto

wakasome kiingereza sijui wakafanye nini, sasa huyu mtu ambaye hata kama ni mgeni amekuja kufanya biashara hapa ina maana hatuthamini na sheria hapa ichukue mkondo wake wala si Wizara ya Elimu, mambo ya kubembelezana katika mambo ya kisheria yamekwisha wakati wake hakuna Mheshimiwa wakati wa kubembelezana umekwisha, lakini sasa tunapokwenda kila mmoja sheria anaifahamu ni dharau, yeye kama mzungu anaweza kudharau bendera yake huko. Kwa hivyo na sisi kama anakuja kwetu Wizara ya Elimu kama inataka kumpa kibali basi ahakikishe mambo haya yanafanyika.

Mheshimiwa nataka nizungumzie pia na wimbo wa mashujaa, wimbo wa mashujaa tumeshaukubali sana lakini nausikia sana kwenye sherehe za Mapinduzi mara nyingi sana kwenye skuli ndio unapelekwa pelekwa lakini kati kati ulikufa kabisa hata kuelekezwa hauendi. Sasa naomba sana Wizara ya Elimu kama mmepewa jukumu hili ili kuwaboresha watoto katika masuala haya na walimu nao ikiwa mwalimu atakwenda kinyume basi na mwalimu achukuliwe hatua, kwa sababu wanafunzi wanamfuata mwalimu na walimu ndio chachu ya mambo haya wanayoyafanya hilo nilikuwa nalizungumza ili tuweze kuliweka vizuri katika masuala haya.

Lakini pia nataka niseme inakuwa aibu timu zetu zozote ambazo zinakwenda nje inapigwa wimbo wa taifa au unakwenda pahala popote hata kama hapa Zanzibar unakuta mtu analia kwa ule wimbo wake wa taifa, wana imani na nchi yao mpaka wanajishika moyo, kwetu sisi hata ukiimbwa unamkuta mtu hata hatizami kabisa kama hana maana nao, Mheshimiwa dharau hii kama mchezaji tukimuona kwenye TV amekwenda pale haimbi ule wimbo wa taifa asipelekwe tena mara ya pili hana maana huyo kwa sababu anatudharau kabisa. Lazima tuangalie hapa sio pahali pa mchezo tunaona vitu vidogo vidogo tu ni bendera ni kitu gani, lakini tunaangalia mpaka kwenye TV kama bendera inaanguka hasa Wachina na watu wengine ambao wanaumwa na nchi yao anakufa nayo bendera haiangushi chini sisi hatuthamini, bado tuko katika mambo madogo madogo ambayo hatujajua baina ya chama wala Serikali tunachanganya tu serikali hiyo hiyo chama ni hicho hicho.

Kwa hivyo ningeshauri sana elimu itolewe vizuri sana baina ya bendera ya chama na bendera ya Serikali, itolewe vizuri sana nembo ya Serikali, na utolewe vizuri sana wimbo wa Serikali kwa heshima zake sio ule wimbo wa mwanamuziki Diamond hapa hapana ule ni wimbo maalum, ikiwa Baraza la Wawakilishi Mhimili mmoja akiingia hapa hasemi mtu wa aina yoyote siku ya ufunguzi mpaka wimbo umalizike na siku ya kufunga mpaka wimbo umalizike, itakuwaje raia na mtu wa chini wadharau lazima tufike pahala tuweze kukaa katika *position*. Sasa mimi nilikuwa nashauri sana ni aibu unamkuta mtu

anakwenda katika michezo wimbo wa taifa haujui hicho nilikuwa naangalia, redio zetu televisheni zetu zinakuwa mtu kwa kuwa ni ya kwake hapigi wimbo wa taifa inakuwaje anapata kibali kutoka wapi, hivyo ningeshauri sana masuala kama haya yakatizamwa.

Lakini narudia tena kuzungumza habari ya umri wa watoto wanatumika vibaya katika kuharibu haya mambo na sheria yetu inafanya mtoto wa miaka kumi na nane hajafika huyo haulizwi kitu, basi utakuwa ni mchezo ambao haufiki mwisho maana yake matumizi yetu ni hayo. Kwa hivyo mimi nilikuwa nachangia hayo kwa sababu ya mwelekeo kidogo wa masuala haya ambayo kwa ukweli ni muhimu sana.

Lakini jengine nazungumza kwamba mtu mwengine yeyote hili suala la Na. 10 katika sheria inasema:

> "10. Mtu mwengine yeyote atakayefanya kitendo chochote au kubadilisha neno lolote au kuchapisha maandishi yoyote kwa nia ya kukashfu, au kudharau, au kukejeli bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar atakuwa ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na kifungo kisichopungua mwaka mmoja au kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo."

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia sana nimeona kwenye upeo mkubwa umekuja kwenye masuala ya faini kuliko kuwa na masuala ya kifungo. Mhe. Mwenyekiti, unajua mtu kwa jeuri yake anaweza akafanya jeuri sana ingawa vyote viwili vinaweza vikatumika, lakini ni vizuri sana maana yake hapa itakuwa kama tunafanya biashara ikiwa mtu shilingi milioni moja anaweza akachana tu, shilingi milioni moja sio pesa nyingi kwa sasa hivi, lakini kifungo kingeanza mwanzo baadae tuangalie hali halisi inavyoangalia hii *face* ambayo imezunguka hapa ni kwamba tumeanza na faini. Mheshimiwa tuanze na kifungo sio faini halafu ikiwezekana ndio hiyo faini.

Sasa mtu unapoliweka neno mwanzo linaonekana kwamba faini ni bora kuliko kifungo, mimi ningeshauri hapa lianze na kifungo halafu faini ije baadae. Kwa hivyo, ningeshauri sana katika kifungu nambari 11 ili iwe adhabu ambayo sio ya kuchezea kirahisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii nilikuwa najaribu ibadilike ingawa vyote viwili vinatumika lakini nambari moja kianze kifungo halafu fedha ije baadae. Kwa sababu tumeangalia sana upande wa Zanzibar mimi nasema kweli tukitaka tusitake hatujakuwa makini sana katika masuala ya kuwekeana heshima.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan naomba umalizie nakuongeza dakika moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Haina shida Mheshimiwa lakini nilikuwa nazungumza upande wa Zanzibar tunatunga sheria sana, tuko makini katika kutunga sheria, tunatunga sheria nzuri, lakini usimamizi unakuwa hautimii malengo. Sasa hizi sheria zinaweza kuwa tulikuwa hatuna tumebadilisha na tutazitunga lakini usishangae hii ikaja tena alifu ulelaulela. Kwa hivyo, nilikuwa nazungumza na watakaokuwa wasimamizi wa sheria hii, mimi ningeomba sana serikali si jambo la mchezo wala si la kuchezea.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Sarahan, sasa nimwite Mhe. Mwinyihaji Makame. Lakini pia nilikuwa namuomba radhi Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kabla ya kumwita yeye nitamwita Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia wasaa huu kuchangia mswada huu ulioko mbele yetu wa kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya Mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar na kutunga sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina *observations* chache tu. Kwanza kwenye kutunga au kwenye kifungu cha 8 ambapo kinampa Mhe. Waziri uwezo wa kutunga kanuni. Mhe, Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwanza kabisa nimeangalia sana sikuona katika hizi kanuni zilizokuwa *highlighted* humu inayozungumzia sifa za kitambaa cha bendera. Nafikiri hili ni suala la msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona kuna bendera aina nyingi nyengine zinatumia vitambaa vya bafta kuwa bendera. Sasa hii ni bendera ya nchi lazima iwe na heshima yake na napongeza sana wazo hili la ku-*review* mswada kuleta sasa vipengele ambavyo vinaongeza heshima ya bendera yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo ukilinganisha na Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bendera ya *CDF*, Bendera ya Mkuu wa Majeshi na Bendera ya Mhe. Rais zina heshima yake kwa uzito wa kitambaa unahisi kweli hizi ni bendera za wakuu. Sasa na hii bendera yetu ningeshauri sana tuiwekee sifa itajwe hasa kwenye Kanuni, Bendera ya Zanzibar kitambaa chake kiwe

hivi, akinamama wenyewe wanajua zaidi nailoni au *cotton* watataja, lakini lazima iainishwe isiwe kitambaa chochote tu cha bendera.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni saa za kupandisha na kuteremsha bendera. Mheshimiwa sote mashahidi katika shehia zetu tunakuta bendera haiteremshwi mpaka inachanika, siku ya kuteremshwa kwake siku ya kubadilishwa. Sasa uwekwe utaratibu na nidhamu saa 12 inapandishwa, saa 12 inateremshwa. Tulipokuwa wadogo siku zile baada ya Mapinduzi hamasa zile wakati honi ikilia popote ulipo unatakiwa usimame, ukaze mguu na matarumbeta yanalia bendera inateremshwa. Sasa si vibaya kama watu wako maeneo ya Malindi yale, maeneo ya ng'ambu, maeneo ya Ziwani Makao Makuu ya Polisi, bendera inateremshwa na ile tarumbeta inalia lazima usimame pale bendera inateremshwa. Hiyo nafikiri ndio inarudisha ile hisia na hamasa kweli hii nchi ya Kimapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, ni vigumu kuzuia nchi nzima harakati lakini nasema sehemu hizo ambazo tarumbeta inapigwa lazima watu wasimame.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mwengine ni kwenye wimbo wa taifa. Wimbo wa Taifa Mheshimiwa mtakubaliana na mimi ni kweli lazima nao kwenye vyombo vyetu vya habari wimbo wa taifa upigwe. Lakini sasa ukiangalia *ZBC Radio* siku hizi haifungwi, nafikiri sijui tumuombe Mwenyezi Mungu sijui mpaka lini, lakini saa 24 ni maendeleo tunashukuru. Zamani saa 12 unaanza wimbo wa taifa baadae tena inakuja dua ni vyema, sasa siku hizi kabla ya saa 12 yaani ikifungwa saa sita usiku bora nianze kinyume nyume, saa sita usiku wakati inafungwa ilikuwa inapigwa dua halafu wimbo wa taifa inazimwa *studio*. Lakini sasa saa sita usiku ikimaliza *ZBC Radio* inaingia *Spice FM* moja kwa moja hakuna ule wimbo wa taifa umepotea.

Kwa hivyo, asubuhi wanamaliza *Spice FM* wanarudi *ZBC Radio* pia wanaunga moja kwa moja wimbo wa taifa haupigwi. Sasa hata watu waliokuwa wamezowea heshima ile haipo. Kwa hivyo, mimi nataka kushauri tutafute utaratibu katika kufunga na kufungua kwa sababu ile ni redio moja wanamaliza wanakwenda *Spice FM* kwa majina waliyoyataja wenyewe, ijapokuwa tunajua ndio hiyo hiyo, lakini wametaja majina mawili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, pia nashauri hata huu wimbo wetu wa sisi sote tumegomboka, ni vyema pale saa sita usiku unapigwa wanafunga *studio* na bendera inatembea ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wimbo unaimbwa ule lazima itakuingia hamasa na vijana wetu siku nyingi siku hizi *Alhamdulillah* wanakaa macho zaidi ya saa sita. Kwa hivyo, mimi nataka kupendekeza tutafute utaratibu Mhe. Waziri mwenyewe atakaa na wataalamu

tuone jinsi gani vyombo vyetu hivi viwili vya televisheni na redio wimbo wa taifa na suala la sisi sote tumegomboka upigwe katika kufunga na kufungua idhaa zetu.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nije kwenye mchora nembo hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lazima tumpongeze mchora nembo hii kwa kweli ni mkereketwa mzuri na amebuni na kuonesha kweli vipi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilivyopatikana. Silaha zote zipo hapa, ukiangalia bendera ya Saudi Arabia mbali ya *Lailahailallah Muhammad Rasulullah* kuna kitu pale, wengine wananambia kuna upanga. Sasa inaonesha wazi na haya mambo mengine yaliyomo mnazi, mkarafuu na visiwa vyetu viwili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa taarifa ziliopo yule mchora nembo tunashukuru kwamba malipo yake amefanyiwa baada ya kipindi kirefu, lakini kwa kweli salamu tulizozipata kwamba hakupatiwa haki yake inavyopaswa. Sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri hili bora akae naye tusimnyonge huyu kajitolea na akashinda mashindano ya nembo, kashinda na kawashinda watu akapatikana yeye akachora na katupa kitu cha milele cha daima mpaka leo. Ingekuwa nchi za wenzetu Ulaya huko yule ana *owners right*, ana *percentage* yake kila mwaka au miaka miwili anapewa. Sasa yeye sijui kapewa kiasi gani lakini kuna malalamiko kwamba alichopewa kwa kweli hakuridhika na kama hakukuwa na makubaliano kidogo haipendezi, ni mzalendo huyu kajitolea, mwenzetu lazima atizamwe kwa jicho la huruma.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri hili suala aliangalie vizuri sana haipendezi kabisa mtu kama huyu kusikitika kwa kitu kama hichi. Lakini nasikia hivi sasa kuna marekebisho kidogo ya hii nembo yanafanyika, bahati nzuri kapewa tena kazi yeye huyu mchoraji unaona bado tunamuhitaijia. Sasa kama bado tunamhitaji mimi ningeshauri sana serikali ikakaa naye, ikakubaliana naye na yeye akasema akatoa joto lake, jamani hii kazi inaumza kichwa na mimi nazeeka sasa siku nyingi, kwa hiyo na mimi nisaidieni hiki niendeshe maisha yangu, haitopendeza kwa kweli tukamfanya na yeye asikitike kwamba duh! yote niliyoifanyia serikali yangu imenitizama hivi!

Mwisho kabisa kwenye jadweli la pili Mheshimiwa ukurasa wa 242 chini ya kifungu cha 4 linasema Nembo ya Serikali ya Zanzibar. Mheshimiwa ni lazima tuite jina kikamilifu Nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Najua huku chini imesemwa lakini hapo juu imeanza Nembo ya Serikali ya Zanzibar, tuiweke kama ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huu mfupi naunga mkono hoja na kweli vielelezo hivi vitaonyesha kwamba Dola yetu ya Zanzibar ipo naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipatia fursa hii niweze kusema machache katika Mswada huu. Kwanza kabisa niwashukuru sana watendaji wetu wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuletea Mswada huu katika wakati muwafaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika kifungu namba 7 ambacho wenzangu wengi wamekizungumza na mimi ningependa nikitilie mkazo kifungu hichi. Kifungu kinaeleza naomba ninukuu,

> " 7. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo", mambo hapa yakaelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka tu nitoe ushauri kwa kweli lazima yale mambo au vikwazo vinavyoonekana hapa kutumia basi viainishwe ili wananchi wa Zanzibar waweze kupata fursa nzuri ya kutumia vifaa hivi Bendera yao, Nembo yao waweze kuitumia katika matumizi yenye maslahi, na tutakapoweka tu ni marufuku moja kwa moja kitendo hichi kitawanyima uzalendo wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu hivi ni vitu vya kujivunia katika utaifa wake mtu, kwa hivyo ni vizuri tukaainisha ile mipaka ambayo itaonesha kwamba ukifanya hivi hili ni marufuku na hili litakuwa ni haki yako ya msingi kutumia.

Mhe. Mwenyeki, nikitoka katika kifungu hicho namba 7 nije katika kifungu namba 8(k) ambacho kinaonesha matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ambao utatumika katika skuli za umma na skuli binafsi. Mimi hapa naomba tuongeze na vyuo. Katika vyuo vyetu bado tupo na wale wale wanafunzi na hapo ndio wanaonekana kwamba ni wanafunzi wamekomaa sasa kiakili wanahitaji sana kuelewa zaidi wimbo wa taifa lao na kuuheshimu na kuuenzi. Kwa hivyo naomba neno vyuo nalo liwepo ili huu wimbo wetu wa taifa uweze kuwepo katika maskuli yetu ya umma na binafsi lakini na vyuo vyetu vyote ambavyo vinahusu taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu 8(n) ambacho kinaonesha nusu mlingoti. Kifungu hiki ningeomba iainishwe katika kanuni siku zile ambazo itatokea dharura ya kupepea bendera nusu mlingoti kama zitakuwa tatu au zitakuwa saba au itakuwa mwezi, lakini iainishwe katika Kanuni ili kuja kuchelea wale

ambao watakuja kujisahau wakaweza kuiacha tu ile bendera yetu inaendelea tu kuwa nusu mlingoti kwa siku ambazo hazina idadi. Sasa tukiifunga katika kanuni watu wataweza kuelewa kama hapa siku zilizoainishwa ni tatu au saba au mwezi. Matumizi hayo yaje yatumike vizuri na isije ikawa kiholela.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kifungu namba 8(o) ambacho hichi kinaeleza uchapishaji na uuzaji. Mimi nilikuwa nataka nishauri na ndio pale nilipokuwa naanza kusema mwanzo kama tutakuwa tumewakosesha watu uzalendo wa kutumia vifaa hivyo. Nashauri kuwa na chombo maalum ambacho kitashughulikia utoaji wa leseni au kibali au tozo yoyote ambayo yaweza kutumika matumizi haya ya Bendera au Nembo kwa kupitia mavazi, tunajua kwamba huwa tunatumia bendera hizi katika kanga ni ufanyaji wa biashara. Sasa hicho chombo ndio kitaweza kuwaeleza vizuri wale watumiaji ili waweze kutumia vizuri vifaa hivi na visipatikane katika uharibifu. Hapa serikali pia itaweza kuingiza mapato kupitia suala hili. Lazima watu watatumia vitu hivi lakini na serikali itakuwa inaingiza mapato.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kifungu cha 9. Kifungu hichi kimeonesha uwezo wa Waziri. Mhe. Mwenyekiti, uwezo hapa aliyopewa Waziri ni uwezo mkubwa na tunaogopa yasije yakatokea yale maslahi binafsi, kwa sababu kuna mfungamano wa kifungu hichi namba 9 na kifungu namba 7. Kifungu namba 7 kimeeleza marufuku lakini kifungu namba 9 kimekuja kumpa Waziri uwezo wa kusamehe. Sasa hapa tusije tukafanya kosa la kuona kwamba Waziri atakuwa yuko huru hili kuweza kulifanya peke yake. Naomba maamuzi ya BLM yapatikane ili kuweza kuondosha ubinafsi wa mtu, huu uwezo aliyopewa Waziri aweze kupata ushauri kule BLM afanye nini likitokea suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu sio mkubwa ni mdogo kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia na wameshaeleza lakini pia nilikuwa naomba Mswada huu tutakapoupitisha hapa na *in shaa Allah* utapita kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Ninachoomba Serikali ijitahidi kutoa elimu ya kutosha kwa sababu matumizi ya Nembo na Bendera na Wimbo ni vitu muhimu sana katika taifa letu. Hivyo kuweza kuwekwa vipindi maalum ambavyo vitakuwa vinapatikana katika redio, televisheni au vijarida mbali mbali ili watu wetu waweze kupata taaluma ya kutosha wasije wakaingia katika makosa ambayo yamo katika haki zao za msingi za matumizi. Kwa hivyo naomba sana Serikali iweze kutoa elimu, kwa sababu watu kama tunavyoelewa sio waelewa sana wa sheria. Kwa hivyo ni vizuri kwa jambo hili la kitaifa ambalo wao wana manufaa nalo kwa hivyo waweze kupewa elimu ya kutosha, kuwekwe vipindi ambavyo vitaweza kusaidia kupata elimu hii ili wapate usahihi wa kutumia vyombo vyao hivi kwa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana mfupi tu na Waswahili wanasema uliza ujinga upate werevu, nataka nifahamu na kuuliza si ujinga. Kutakuwa na wimbo wa Taifa Zanzibar huwa tunaulizwa uraia Mtanzania, utaifa Mtanzania, nataka nifahamishwe kidogo kwa lugha nyepesi hapa kidogo pamenichanganya ndio narudia ule msemo, uliza ujinga upate werevu. Hapa nataka nifahamishwe kidogo kwa lugha nyepesi kabisa hili ndio nililoliona mimi. Elimu yangu ni ndogo lazima nikiri Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri ndio nikawa sijaupata Unaibu Waziri wala Uwaziri.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu namba 7 naomba nikinukuu Mhe. Mwenyekiti.

“Ni marufuku Mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo”.

Waheshimiwa Wajumbe wengi walipiga kelele suala hili na itakuwa ni aibu timu zetu za taifa zinapokwenda kuchukua bendera kuitangaza Zanzibar. Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Suleiman alilizungumza suala hili, tumeona wenzetu hata Kenya vibiriti vyao kutiwa nembo ya bendera. Kwa hivyo hapa watu wengi na wengi wapeni ninafikiri Serikali sikivu kwa hili wataliangalia. Lakini leo Waziri anakuwa na mamlaka ya kuhukumu tuiwachie Mahkama itakuwa Waziri kapewa nguvu katika kifungu namba 9.

Jambo jengine kifungu (f) kimetangaza kutumia nembo ya bendera na wimbo kama mapambo au mambo ya sanaa, tumeona wenzetu Wamasai na kutaja kabila si makosa wanatengeneza vile vitu bendera ya Tanzania rangi ya buluu na kijani, kama bangili zile wanatangaza. Mhe. Hassan kazungumza bendera tunatangaza biashara leo tunapiga kelele kuhusu utalii wetu, tutautangazaje utalii wetu bila kutia bendera. Kitu cha kusikitisha, mapambo tuyatie.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, chengine mambo ya *souvenir* yaachiwe. Hili nipendekeze kwa maoni yangu mimi na Waziri anaweza akayachukua au akayaacha njiani katika kutunga Kanuni, hii naomba vyama vya siasa tumeona juzi Marekani na hii italeta umoja. Vyama vya siasa vilivyokwenda bendera ya Zanzibar iwepo. Tumeona uchaguzi wa Marekani juzi hatukuona bendera za wapinzani mimi sijawahi kuziona, bendera ya nchi. Kwa hili pendekezo langu katika Kanuni atazozitunga Waziri bendera ya nchi iwepo, italeta kipa umbele.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, huu wimbo ningependekeza baada ya kama nitapata jawabu iwe Mapinduzi kutuletea, mapendekezo yangu kama nitapata jawabu la mwanzo niliilouliza badala ya sisi sote Jamhuri kutuletea iwe Mapinduzi kutuletea. Hayo ni maoni yangu Mhe. Mwenyekiti.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nitahitaji maelezo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia katika Mswada huu muhimu uliowasilishwa mbele yetu wa matumizi kuhusiana na mambo ya Bendera, Nembo na Wimbo wa Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu leo sina makubwa kwa sababu kuna watu wengi wamenifilisi na ndio kawaida ya kukaa mwisho. Mhe. Mwinyihaji Makame pale Mwenyekiti kanimaliza kwa hivyo sawa. Lakini ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Mswada huu umefika wakati muafaka tukizingatia kwamba nchi yetu inahitaji mabadiliko mengi kutokana na kasi ya maendeleo inayofuata. Nchi yetu imepiga hatua ya kimaendeleo, watu wamekuwa, idadi ya watu imeongezeka na vitu vingi vimeongezeka. Sasa kadri unavyoongeza idadi ya watu unaongeza idadi ya kipato na pia unaongeza idadi ya mahitaji mbali mbali likiwemo la sheria. Sheria tuliyokuwa nayo sisemi mimi kama ilikuwa ni mbaya ilikuwa ni nzuri lakini kwa sasa imefika wakati kwamba haikidhi haja na ndipo ikaonekana kwamba ipo haja sasa ya kufuta sheria na kutengeneza sheria mpya ambayo itaendana na kasi ya ulimwengu wa leo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na mambo ya bendera mabadiliko ya sheria hii na umuhimu wake wa kutunga Kanuni mimi nimeona iko haja, kwa sababu gani ya kuhofia kutumika vibaya kwa bendera yetu ambayo ndio utambulisho wa nchi yetu. Tutakapoiacha bendera hii kukawa hakuna sheria inayoilinda kwenye matumizi ni sawa sawa na tuliokuwa tunajidharau wenyewe. Kwa sababu watu ambao hawapendi maendeleo ya nchi hii ni wepesi kwao kama walivyosema wenzangu waliotangulia kuweza kuichukua na kuidhihaki bendera ya nchi ambayo ndio utambulisho wa nchi yetu. Kwa hivyo ili kuipa thamani bendera yetu mimi nilikuwa nashauri na ninasisitiza mambo yafuatayo:

Kwanza kuwepo na kanuni kama alivyopewa Waziri uwezo katika kifungu cha 8(1) kinachosomeka kwamba, "Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni ya masharti ya Sheria hii", na kwa sababu ya umuhimu wa sheria hii ili iweze kutekelezeka, namuomba Waziri punde

Mswada huu utakapokuwa sheria tutakapoupitisha na *inshaallah* tutaupitisha leo aharakishe kutunga Kanuni ambazo zitaongoza matumizi bora ya bendera yetu. Ndani ya Kanuni hizi nilikuwa napendekeza mimi nitaje, Kanuni ieleze ni muda gani tunaweza tukaitumia bendera. Tumeona kwamba baadhi ya bendera kwenye maofisi yetu kama walivyosema wenzangu zinawekwa mpaka zinachanika si jambo zuri. Sasa nilikuwa napendekeza kwamba matumizi ya benderea yatajwe kwenye Kanuni kwamba bendera itumike kama ni kwa kipindi cha miezi mitatu au miezi minne, au miezi sita ili kuhofia kuja kuchakaa kwa bendera ikaonekana kama bendera yetu imechakaa na hatimaye kuchanika chanika. Kwa hivyo, mimi napendekeza na ninamuomba sana Waziri wakati atakapotunga Kanuni ainishe kwenye Kanuni ni muda gani utakaotumika kwa bendera kwa kupachika. Kama itatumika kwa miezi mitatu au miezi minne au miezi mitano ikisha iseme kwamba zaidi ya muda huu ni marufuku kwa bendera kutumika, itatoa nafasi kwa watumishi wetu kuweza kujipanga kupata bendera mpya kila wakati bendera yetu ikaonekana kuwa bado ni nzuri, ni nzima inapendeza. Hilo la kwanza.

Pia kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba zamani bendera ilikuwa ikipachikwa na ikipachuliwa kulikuwa na alama maalumu inapigwa kama ni honi au kule kwetu sisi alisema Mhe. Mwinyihaji Malindi, N'gambu kule na kwengineko kulikuwa kuna king'ora lakini sisi kulikuwa hakuna ving'ora kwetu ilikuwa kunapigwa firimbi inaashiria kwamba sasa bendera inapachikwa au sasa bendera inapachuliwa. Sisi tunasimama na mpaka kile kitendo ima cha kupachika au cha kupachua kinamalizika ndio tunaruhusiwa kwenda zetu. Lakini sasa jambo lile limetoweka kabisa. Sasa kwenye sheria hii napendekeza wakati wa kutunga Kanuni napendekeza kwamba iwe ni miongoni mwa vipengele vya Kanuni, kwamba kwa yale maeneo ambayo yatapaswa kupachuliwa bendera, wapita njia kwa ile dakika moja mtu haiwezi kumzuilia kitu. Kwa sababu *just* dakika moja anasimama, bendera inapachikwa au inapachuliwa basi ikisha anaendelea na safari yake inaleta heshima. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama hatukuitungia Kanuni kwenye sheria jambo hili litaendelea kuwa hivyo hivyo.

Pia nimeiona katika bendera yetu hii kuna bendera ya Jamhuri ya Muungano mimi nafurahia sana na naomba sana hii bendera naiona imeweka *size* ya 48 chini kuna 8 kwengine kuna 2 sijui kama inawezekana kwa nini isiongezwe hapa juu kidogo ikakaa vizuri, ikaonekana zaidi maana yake na sisi tumo humu badala ya 48 angalau ikenda angalau 50 hapa lakini hatujui. Lakini pia kwenye hii kuna mistari. Mimi nilikuwa napendekeza katika bendera pia kuwepo na alama ya siri alama ambayo tutakuwa tunaijua wale watu maalum watakaopewa kazi ya kuchapisha bendera ambao pia napendekeza kwenye

Kanuni wapendekezwe kwamba bendera hizi washughulikiaji wa kutoa bendera hizi ni watu fulani au Wizara fulani na iwe ni marufuku kwa Wizara nyengine kwa mtu mwengine kutoa bendera, hii itatusaidia sisi kuchapisha ovyo bendera zetu na kuwapa mwanya watu wengine kuweza kutengeneza bendera.

Jambo hili pia sambamba na hili ambalo nalipendekeza kwenye nembo ya taifa, kwamba kwenye nembo ya taifa nako kuweko na alama maalum ya siri itakayowekwa kwa ajili ya kuihifadhi na kuilinda ile nembo ya taifa. Kwa sababu tumeonekana kwa sasa kuna watu wengi kutokana na teknolojia ya sasa ya kompyuta ilivyoingia watu wanaweza kubuni mambo mengi, watu wanaghushi hata nyaraka za Serikali na mambo mengine. Sasa napendekeza kuiwekea alama maalum kwenye nembo pamoja na hayo lakini iwepo alama ya siri hata ndogo ambayo wale watengenezaji wa zile nembo watakuwa wanaijua wao tu na si vibaya kwa yule mtengenezaji akalishwa kiapo cha kutunza siri ya alama za siri atakazoziweka kwenye nembo zetu. Kwa sababu hii ni moja ya utambulisho wa taifa, hii ni mali ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yameelezwa na wenzangu wameyasema mengi, lakini kuhusu nembo ya taifa wenzangu walipendekeza, lakini mimi napendekeza kwamba ni vizuri tukazitolea ufafanuzi zile alama zetu kwa sababu kwenye bendera tunaijua tumeiona, tunajua visiwa, maana yake nyeusi ni watu yaani Waafrika, kijani ni ardhi, bluu ni bahari na hapa hii bendera ya Jamhuri ya Muungano tayari imetiwa kwenye sheria ndio muungano wetu. Sasa na kwenye nembo yetu kuna mkarafuu, kuna mnazi, kuna visiwa viwili lakini kuna shoka na panga na hivi navyo ni vizuri ili vizazi vyetu wakaweza kuvitambua tukavijua hasa vikawekwa kwamba shoka au panga ndio asili ya mapinduzi au vipi itakavyotafsiriwa. Lakini ni vyema hizi silaha mbili zikatafsiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye Wimbo wa Taifa. Wimbo wa mashujaa wenzangu wengi wameuzungumza kwamba ni wimbo wetu wa mashujaa na kweli tunapendekeza uwe hivyo. Lakini pia nilikuwa na mapendekezo yangu nilikuwa naomba kwenye huu wimbo wa mashujaa ambao tunauomba hata kwenye sherehe zetu za kitaifa nimebaini kwamba watu wengi ule wimbo hawaujui, wanaitikia wanafuata zile ala zinazopigwa tu. Lakini nilikuwa na pendekezo langu moja tunapokuwa na sherehe zetu kama hivi kabla ya wale *brass band* kupiga ule wimbo au wale wageni wetu wanapoingia pale viwepo vipeperushi vitakavyoainisha ule wimbo utakaoeleza zile beti za ule wimbo, ili mtu kama haujui kwa moyo atakuwa na yeye anauimba pale. Kwanza itatoa

hamasa lakini pia itatoa uelewa kwa watu wengine kuufahamu wimbo wetu wa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya haya niliyoyazungumza mimi naungana na wenzangu wote waliotangulia kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na nawaomba Wawakilishi wenzangu tuupitishe Mswada huu ambao umekuja kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kuchangia Mswada huu muhimu sana katika nchi yetu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kufika hapa nikiwa na afya njema na kuweza kuchangia Mswada huu, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa utendaji wake mzuri kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria leo kwa umakini wake mkubwa sana.

Pia nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa umakini wake mkubwa na niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Mswada huu na mimi ni mjumbe wa Kamati hii. Kwa hivyo nawashukuru sana Mswada huu kuja wakati muafaka kabisa katika nchi yetu na jambo muhimu kama hili la bendera na wimbo wa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie hapa kidogo kwenye Mswada huu. Nashukuru sana Mswada huu kupitia Sheria Nam. 1 ya mwaka 1985 juu ya sheria hii ya Bendera ya Zanzibar na pia Nam. 12 ya 2004 na kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru Mswada huu umekuja wakati muafaka kuweka nafasi nzuri nchi yetu hasa katika mambo ya bendera ni utambulisho mkubwa kwa mataifa yote. Mhe. Mwenyekiti, mimi niaze hapa kuomba kujua na ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri kwa sheria hii imefuta Sheria Nam. 12 ya 2004, kwa hiyo inahitajika kifungu cha 1 cha Mswada huu wa sheria kieleze sheria hii ni ya mwaka gani? Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri utapokuja utanieleza kama ambavyo sheria hii ilivyofutwa ilivyoeleza katika kifungu kama hiki.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mswada huu kuhusu matumizi ya bendera na wimbo wa Taifa katika kifungu cha 6.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6 cha Mswada huu maneno ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria. Maneno haya naomba sana yaondoke na yasomeke kama maneno ambayo matumizi yake yameanishwa katika sheria au sheria nyengine yoyote. Nilikuwa naomba hivi vikwazo ambavyo kwa sheria hii viangaliwe sana kwa sababu haijawekwa vikwazo. Kwa hiyo naomba sana viwekwe vikwazo kwa Sheria Nam. 6, mwiko wake na mwisho wake.

Pia nije kwenye hoja ambayo ninaisema kwamba matumizi haya hayana vikwazo hayajatosheleza kimaana, lakini inapotumika maneno nilivyoeleza hapo juu tumeondoa utata kwa kutoathiri sheria na sheria nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme hapa kwa mfano sheria hii imesema tu lakini haijaweka ukomo wake wapi wa kutumia. Lakini mimi niseme kwa mfano tumetoka hapa kwenda nchi za nje na wasanii wetu au timu yetu ya mpira kwa mfano. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kujua Mhe. Mwenyekiti itakapofika kule timu kama ile kupeperusha bendera yetu ya Zanzibar na kama tunavyojua timu kama hizo mara nyingi zinapeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, kwa Sheria hii tutaweza kupeperusha bendera yetu ya Zanzibar ili tuweze kuitangaza nchi yetu kama vile wasanii wetu wanapokwenda nje au mambo mengine tofauti tofauti. Kwa hivyo, naomba kidogo maelezo Mhe. Waziri unieleze.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye kifungu cha 7 cha Sheria hii, naomba kiongezwe kifungu kidogo cha (2) kisomeke “isipokuwa kwa pale mara ambapo yatakuwa ni faida kwa Taifa la Zanzibar”.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano kwa sababu matumizi haya katika kifungu hiki cha 7, kinazungumzia matumizi lakini kwa mfano kwa manufaa ya Taifa la Zanzibar. Kwa mfano, maonesho ya kibiashara wananchi wetu walipokwenda Brazil au Ujerumani au sehemu mbali mbali jee, kama wakienda kule kwa Sheria hii wataruhusiwa kupeperusha Bendera ya Zanzibar kwa ajili ya maonesho ili kuweza kuitangaza Zanzibar, hasa ukitazama kwamba maonesho mengi yanayofanyika wajasiriamali wanakwenda wanatangaza biashara zetu kama karafuu, mafuta ya nazi na *spices* zetu, kutangaza utalii. Kwa hivyo, naomba kujua Sheria hii na kutumia bendera yetu kwenye sehemu kama hizi, nilikuwa naomba kujua maonesho hayo yataruhusiwa ili kuweza kufaidisha nchi yetu katika mambo mbali mbali ya kuitangaza Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwenye kifungu cha 8 "matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika skuli za

umma, skuli za binafsi". Hili ni jambo zuri na sisi tulipokuwa tunasoma Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa wimbo wa Taifa lazima asubuhi uimbwe kila siku, wimbo wa Taifa ni tunu kusomwa katika maskuli. Lakini kwa muda huu mkubwa sana hasa skuli za binafsi imekuwa wimbo huo wameuacha. Kwa hivyo, naomba msisitizo mkubwa na sheria iwe kali kila skuli lazima wimbo huu watoto waimbe, kwa sababu watoto watakapoimba watapata kujua akilini historia na wimbo wa Taifa letu wapate kuujua kama sisi tulipokuwa wadogo ilikuwa wimbo huu tunaimba kila siku asubuhi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba hili ni kama ombi liongezwe wimbo wetu wa mashujaa. Wimbo wa mashujaa tulikuwa tunaimba pia tulipokuwa wadogo maskulini na ulikuwa una *message* kubwa, unafahamisha mambo mengi sana ya Mapinduzi yetu hata kuwafariji wale mashujaa waliopindua nchi hii. Kwa hivyo, mimi naomba wimbo ule pia ungetiwa kwenye Sheria hii au Kanuni yoyote maskuli pia wakaaza kuimba, baada ya wimbo wa Taifa ukaimbwa wimbo huo, na hiyo ikawa ni lazima kila skuli waimbe kama sisi tulivyokuwa wadogo tulikuwa tunaimba wimbo huu, basi na wao watoto wa sasa hivi waanze kuimba kwa sababu wapate historia ya kujua kama nchi hii imetokea wapi na kuna watu waliikomboa nchi hii hata kufikia hapa.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuongeze wimbo huu wa mashujaa uimbwe maskulini ili tuweze kufaidisha watoto wetu wadogo hata kwenye televisheni yetu ya *ZBC* imekuwa sasa hivi wimbo ule kuupiga kuna kama aibu fulani wanaona, au sijui kuna nini sielewi. Kwa nini wimbo ule usiwe kila siku maalum ukawa unapigwa ili kutukumbusha wale wazee wetu waliofanya kazi kubwa katika nchi hii. Ule wimbo una *message* kubwa na ni mzuri sana hata wasanii wetu tuwe tunawafanyia Mhe. Waziri wa Habari pia afanye kama *remix* wimbo huo iwe ni nyimbo ya kisasa kabisa iweze kupigwa sehemu nyingi katika nchi yetu Zanzibar na Taifa zima kwa ujumla. Kwa hivyo, naomba sana wimbo ule utoe msisitizo kuanzia skuli pia kwenye *media* zetu ziweze kupigwa wimbo huo kwa kila siku kwenye TV zetu tuwe tunauona na ufanyiwe *recording* kabisa mpaka *video* kabisa ili tuweze kufaidika na wimbo huo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe sana Serikali huu Mswada ni mzuri na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia sina matatizo nao, kwa sababu suala la bendera na suala la nembo kwa kweli hili ni jambo zuri kwa Taifa la Zanzibar, kwani kila mtu anatakiwa aringie utaifa wake, hata Waswahili wanasema “Mkataa kwao mtumwa”. Kwa hivyo, wimbo huu na bendera mimi napongeza na Mswada huu mzuri umekuja muafaka na naunga mkono asilimia mia, mimi na Kamati yangu sina mashaka nao kabisa. Lakini niiombe Serikali itizame

vizuri na kwa uwazi juu ya matumizi mazuri ya bendera iangalie sana matumizi mazuri yako wapi. Kama matumizi mazuri yanatakiwa basi yatumike vizuri na kama utakuwa makatazo ya bendera na wimbo wa Taifa pamoja na nembo haya mambo yaangaliwe sana na serikali na yatiliwe mkazo kwani hili jambo sio la masihara ni jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano nimuombe Mhe. Waziri atupe ufafanuzi kama mtu anapenda kuvaa bendera yake kama vile *T-shirt* ya bendera ya Zanzibar, hilo jambo zuri kwani unatangaza Zanzibar yetu. Kama kutakuwa na jambo kama hilo zuri basi naomba na wananchi wapate uelewa wa jambo hili kwani sio baya, na kama wametumia bendera vibaya basi mimi naomba Mhe. Waziri hatua kali zichukuliwe na serikali yetu naiomba isimamie vizuri sana suala hili la bendera na nembo na wimbo huu uwe makini kwa kulindwa na hadhi yake. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti hili suala litiliwe mkazo sana kwa ajili ya kuipa heshima yake bendera, wimbo na nembo yetu kwa ajili ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya mchango wangu sio mkubwa naunga mkono asilimia mia kwa mia.(*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu ambao umekuja mbele yetu.

Kwanza kabisa naipongeza wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1986. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza kabisa nichangie katika kifungu hiki Nam. 6.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kimegusiwa sana lakini na mimi katika *point* yangu nakigusia. Kifungu hiki kimeeleza kwamba. “Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar vitatumika katika maeneo ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria”.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, vikwazo gani naona hawakuanisha ilikuwa watuwekee vikwazo ili tuvijue ni vikwazo gani vinavyohusiana na hayo. Na vile vile vikwazo kwa mujibu wa Kanuni ilikuwa iwekwe hapa kwa mujibu wa Kanuni na Sheria na sio kwa mujibu wa sheria. Mhe. Mwenyekiti, kipengele hiki napendekeza kiwe hivi “kwa mujibu wa Kanuni na Sheria”.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika kifungu hiki cha 7, ukurasa wa 2 ambavyo vingi vimegusiwa lakini na mimi nagusia. “Ni marufuku kwa Mtu

yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo".

Mambo haya tumeanishiwa lakini na mimi nagusia kuhusiana na mambo ya biashara, kwa sababu wengi wa Wazanzibari ni wafanyabiashara na wengine mapendekezo yao nikiweka bendera hii ya Zanzibar ndio kitambulisho chake cha biashara yake. Kwa hivyo, napendekeza kwamba haya marufuku ilikuwa yawe na mipaka fulani, kwa sababu hawa wafanyabiashara nao walikuwa wanataka kuitumia bendera yao kwa biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 7(f) kama mapambo au mambo ya sanaa. Mhe. Mwenyekiti, wengi wao wanataka kuitumia bendera hii pengine kwenye maofisi au kwenye majumba yao na hata pia kwenye magari. Ni vizuri sana tungeekewa haya marufuku yangekuwa na mipaka kwani wengine wanataka kutumia kwenye mapambo ya magari yao ama nyumba zao kwa ajili ya kuitumia bendera yao ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwenye kifungu hiki cha 8(e) "Nidhamu na heshima ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa". Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki kuwe na chombo maalum cha utengenezaji ili kuepusha utofauti wa rangi na utofauti wa ile *quality* ya bendera yenyewe. Kwa hivyo, napendekeza kwenye kifungu hiki kuwe na chombo maalum cha kutengeneza hizi bendera ili kutofautiana rangi pamoja na *quality* ya kitambaa kinachotaka kutengenezewa Bendera yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kuhusiana na huu wimbo wetu wa Taifa, Nembo ya Serikali na Bendera ya Zanzibar. Kwa hiyo, ningependekeza iingizwe katika mitaala ya skuli za maandalizi, msingi pamoja na sekondari. Wimbo wa Taifa pamoja na Nembo ya Serikali unapoingizwa kwenye maskuli yetu wanafunzi wa maandalizi wanapata kuutambua na wanapata kuelewa vizuri bendera yao pamoja na ule wimbo unapoimbwa utakapokuwa kwenye mitaala yao ya skuli nadhani wanafunzi hawa kuanzia msingi watafahamu nini dhamira iliyokusudiwa kwa wimbo huu wa Taifa, Bendera pamoja na Nembo ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wameelezea kuhusu huu wimbo wa sisi sote tumegomboka, na mimi napenda kusisitiza kwa sababu wimbo huu ukiwekwa kwenye maskuli yetu unapoimbwa wewe mwenyewe kwanza utajiuliza au utajitafakari unahusiana na nini. Kwa kweli wanafunzi pale wanapokuwa wadogo wakiusikia wimbo huu wanajiuliza, natoa mfano hata mimi mtoto wangu sasa hivi katika skuli yao ya Kizimbani huu wimbo unaimbwa alinifuata

akaniambia mama nifahamishe huu wimbo. Kwa hivyo, nadhani wimbo huu wakiupata hawa wanafunzi wadogo wataelewa na wataona kwamba dhamira ya serikali ya kuweka wimbo huu unahusiana na nini? Ni kwamba unahusiana na mashujaa wetu ambao wamepagania nchi yetu hadi kufikia hapa. Kwa hivyo, napendekeza wimbo huu ungewekwa kwenye Mswada huu ili kuonekana kwamba una umuhimu kiasi gani kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi michango yangu ni michache kabisa lakini namalizia kwenye kifungu hiki hiki cha 8(p). Kwenye kifungu hiki nataka ufafanuzi wa uondoshaji, kwa sababu haukufafanuliwa kwamba uondoshaji nini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kwa hayo machache naunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji ni wengi naona wanazidi kujitokeza lakini nilikuwa nawaomba sana wale ambao watakuwa sijawataja hapa waandike michango yao kwa maandishi na wampelekee Waziri moja kwa moja. Ahsanteni. Ananyefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu unaohusiana na masuala ya Bendera, Nembo pamoja na Wimbo wa Taifa letu tukufu la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri lakini pia na Kamati na Wajumbe wengi mbali mbali ambao wamechangia vizuri na kwa ufasaha juu ya mswada huu muhimu. Nimpongeze sana Mhe. Omar ingawa hayupo kwa sababu aliniomba nisichangie mpaka yeye achangie ili nisimnyime *point* zake na ndio maana nikaona leo nikae mwisho, mwisho. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kuuchangia Mswada huu kwanza niseme tu kwamba kwa ufupi Serikali tumechelewa kuuleta Mswada huu. Kwanza kuna suala la wimbo wa taifa ambalo lilikuwa halipo kwenye sheria, lakini vile vile kuwepo kwa sheria mbili ya nembo na ile ya bendera. Kwa kweli tumechelewa kidogo lakini nafikiri sasa tunaanza ukurasa mpya.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyoelewa kwamba vitu hivi vitatu ni sehemu ya vitu vya kisanaa na kama ni vitu vya kisanaa maana yake uzuri wake viwe katika hakimiliki. Sina hakika lakini nina asilimia kubwa kwamba serikali ina hakimiliki ya vitu hivi. Lakini ningependa Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutwambia kama serikali ina hakimiliki ya vitu hivi na tumeshuhudia makosa mbali mbali yakifanywa kuhusiana na hivi vitu, ni kesi ngapi ziliripotiwa

zinazohusiana na matumizi mabaya ya nembo, wimbo wa taifa na bendera kama hakimiliki ipo, ukiacha kuwepo kwa sheria.

La pili, nije katika Mswada wenyewe, kwenye Sehemu ya Pili ukurasa wa 238, kifungu cha 4 napenda nikinukuu,

Kifungu cha 4 kinasema kwamba:

"Kutakuwa na Nembo ya Serikali kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984".

Lakini tukienda katika Katiba yenyewe katika kifungu hicho kinasomeka hivi:

"Kutakuwa na Muhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao alama yake itakuwa kama itavyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Mwenyekiti, hapa ninapata kigugumizi, huku kuna nembo ya serikali, huku kuna muhuri wa serikali, vitu hivi naona kama ni vitu viwili tofauti. Kwa hivyo, ningependa Mhe. Waziri atakapokuja atuwekee wazi juu ya hiki kilichonukuliwa katika Mswada na hiki kilichoko katika Katiba ni vitu sawa au kama ninavyoviona mimi ni vitu viwili tofauti, kama ni vitu viwili tofauti basi turekebishe katika kifungu chetu cha Mswada kwa sababu hivi sasa si wakati wa kurekebisha sheria, wakati wa kurekebisha Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo ambalo naliona nalo lina uzito wake ili tuepuke kugongana katika Mswada huu wa Sheria na Katiba yetu ya Serikali ya Mapinduzi, sasa nije katika kukazia kazia katika yale ambayo wenzangu pengine wamechangia.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7 cha Mswada huu kimezungumzia marufuku na wenzangu wengi wameweza kuchangia suala hili. Pamoja na malengo mengine ya vitambulisho hivi au vielelezo hivi vya taifa, lakini jengine kubwa zaidi vitu hivi vinajenga uzalendo, vinajenga fahari lakini vile vile ni tunu kwa wananchi wa Zanzibar. Sasa tunapoweka marufuku maana yake tutakuwa tunashindwa kuweza kujenga uzalendo, fahari na tunu ya vitu hivi. Kwa hivyo, ningependa sana kifungu hiki kama walivyotangulia wenzangu kitazamwe upya ili kuweza kutoa mwanya vile vile wa lengo hili nalo kutekelezeka, tuweke marufuku lakini vile vile kuwe na mlango mwengine kwa wale ambao watataka kuweza kuvitumia hata kama kwa njia ya tozo lakini iweze kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kwa mfano kuweka bendera kama pambo ndani ya gari yangu ile ni fahari, sasa utakapopiga marufuku sijui ufahari huo utapatikana wapi. Kwa wenzetu vile vile bendera zinatumika hata na wananchi katika kupeperusha katika nyumba zao, nchi kama za Scandinavia hili ni jambo la kawaida kuona nyumba ya raia inapepea bendera. Sasa vitu kama hivi unapoanza kupiga marufuku mimi nafikiri huwezi ukajenga uzalendo, mapenzi na ule ufahari wa mwananchi katika nchi yake. Kwa hiyo, tulitizame vizuri suala hili la kifungu cha 7.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la ukubwa kifungu cha 8(2)(a) suala la ukubwa na vipimo au ya vipimo. Mheshimiwa kama tutaamua tuwe na aina mbali mbali za bendera kwa mujibu wa *size,* tutakapoweka *size* hii ambayo tumeipendekeza kwa mujibu wa kitambulisho au kielelezo ambacho kinajionesha kwenye jedwali itakuwa tumejifunga.

Mhe. Mwenyekiti, vipimo ambavyo vimeainishwa ni vipimo ambavyo vinahusiana na bendera kubwa tu ambazo zinatumika katika maofisi ya serikali. Lakini kama tutakuwa na *size* tofauti za bendera kutegemeana na matumizi basi utakuta kwamba vipimo hivyo tulivyoviweka hapo itakuwa havina uzito. Aidha, katika Kanuni ambazo tutazitunga basi ziweze kutazama zile *size* ambazo tutakubaliana. Kuna *size* za bendera ambazo zinapepea katika ofisi zetu za Serikali ambazo zinakaa juu ya meza, zile ni bendera ndogo. Je, *size* itakuwa ni hiyo hiyo, lakini tuna bendera ambazo kama tutakubaliana za mapambo, kutakuwa na bendera pengine kama tutakubaliana hata raia waruhusiwe basi tunaweza pia tukawa na *size* tofauti. Kwa hivyo, suala hili la ukubwa wa vipimo lisitazame tu zile bendera ambazo zinawekwa katika ofisi za Serikali, lakini vile vile na zile ambazo tunaweza tukakubaliana ambazo zinaweza zikaendelea kujenga uzalendo na kujenga ufahari wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala la nidhamu, kifungu cha 8(2)(e). Nidhamu na heshima ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa. Wenzangu wamezungumza sana juu ya suala hili la nidhamu, ukweli kuna wakati mwengine nidhamu ya vitu hivi inakuwa inaondoka, nidhamu itakapokuwa kuna fursa au wajanja fulani wanatumia kuzitengeneza hizi bendera hapo nidhamu itaondoka kwa sababu *size* zinaweza zikawa tofauti, lakini hata hizi rangi zinaweza kupishana manjano ile tuliyokubaliana atakayetengeneza mwengine bila ya idhini maana yake anaweza akaleta manjano nyengine, buluu nyengine au kijani nyengine. Sasa hapa utakuta kwamba nidhamu inaweza ikaondoka katika bendera hizi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunavyozungumza kuna watu mbali mbali ambao wanatengeneza hizi bendera, kwa sababu inawezekana hakuna kitengo maalum ambacho watu wanajua hasa kwamba nikienda ofisi fulani nitainunua bendera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa hii italeta mianya itakapokuwa hakuna kitengo maalum. Hapa ninashauri kwamba serikali lazima iwe na kitengo maalum ambacho kitakuwa kinasimamia uchapishaji na uzalishaji ambapo hii ndio itaweza kulinda nidhamu ya vitu hivi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wakati mwengine nidhamu hizi tunaziharibu wenyewe katika Taasisi za Serikali. Nimeshuhudia baadhi ya taasisi za Serikali zinapokuwa na maadhimisho ya sherehe mbali mbali huwa zinafungwa mabango katika mabarabara yetu na mabango yale wakati mwengine yana nembo za serikali, lakini utakuta bango na sherehe ishamaliza, bango lile linaendelea kuwepo mpaka linachanika pale pale na lina nembo ya serikali. Sasa hii nidhamu itakuwa haipo, kwanza maudhui ya ile sherehe itakuwa ishapita lakini vile vile kubaki nembo pale kwa muda mrefu maana yake hatuitendei haki hiyo nembo. Kwa hivyo, ningependa sana Mhe. Mwenyekiti, katika hili tuwe makini katika kuangalia nidhamu juu ya vitu hivi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nisisitize kidogo tu katika suala zima la matumizi ya wimbo wa taifa katika skuli zetu. Msisitizo ni kwamba ni vizuri sana kurejesha ile hali ambayo ilikuwepo zamani. Mimi nakumbuka miaka ya 1970 alikuwa amepita mtu mmoja ambaye aliandaliwa vizuri sana kuweza kupita skuli hadi skuli kuweza kuimbisha wimbo, nakumbuka ulikuwa unaitwa Kinate.

(Hapa Mhe. Mjumbe aliimba wimbo huo)

"Kinate kinanguruma, kinate hicho kinanguruma". (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mpaka nimemaliza sikuwahi kufahamu hasa maana ya Kinate kinanguruma. Sasa nafikiri umefika wakati watafutwe vijana wapite skuli wakafundishe hasa huu wimbo wa taifa na wimbo wa mashujaa. Kwa sababu ile Kinate mimi sikuifahamu maana yake mpaka hii leo, sasa tutilie mkazo kitu ambacho kina manufaa kwa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisisitize tu elimu iendelee kutolewa kwanza juu ya sheria hii, kwa sababu sheria hii ina wadau mbali mbali na hivi sasa umefika wakati wa kutolewa elimu kama alivyosisitiza Mhe. Panya Ali Abdalla kwamba elimu itolewe ili kuweza kuona kwamba wananchi wengi zaidi wanapata umuhimu wa vitu hivi ili viweze kutumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi niungane na wenzangu na niwashauri wenzangu wengine tuunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia Mswada huu muhimu kabisa kwa ustawi na maendeleo ya vijana wetu. Katika michango mbali mbali imetajwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba itakuwa na nafasi muhimu sana katika kujenga na kutumia na kuimarisha uzalendo kwa kuwafunza vijana tokea skuli za msingi hadi Vyuo Vikuu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hivi sasa wizara inaendelea na juhudi hizo za kufufua matumizi ya wimbo wa taifa pamoja na wimbo wa mashujaa. Hivi sasa pia wizara karibuni imeunda kamati maalum ambayo itapita katika skuli zetu kwa ajili ya kufundisha wimbo kwa sauti yake na haiba na mitindo yake, timu hiyo itaunganisha watu mbali mbali wakiwemo watu wa vikosi na watu wengineo, pia watajumuika katika kamati hiyo ambayo wizara imeunda. Kwa hivyo, kuwepo kwa Sheria hii kutatupa nguvu zaidi ya kufanya kazi, lakini tayari sasa tumefanya kazi hiyo na ina changamoto tunapambana nazo lakini zinakwenda hatua kwa hatua ili kuona jambo hili linafahamika.

Mhe. Mwenyekiti, tunafanya hivyo kwa kuelewa kwamba mambo haya matatu ambayo tunayazungumza sasa hivi, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, ni mambo muhimu sana kwa nchi yoyote. Baadhi ya watu wanaweza kudhani labda haya tunayoyafanya yanahusu Zanzibar hata, haya yako katika mataifa yote na nchi zote duniani. Kwa hivyo, nataka niseme kwamba nyimbo hizi na mambo mengine yote haya matatu yataelekezwa pamoja na wanafunzi kufahamu maudhui yake, tofauti kidogo alivyozungumza mtangulizi wangu hapa sasa hivi anasema Kinate mpaka leo hakuijua maana yake. Hivyo sisi hatutotumia mtindo ule, tutajaribu kuwaeleza wanafunzi pia waelewe maana yake na kwa maana hiyo tutakuwa tunawasomesha historia waelewe nchi inatoka wapi, lakini pia waelewe umuhimu wa kulinda na kutetea nchi, pia waone fahari wajifaharishe kwa nchi yao wasione aibu. Kwa hivyo, mambo hayo tutayatilia mkazo katika utekelezaji wa jambo hili wakati wa kupitishwa sheria, lakini hata kabla ya kupitishwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kuzungumza jambo jengine kwamba mambo haya yasichukuliwe tu kama ni nyimbo kama alivyosema mwenzangu mmoja hii ni sanaa. Kwa hivyo, na maudhui yake mengi na maudhui hayo kwa upamoja wake inasaidia sana kujenga, si uzalendo peke yake lakini pia kujenga

uraia. Kipimo kimoja cha uraia ni kuheshimu nembo za taifa lako, ni kuheshimu wimbo wa taifa lakini pia na kuheshimu nyimbo mashuhuri au tunaita nyimbo za mashujaa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba nilimsikia siku moja Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwamba, mara nyingi likija suala zito ametingwa kurudia skuli kidogo kujikumbusha na mimi nimerudi skuli kujikumbusha juu ya jambo hili. Nimefungua vitabu kuona wenzetu wanafanya nini, nimeona katika nchi moja ambayo inaitwa Ureno au Kiingereza wanaita Portugal na wao pia wanao wimbo wa ukombozi. Sababu ya kuwepo nyimbo hii ni kwamba inafanana na kwetu baada ya kuondosha ule utawala wa kidikteta Antonym of Salsa basi wakaona lazima nyimbo ambayo ilitoa mchango mkubwa katika Mapinduzi yale iendelee kutumika na kwa bahati nzuri inaendelea kutumika hadi leo. Nyimbo hiyo na mimi pia nimeikariri nitasema maneno mawili matatu tu nyimbo ya Kireno inasema:

(Hapa Mhe. Mjumbe aliimba wimbo wa Kireno ufuatao:)

"Grandola vila moreno, terra da fraternidade" (Makofi)

Mhe. Mwenyekiti, ni nyimbo ambayo umuhimu wake ni kwamba ilisaidia katika kujenga muamko wa mapinduzi, nyimbo ilikuwepo kabla lakini ilisaidia kufanya hivyo. Kwa hivyo, wanaendelea kuitumia hadi hii leo na matumizi yao yanafanana na sisi, katika ile siku ya Mapinduzi yao Tarehe 25, Aprili huwa inaimbwa sana kama tunavyofanya sisi siku ya Mapinduzi huwa tunaitumia sana. Kwa hivyo, nataka niseme kwamba nyimbo hizi ziko katika mataifa mbali mbali na zinatumika kwa uzito wake na kwa fahari kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulisema nije katika matumizi ya bendera. Nadhani hili ama kupitia Kanuni au kupitia miongozo liwekwe sawa sana. Kwa sababu katika Ofisi za Serikali ziko nyingi hasa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tuna skuli nyingi, iwekwe wazi pengine skuli gani zitaweza kutumia bendera. Hivi sasa hakuna maelekezo maalum na ndio utakuta baadhi ya skuli kuna bendera baadhi hazina hatukujua kwa vigezo gani, utakuta labda Lumumba kuna bendera lakini ukienda skuli nyengine yenye hadhi kama ile ya Lumumba kama Sekondari *Advance* hakuna bendera. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu kuweka taratibu baadae za kutumia bendera hizi hasa katika taasisi hizi za elimu ambapo tunazo nyingi mno.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulichangia zaidi ni suala hili kwa kuwa mimi natoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini pia ni

mwalimu kuingizwa katika mitaala yetu katika madarasa mbali mbali. Haya na mimi pia baada ya kurudi skuli kufungua vitabu nimeyaona, katika Vyuo Vikuu pia nyimbo hizi zinasomeshwa katika ngazi za kitaalamu katika uchambuzi wake ili zifahamike. Kwa hivyo, na sisi si vibaya tukafanya hivyo lakini pia zinatumika kwa wageni. Wageni wanapofika katika Vyuo Vikuu vile basi jambo la mwanzo wanalofundishwa ni nyimbo za taifa na nyimbo mashuhuri katika nchi ile, utaimba tu hata kama lugha unaifahamu au huifahamu lakini utaimba. Mhe. Mwenyekiti, na sisi kwa bahati nzuri katika Chuo Kikuu cha Taifa tunapokea wageni pia huwa tunawaimbisha hizi nyimbo za taifa letu, wanaimba lakini pia baadae huwa tunawafafanulia maana yake. Kwa hivyo, ningependa pia suala hili tuliingize katika mitaala yetu.

Jambo jengine muhimu kabisa Mwenyekiti nadhani sasa tuanze kujenga tabia za kuelimishana, kufundishana na kukumbushana umuhimu wa mambo haya matatu ambayo tunayazungumza leo. Kuna baadhi yetu hatuyaelewi, kuna baadhi yetu tumesahau, tunaelewa lakini tumesahau. Kwa hivyo ni vyema tukachukua juhudi hii ya kuelimishana. Sheria nzuri kabisa ni ile ambayo baada ya kupitishwa kwake wananchi wake wanaelimishwa nayo, kwa hivyo baada ya kupitisha sheria hii tutumie fursa hiyo sote kuwaelimisha wananchi wetu juu ya haya mambo matatu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia jambo jengine ambalo ni muhimu sana kwamba kuanzia sasa tujenge desturi ya kuthamini vyetu mpaka tusahau vya wenzetu, kwa lugha nyengine lazima mambo haya matatu yasidhihakiwe, tusifanye dhihaka juu ya mambo haya. Wenzetu katika nchi nyengine wanathamini sana mambo haya na sisi tusifanye dhihaka na si lazima sana kutumia kanuni na sheria lakini tuendelee kuelimishana nadhani itafika wakati tutaelewa. Kwa hivyo, ni muhimu sana mambo haya kuyazingatia sana. Kuna mambo mengine nadhani imefika wakati ili kuwa na msimamo wa pamoja wa kitaifa mambo mengine muhimu ya kitaifa ni muhimu kuingizwa katika katiba, sizungumzi leo lakini hapo baadae tuyatafakari, yale muhimu yenye maslahi ya taifa ni vyema yakaingizwa katika Katiba ili kila atakayekuja ayaheshimu mambo kama hayo.

Jengine kuna mchangiaji mmoja alizungumza ambaye na mimi nataka nimuunge mkono kwamba ni muhimu kuongeza mawanda ya matumizi ya mambo haya ambayo tunayataja leo, nembo, wimbo wa taifa na wimbo mashuhuri. Kwa sababu mambo haya tunayatumika katika kujenga uzalendo, kuonesha historia ya jamii, tukibana bana sana lile lengo letu huenda lisifikiwe. Hata hivyo, katika kuongeza mawanda lazima tuwe makini, wakati gani, mahali gani na muda gani; lakini ni vyema kuwa na aina fulani ya matumizi

zaidi kuliko kujibana sana, tukijibana sana lile lengo letu la kuwafikia wananchi wetu kuelewa mambo ya historia na nchi yao na thamani itakosekana. Kwa maana hiyo, kile kifungu cha marufuku inabidi kitizamwe upya. Kutizama kwa maana kwamba si sawa sana kuweka katika kapu moja mambo haya yaweza kutofautiana katika matumizi yake. Nembo inaweza kuwa na mawanda yake maalum, wimbo wa taifa mawanda yake maalum na nyimbo ya ukombozi mawanda yake maalum, tukiweka katika kapu moja tukaweka marufuku moja tunaziathiri nyengine. Kwa hivyo, nadhani kama tutaweka marufuku basi twende kwa vifungu nembo ya serikali marufuku yake haya, wimbo wa taifa huu nao, tukichanganya pamoja tunaweza kuathiri na lile lengo letu hasa la msingi la kujenga uzalendo itakuwa vigumu kuweza kulifikia. *(Makofi)*

Suala jengine nimeshalisema hapo mwanzo lakini ni suala la uwezo wa waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wetu umekwisha lakini malizia nakuongeza dakika moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante, ni kwamba uwezo wa waziri kuweza kusamehe si jambo jipya ndugu wawakilishi tuelewe zimo katika sheria zetu mbali mbali. Kwa mfano katika ile sheria ya fedha waziri ana uwezo wa kusamehe kodi ambapo kwa maoni yangu ni jambo kubwa sana na kusamehe kwake pia kuna utaratibu wake. Huyu waziri pia anayeshughulika na suala hili naye pia kutakuwa na taratibu zake za kusamehe si kwamba anasamehe hivi hivi. Kwa hivyo, tuelewe kwamba tukianza kutia shaka na utendaji wa ofisi hii nadhani wakati tunatia shaka na Wizara ya Fedha na Mipango kwa nini wana uwezo wa kusamehe.

Baada ya kusema hayo labda nilimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilima mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi kwanza niwapongeze wachangiaji wote ambao wamechangia katika mswada huu, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea mswada huu, mswada ambao ni wa kujenga na kuleta maslahi ya taifa letu. Pia nimpongeze Mhe. Waziri toka jana mswada wake umepata wachangiaji wengi sana na hii ni kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wanataka kuona mabadiliko katika miswada hii iliyoletwa na *In shaa Allah* tukijaaliwa kesho tutampisha Naibu Waziri na

Waziri mwenyewe husika kufanya majumuisho ili tupitishe mswada huu na kuwa sheria.

Kwa hivyo, nawatakia kila la kheri na naakhirisha kikao hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 Kikao kiliakhirishwa hadi
tarehe 17/02/2017 saa 3:00 asubuhi)